

## **SURA YA 16**

---

### **KANUNI YA ADHABU**

**[SHERIA KUU]**

### **MPANGILIO WA VIFUNGU**

Kifungu                    Jina

**SEHEMU YA KWANZA  
MASHARTI YA JUMLA**

**SURA YA KWANZA  
MASHARTI YA MWANZO**

1.     Jina fupi
2.     [Kutotumika]
3.     Kubakizwa kwa sheria fulani.

**SURA YA PILI  
TAFSIRI**

4.     Kanuni ya kawaida ya tafsiri.
5.     Tafsiri

**SURA YA TATU  
MATUMIZI YA KANUNI HII YA ADHABU**

6.     Mipaka ya Mamlaka za Mahakama
7.     Makosa yatendwayo kwa kiasi fulani ndani ya mamlaka na kwa kiasi fulani nje ya mamlaka.

**SURA YA NNE  
KANUNI ZA JUMLA KUHUSU UWAJIBIKAJI WA KIJINAI**

8.     Kutokujua sheria.
9.     Kudai haki kwa nia njema.
10.    Uhusiano wa dhamira au nia.
11.    Dhania visivyo kweli.
12.    Kuchukuliwa kuwa na akili timamu.

13. Ugonjwa wa akili.
14. Ulevi
15. Umri mdogo.
16. Kinga ya jumla kwa Maafisa.
17. Shurutisho.
18. Kulinda mtu au mali.
- 18A. Haki ya kujilinda
- 18B. Kutumia nguvu katika kujilinda.
- 18C. Pale haki ya kujilinda inapozidi na kusababisha kifo.
19. Kutumia nguvu katika kukamata.
20. Shurutisho linalotolewa na mume.
21. Mtu kutokuadhibiwa mara mbili kwa kosa lilelile.

**SURA YA TANO  
WASHIRIKI KWENYE MAKOSA**

22. Wakosaji wakuu.
23. Makosa yanayotendwa na wakosaji walioshirikiana katika shitaka lenye kusudio moja.
24. Kumshawishi mwingine kutenda kosa.

**SURA YA SITA  
ADHABU**

25. Aina za adhabu.
26. Hukumu ya Kifo.
27. Kifungo.
28. Adhabu ya viboko.
29. Faini.
30. Kunyang'anywa mali
31. Fidia.
32. Gharama
33. Dhamana kwa ahadi ya kutunza amani.
34. [kimefutwa.]
35. Adhabu ya jumla kwa makosa ambayo adhabu zake hazijafafanuliwa.
36. Adhabu za pamoja isipokuwa kama itaamriwa vinginevyo.
37. Mfungwa aliyetoroka kutumikia kifungo kisichoisha pale anapokamatwa.
38. Kuachiwa bila masharti na kuachiwa na masharti.
- 38A. Kutenda kosa kwa mara nyingine.
- 38B. Matokeo ya kupatikana na hatia na kuachiwa.

**SEHEMU YA PILI  
MAKOSA YA JINAI**

*Divisheni ya I – Makosa Dhidi ya Amri za Serikali*

**SURA YA SABA  
UHAINI NA MAKOSA MENGINE DHIDI YA SERIKALI**

39. Uhaini.  
 40. Makosa ya uhaini  
 41. Kuficha uhaini.  
 42. [Kimeachwa.]  
 43. Kudhamini shughuli za kivita.  
 44. [kimebadilishwa.]  
 45. Kuchochea Uasi.  
 46. Kuwasaidia wanajeshi au maafisa wa polisi katika vitendo vya uasi.  
 47. Kuwashawishi wanajeshi au maofisa wa polisi kutoroka.  
 48. Kusaidia mateka wa vita kutoroka.  
 49. Tafsiri ya kitendo kinachojionyesha.  
 50.-54. [Vimefutwa.]  
 55. Nia ya kufanya uchochezi.  
 56.-58. [Vimefutwa.]  
 59. Viapo visivyo halali ili kutenda makosa.  
 60. Viapo vingine visivyo halali ili kutenda makosa.  
 61. Kulazimishwa kama utetezi.  
 62. Mafunzo ya Kijeshi yasiyo halali.  
 63 - 63A [ Vimefutwa]  
 63B Kuonyesha kutoridhika na dhamira ya chuki kwa nia isiyo halali

#### SURA YA NANE

#### MAKOSA YANAYOATHIRI MAHUSIANO NA MATAIFA YA NJE NA AMANI NA UTULIVU WA NCHI ZA NJE

- 64.(Kimefutwa)  
 65.Uandikishaji askari wa kivita kwa nchi za kigeni  
 66.Uharamia.

#### SEHEMU YA TISA MIKUSANYIKO ISIYO HALALI NA GHASIA NA MAKOSA MENGINE DHIDI YA UTULIVU WA UMMA

- 67-73 (Vimefutwa).  
 74 Maana ya mkusanyiko usio halali na ghasia.  
 75 Adhabu kwa mkusanyiko usio halali .  
 76 Adhabu kwa kufanya ghasia  
 77 Kutoa tamko kwa wafanya ghasia kutawanyika.  
 78 Kutawanyika kwa wafanya ghasia baada ya tamko kutolewa.  
 79 Ghasia baada ya tamko.  
 80 Kuzuia au kupinga kutoa tamko.  
 81 Wafanya ghasia kuharibu majengo n.k.  
 82 Wafanya ghasia kubomoa majengo n.k.  
 83 Kuingilia kwa ghasia reli, magari n.k.  
 84 Kutembea na silaha hadharani.  
 85 Kuingia kwa nguvu.

- 86 Kuzuia kwa nguvu.
- 87 Mapigano
- 88 Kuchochea mapigano ya watu wawili..
- 89 Lugha ya matusi, mzozo na kutishia kutumia nguvu.
- 89A Kuvinjari na kuzonga.
- 89B Kutishia.
- 89C Kushawishi watu wasisaidie mipango ya kujitolea.
- 90 Mkusanyiko kwa madhumuni ya kufanya magendo.

*Divisheni ya pili. - Makosa Dhidi ya Utawala Wenye Mamlaka Halali*

**SURA YA KUMI  
KUTUMIA MADARAKA VIBAYA**

- 91-93 (Vimefutwa)
- 94 Maafisa wanaosimamia mali ya watu maalum kwa kazi maalum
- 95 Madai ya uongo ya maafisa
- 96 Kutumia vibaya madaraka
- 97 Maafisa wa Serikali shahada za uongo
- 98 Matumizi yasiyoruhusiwa ya viapo vya nje ya Mahakama.
- 99. Matumizi ya uongo ya mamlaka
- 100. Kujifanya mtumishi wa umma
- 101. Kutishia kuwajeruhi watumishi walioajiriwa kwenye utumishi wa umma

**SURA YA KUMI NA MOJA  
MAKOSA YANAYOHUSU USIMAMIAJI WA HAKI**

- 102. Ushahidi wa uwongo na kushawishi kusema uwongo.
- 103. Maelezo ya uwongo ya wakalimani.
- 104. Adhabu kwa ushahidi wa uwongo.
- 105. Ushahidi juu ya shitaka la kutoa ushahidi wa uwongo.
- 106. Kutunga ushahidi
- 107. Kuapa uwongo.
- 108. Kudanganya mashahidi.
- 109. Kuharibu ushahidi.
- 110. Njama ya kuzuia haki na kuingilia mashahidi.
- 111. Kuweka pamoja makosa isivyokuwa halali.
- 112. Kuweka pamoja mashitaka ya adhabu.
- 113. Matangazo kwa mali iliyobiwa.
- 114. Kudharau mahakama .
- 114A. Kuzuia au kukinga uwasilishaji au utekelezaji wa hukumu.

**SURA YA KUMI NA MBILI**

**KUOKOA, KUTOROKA NA KUWAKINGA WATUMISHI WA MAHAKAMA**

- 115. Kuokoa.
- 116. Kutoroka kwenye kifungo halali.
- 116A. Kutokuhudhuria kazi za kifungo cha nje.
- 117. Kusaidia wafungwa kutoroka.
- 118. Uondoshaji n.k wa mali iliyokamatwa kihalali.
- 119. [Kimefutwa]

**SURA YA KUMI NA TATU**

**MAKOSA YA MADOGOMADOGO DHIDI YA MAMLAKA YA UMMA**

- 120. Udanganyifu na uvunjaji wa uaminifu kwa watumishi wa umma
- 121. Kuupuza wajibu wa kikazi.
- 122. Kutoa taarifa za uongo kwa watumishi wa umma .
- 123. Kutokutii wajibu wa kisheria.
- 124. Kutokutii amri halali.
- 124A. [Kimefutwa.]

*Kigawo cha Tatu. – Makosa yanayodhuru Umma kwa Ujumla*

**SURA YA KUMI NA NNE**

**MAKOSA YANAYOHUSIANA NA DINI NA MAZISHI**

- 125. Fedheha kwenye dini.
- 126. Kufanya fujo kwenye mikusanyiko ya dini.
- 127. Kuingia kwenye mazishi au sehemu nyingine bila idhini
- 128. Kuzuua mwili wa mtu aliyekufa kuzikwa.
- 129. Kutamka maneno kwa nia ya kuudhi imani ya dini.

**SURA YA KUMI NA TANO**

**MAKOSA DHIDI YA UTU**

- 129A. Tafsiri ya mwanamke.
- 130. Kubaka.
- 131. Adhabu ya kubaka.
- 131A Adhabu ya kubaka kulikofanywa na kikundi
- 132 Kujaribu kubaka
- 133. Kutorosha
- 134 Kutorosha mwanamke wa chini ya miaka kumi na sita
- 135 Kujamiiana kwa watu na shambulio la aibu kwa mwanamke
- 136 (Kimefutwa)
- 137 Kunajisi majuha au punguani
- 138 Mume kumnajisi mkewe aliye chini ya umri wa miaka kumi na tano n.k

- 138A. Vitendo vya shambulio la aibu kati ya watu  
 138B. Kuwatumia watoto kwa ngono  
 138C. Matumizi mabaya ya ngono  
 138D. Shambulio la aibu  
 139 Uwakala wa ukahaba  
 139A. Kusafirisha watu  
 140 Uwakala wa ubakaji  
 141 Mwenye nyumba n.k. kuruhusu kunajisiwa kwa msichana wa chini ya miaka kumi na miwili kwenye nyumba yake.  
 142 Mwenye nyumba n.k , kuruhusu kunajisiwa msichana wa umri chini ya miaka kumi na sita kwenye nyumba yake.  
 143 Kuzuia katika jengo lolote au katika danguro kwa nia fulani.  
 144 Uwezo wa kupekua.  
 145 Mwanamume kuishi kwa pato la ukahaba au ukowadi.  
 146A Mwanamke anayeishi kutokana na au kwa kusaidia ukahaba  
 147 Uwezo wa kupekua.  
 148 Kumiliki danguro.  
 149 Njama ya kushawishi kujamiiiana kusiko halali.  
 150 Kujaribu kutoa mimba.  
 151 Kusababisha kuharibika mimba.  
 152 Kutoa dawa au vifaa vya kutoa mimba.  
 153 Ufahamu kuhusu umri wa mwanamke si muhimu.  
 154 Makosa ya kinyume cha maumbile.  
 155 Kujaribu kujamiiiana kinyume cha maumbile.  
 156 Shambulio la aibu kwa wavulana wa chini ya miaka kumi na nne.  
 157 Matendo ya aibu baina ya wanaume.  
 158 Wanaume kujamiiiana na maharimu.  
 159 Amri ya ulezi  
 160 Wanawake kujamiiiana na maharimu.  
 160A Adhabu kwa makosa ya kujamiiiana.  
 161 Kipimo cha undugu.  
 162 Idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

#### SURA YA KUMI NA SITA

#### MAKOSA YANAYOHUSIANA NA NDOA NA WAJIBU WA MAMBO YA NYUMBANI

- 163 Ndoa ya hadaa.  
 164 (Kimefutwa).  
 165 Sherehe ya ndoa iliyofanyika kihadaa bila ya ndoa halali  
 166 Kutelekeza watoto.  
 167 Kupuuza kutoa chakula n.k. kwa watoto.  
 168 Tajiri kutompatia mtumishi wake au mwanagenzi wake mahitaji.  
 169 Kuiba mtoto.  
 169A Ukatili kwa watoto.

**SURA YA KUMI NA SABA**  
**ADHA NA MAKOSA DHIDI YA AFYA NA HALI INAYOFAA**

- 170 Adha za kawaida.  
171 Nyumba za kamari.  
171 A Katazo la mpango wa piramidi  
171 B Katazo dhidi ya ushawishi.  
171 C Fasiri  
172 Nyumba za kupingiana  
173 (Kimefutwa)  
173 A (Kimefutwa)  
173 B Barua zinazofanana.  
174 Maana ya mtunzaji wa majengo  
175 Upitishaji wa matangazo ya kinyaa.  
176 Wavivu na wazembe.  
176 A mahala pa kuhifadhi makahaba  
177 Wazembe na wazururaji.  
177A Kuacha kutoa hesabu ya fedha iliyokusanywa kwa matumizi ya Umma.  
178 Makosa yanayohusu uvaaji wa vazi rasmi bila mamlaka.  
179 Kitendo cha uzembe ambacho kinaweza kueneza maambukizo.  
180. Kuchanganya na kitu kingine chakula au kinywaji kinachokusudiwa kuuzwa  
181 Kughushi chakula au kinywaji kinachokusudiwa kuuzwa.  
182 Kuuza chakula au kinywaji chenye madhara  
183 Kughushi madawa  
184 Kuuza madawa yaliyoghushiwa  
185 Kuchafua maji  
186 Kuchafua hewa  
187 Biashara mbaya

**SURA YA KUMI NA NANE**  
**KASHIFU**

187-194 (Vimefutwa)

**SURA YA KUMI NA TISA**  
**MAKOSA YA KUHODHI BIDHAA NA YANAYOHUSIANA**

- 194A Kuhodhi bidhaa  
194B (Kimefutwa)

*Divisheni ya IV- Makosa Dhidi ya Mtu*

**SURA YA ISHIRINI  
KUUA KWA KUKUSUDIA NA KUUA BILA YA KUKUSUDIA**

- 195 Kuua bila ya kukusudia.
- 196 Kuua kwa kukusudia
- 197 Adhabu ya kuua kwa kukusudia.
- 198 Adhabu ya kuua bila ya kukusudia.
- 199 Kutiwa hatiani kwa kosa la kuua mtoto mchanga katika mazingira fulani.
- 200 Nia ya uovu.
- 201 Kuua kwa kukasirishwa.
- 202 Maana ya kukasirishwa.
- 203 Maana ya kusababisha kifo.
- 204 Wakati ambapo mtoto anadhaniwa kuwa ni mtu .
- 205 Kikomo cha muda wa kufa.

**SURA YA ISHIRINI NA MOJA  
WAJIBU KUHUSU HIFADHI YA MAISHA NA AFYA**

- 206 Wajibu wa mtu anayetunza mtu mwengine.
- 207 Wajibu wa mkuu wa familia.
- 208 Wajibu wa mwajiri.
- 209 Wajibu wa watu wanaofanya vitendo vyat hatari.
- 210 Wajibu wa watu wanaotunza vitu hatari.

**SURA YA ISHIRINI NA MBILI  
MAKOSA YANAYOHUSIANA NA KUUA KWA KUKUSUDIA NA KUJIUA**

- 211 Kujaribu kuua kwa kukusudia
- 212 (Kimefutwa)
- 213 Mfichaji wa muuaji wa kukusudia
- 214 Maandishi ya kutishia kuua .
- 215 Njama za kuua.
- 216 Kumsaidia mtu kujiua.
- 217 Kujaribu kujiua.
- 218 Kuficha kuzaliwa kwa mtoto.
- 219 Kuharibiwa kwa mtoto.

**SURA YA ISHIRINI NA TATU  
MAKOSA YA KUHATARISHA MAISHA AU AFYA**

- 220 Kulemaza kwa nia ya kutenda kosa

- 221 Kupumbaza kwa nia ya kutenda kosa  
 222 Vitendo vinavyokusudia kusababisha madhara makubwa au kuzuia ukamataji  
 222A Kumiliki viungo nya binadamu  
 223 Kumzuia mtu kujiooka katika chombo  
 224 Kuhatarisha usalama wa watu wanaosafiri na njia ya reli  
 225 Dhara kubwa  
 226 Kujaribu kujeruhi kwa kitu kinacholipuka  
 227 Kuweka sumu kwa nia mbaya kwa kusudi ya kudhuru  
 228 Kujeruhi na matendo yanayofanana na hayo.  
 229 Kushindwa kutoa mahitaji muhimu  
 230 Wajibu kwa wanaofanya upasuaji wa kitabibu.  
 231 Wajibu kijinai kwa kutumia nguvu zaidi  
 232 Madhara ya ridhaa ya mhanga katika wajibu wa kijinai aliyeruhusu kuuawa kwake

**SURA YA ISHIRINI NA NNE  
JINAI KWA KUPUUZA NA UZEMBE**

- 233 Vitendo nya kupuuza na uzembe  
 234 Vitendo vingine nya uzembe vinavyosababisha madhara  
 235 Kushika vitu nya sumu kwa uzembe  
 236 (Kimeachwa)  
 237 Maonyesho ya taa za uongo, alama au boyo  
 238 Kumsafirisha mtu kwa njia ya majini kwa kukodi katika chombo kisicho salama au kilichojaa.  
 239 Hatari au kizuizi kwenye njia ya umma au njia ya meli

**SURA YA ISHIRINI NA TANO  
MASHAMBULIO**

- 240 Shambulio la kawaida  
 241 Shambulio linalosababisha madhara ya mwili  
 242 Mashambulio kwa watu wanaolinda chombo  
 243 Aina nytingine za shambulio

**SURA YA ISHIRINI NA SITA  
MAKOSA DHIDI YA UHURU**

- 244 Maana ya kuteka nyara kutoka Tanzania Bara  
 245 Maana ya kuteka nyara kutoka kwa mlezi halali.  
 246 Maana ya kutorosha  
 247 Adhabu ya kuteka nyara  
 248 Kuteka nyara au kutorosha kwa nia ya kuua  
 249 Kuteka nyara au kutorosha kwa nia ya kufungia

- 250 Kuteka nyara au kutorosha kwa nia ya kujeruhi
- 251 Kumficha mtu aliyetekwa nyara au kutoroshwa kinyume na sheria
- 252 Kumteka au kumtorosha mtoto kwa nia ya kumuiba
- 253 Adhabu ya kumfungia mtu isivyo halali.
- 254 Kumnumua au kumuza mtu yejote kama mtumwa.
- 255 Mazoea ya kujihusisha na utumwa
- 256 Kumlazimisha mtu kufanya kazi isivyo halali

#### SURA YA ISHIRINI NA SABA WIZI

- 257 Vitu vinavyoweza kuibowi
- 258 Maana ya wizi
- 259 Kesi maalum
- 260 Fedha n.k. iliyozuiwa kwa maagizo
- 261. Fedha n.k. zinazopokelewa na wakala kutokana na mauzo..
- 262. Fedha inayopokelewa kwa niaba ya mwingine.
- 263. Wizi wa watu wenye masilahi katika kitu kilichoibiwa.
- 264. Mume na mke
- 265. Adhabu ya jumla ya wizi
- 266. Kuiba wosia.
- 267. [Kimefutwa]
- 268. Kuiba wanyama fulani
- 269. Kumuibia mtu, n.k.
- 270. Wizi wa watu waliopo katika utumishi wa umma
- 271. Wizi wa makarani na watumishi.
- 272. Wizi wa wakurugenzi au maafisa wa makampuni.
- 273. Wizi wa mawakala.
- 274. Wizi wa wapangaji au wafikiaji.
- 275. Kuiba baada ya kuhukumiwa

#### SURA YA ISHIRINI NA NANE MAKOSA YANAYOHUSIANA NA WIZI

- 276. Kuficha madaftari ya kumbukumbu
- 277. Kuficha wosia.
- 278. Kuficha hati.
- 279. Kuua wanyama kwa nia ya kuiba.
- 280. Kuhamisha kwa nia ya kuiba.
- 281. Kiudanganyifu kutoa bidhaa iliyowekwa rehani.
- 282. Kiudanganyifu kujihusisha na madini ndani ya machimbo.
- 283. Kuchukua madaraka kwa udanganyifu
- 284. Kuchukuwa kusiko sababisha wizi.
- 284A Kusababisha hasara ya fedha au uharibifu wa mali ya mamlaka fulani.

**SURA YA ISHIRINI NA TISA  
UNYANG'ANYI NA KUPORA KWA NGUVU**

- 285. Tafsiri ya unyang'anyi.
- 286. Adhabu ya unyang'anyi
- 287. Kujaribu kuiba.
- 288. Kushambulia kwa nia ya kuiba.
- 289. Kudai mali kwa vitisho vya maandishi.
- 290. Kujaribu kupora kwa nguvu na vitisho.
- 291. Kusababisha utekelezaji wa hati n.k. kwa vitisho.
- 292. Kudai mali kwa kutishia kwa nia ya kuiba.

**SURA YA THELATHINI  
UVUNJAJI WA NYUMBA USIKU, UVUNJAJI WA NYUMBA MCHANA NA  
MAKOSA SAWA NA HAYO**

- 293. Tafsiri ya kuvunja na kuingia.
- 294. Uvunjaji nyumba mchana na uvunjaji nyumba usiku.
- 295. Kuingia kwenye nyumba ya kuishi kwa nia ya kutenda kosa.
- 296. Kuvunja nyumba na kuingia kwa nia ya kutenda kosa.
- 297. Kuvunja nyumba na kuingia kwa nia ya kutenda kosa lolote .
- 298. Kuchukuwa na silaha, n.k kwa nia ya kutenda kosa.
- 299. Jinai ya kuingia bila idhini.
- 300. Kuhodhi

**SURA YA THELATHINI NA MOJA  
UDANGANYIFU**

- 301. Ufafanuzi wa udanganyifu
- 302. Kupata bidhaa kwa njia ya udanganyifu.
- 303. Kupata kutimilizwa kwa dhamana kwa njia ya udanganyifu
- 304. Kuhadaa.
- 305. Kupata mkopo n.k, kwa njia ya uongo.
- 305A Pale ambapo mali au muamana umepatikana kwa ajili ya mtu mwengine.
- 306. Kula njama kwa nia ya kudanganya.
- 307. Udanganyifu katika kuuza au kuweka rehani mali.
- 308. Kujifanya kupiga ramli.
- 309. Kujipatia usajili, n.k. kwa udanganyifu
- 310. Tamko la uwongo ili kujipatia hati ya kusafiria.

**SURA YA THELATHINI NA MBILI**  
**KUPOKEA MALI ILIYOIBIWA AU ILIYOPATIKANA ISIVYO HALALI**  
**NA MAKOSA KAMA HAYO**

- 311. Kupokea mali iliyoibiwa au iliyopatikana isivyo halali
- 312. Watu kusafirisha au kumiliki mali ambazo zinadhaniwa zimeibiwa au zimepatikana isivyo halali
- 312A Kumiliki au kusafirisha vifaa vya umma isivyo halali
- 313 Kupokea bidhaa zilizoibiwa nje ya Tanzania Bara

**SURA YA THELATHINI NA TATU**  
**UDANGANYIFU WA WADHAMINI NA WATU WA KAZI ZA DHAMANA NA**  
**HESABU ZA UWONGO**

- 314. Wadhamini kuuza mali za muamana kwa udanganyifu.
- 315. Ubadhirifu na udanganyifu wa wakurugenzi na maafisa wa mashirika, n.k..
- 316. Maelezo ya uwongo ya maafisa wa makampuni.
- 317. Kughushi hesabu kwa karani.
- 318. Kughushi hesabu kwa mtumishi wa umma.

**SURA YA KUMI NA NNE**  
**MAKOSA DHIDI YA USALAMA WA ANGA**

- 318A Kuhatarisha usalama wa vyombo vya anga.

*Kigawo cha Sita - Uharibifu wa Mali kwa Makusudi*

**SURA YA THELATHINI NA TANO**  
**MAKOSA YANAYOSABABISHA UHARIBIFU WA MALI**

- 319. Uchomaji wa mali kwa makusudi.
- 320 . Kujaribu kuchoma mali
- 321. Kutia moto katika mazao na mimea iotayo.
- 322. Kujaribu kutia moto mazao n.k.
- 323. Kukalibu vyombo.
- 324. Kujaribu kukalibu vyombo.
- 325 Kujeruhi wanyama.
- 326 Adhabu ya kuharibu mali kwa makusudi.
- 327 Kujaribu kuharibu mali kwa milipuko.
- 328 Kusababisha wanyama kupata magonjwa ya kuambukiza.
- 329 Kuondoa alama za mipaka kwa nia ya kudanganya.
- 330 [Kimefutwa]

- 331 Kusababisha uharibifu n.k. katika kazi za reli.
- 332 Vitisho vya kuchoma au kuharibu.
- 332A Kuharibu noti za benki.
- 332B Kurusha kishada.

*Kigawo cha Saba. – Kughushi, , Utengenezaji wa Sarafu,,  
na Makosa sawa na hayo*

#### SURA YA THELATHINI NA SITA TAFSIRI

- 333. Tafsiri ya kughushi.
- 334. Ufafanuzi wa “nyaraka.”
- 335. Utengenezaji wa nyaraka ya uwongo
- 336 Nia ya kudanganya.

#### SURA YA THELATHINI NA SABA ADHABU KWA KUGHUSHI

- 337. Adhabu ya, na adhabu ya jumla kwa kughushi.
- 338. Kughushi ambapo adhapo ni kifungo cha maisha.
- 339. Kughushi hati ya mahakama au nyaraka ya kiofisi
- 340. Kughushi ambapo adhabu nikifungo cha miaka saba.
- 341. Kutengeneza au kumiliki makaratasi au zana za kughushi.
- 342. Kutoa nyaraka za uongo
- 343. Kutoa nyaraka zilizofutwa au zilizomalizika muda.
- 344. Kupata utimilizaji wa nyaraka kwa njia ya udanganyifu.
- 345. Kufuta michanjo katika hundi.
- 346. Kutengeneza nyaraka bila mamlaka
- 347. Kudai mali kwa nyaraka za wosia zilizoghushishiwa.
- 348. Kununua noti zilizoghushishiwa
- 349. Kugushi hati za fedha zinazolipwa chini ya mamlaka ya umma.
- 350. Kughushi daftari la kumbukumbu.
- 351. Kupeleka shahada za ndoa za uwongo kwa msajili.
- 352. Maelezo ya uongo katika daftari la uandikishwaji wa vizazi, vifo na ndoa.
- 352A. Kutoa noti isivyo halali.

#### SURA YA THELATHINI NA NANE MAKOSA YANAYOHUSU SARAFU

- 353. Tafsiri

- 354. Kughushi sarafu.
- 355. Matayarisho ya kutengeneza sarafu bandia
- 356. Kupunguza sarafu.
- 357. Kuyeyusha sarafu.
- 358. Kuzuia na kuharibu sarafu iliyoghushiwa.
- 359. Kumiliki sarafu zilizokatwa.
- 360. Kutoa sarafu za kughushi..
- 361. Utoaji uliorudiwa.
- 362. Kutoa nishani au madini kuwa kama sarafu.
- 363. Kusafirisha sarafu za kughushi.
- 364. Kuhodhi.

**SURA YA THELATHINI NA TISA  
MIHURI YA KUGHUSHI**

- 365. Kumiliki kihesi kwa madhumuni ya kutengeneza stampu.
- 366. Karatasi na vihesi vyta kutengeneza stampu za posta.

**SURA YA AROBAINI  
KUGHUSHI ALAMA ZA BIASHARA**

- 367. Alama za biashara kufafanuliwa.
- 368. Kughushi alama za biashara.

**SURA YA AROBAINI NA MOJA  
KUJIFANYA MTU MWINGINE**

- 369. Kujifanya mtu mwngine kwa ujumla.
- 370. Kwa udanganyifu kukubali hati, kuidhinisha, n.k.
- 371. Kujifanya mtu aliyetajwa kwenye cheti.
- 372. Kuazimisha, n.k, cheti kwa kujifanya mtu mwngine
- 373. Kujifanya mtu aliyetajwa kwenye uthibitisho wa tabia.
- 374. Kuazimisha, n.k. kutoa ushahidi kwa kujifanya mtu mwngine.

**SURA YA AROBAINI NA MBILI  
MATENDO YA SIRI**

- 375.-379. [Vimefutwa]

*Kigawo cha Nanne – Majaribio,, Njama za Kutenda Uhalifu, Kuficha Uhalifu,  
Ushawishi na Uchochez*

SURA YA AROBAINI NA TATU  
MAJARIBIO

- 380. Kujaribu kufafanuliwa.
- 381. Kujaribu kutenda makosa.
- 382. Adhabu kwa majaribio ya kutenda makosa.
- 383. Kupuuza kuzuia kosa.

SURA YA AROBAINI NA NNE  
NJAMA

- 384. Njama ya kutenda kosa linaloadhibiwa kwa kifungo cha miaka mitatu au zaidi.
- 385. Njama ya kutenda kosa linaloadhibiwa kwa kifungo kisichozidi miaka mitatu.
- 386. Njama nyinginezo.

SURA YA AROBAINI NA TANO  
WAFICHAJI UHALIFU

- 387. Ufafanuzi wa wafichaji uhalifu
- 388. Adhabu kwa wafichaji uhalifu wa makosa yanayoadhibiwa kwa kifungo cha miaka mitatu au zaidi
- 389. Adhabu kwa wafichaji uhalifu wa makosa yanayoadhibiwa kwa kifungo kisichozidi miaka mitatu.

SURA YA AROBAINI NA SITA  
USHAWISHI NA UCHOCHEZI

- 390. Kushawishi au kuchochea utendekaji wa kosa.

## SURA YA 16

---

### SHERIA YA KANUNI ZA ADHABU

Sheria ya kuweka Kanuni ya Sheria ya Jinai.

[28 Septemba, 1945]

R.L. Sura 390

R.L. Sura 400

R.L. Sura 440

Sheria Namba:

11 ya mwaka 1930

10 ya mwaka 1936

24 ya mwaka 1939

16 ya mwaka 1943

21 ya mwaka 1945

11 ya mwaka 1954

47 ya mwaka 1954

19 ya mwaka 1958

5, 23, 44 na 60 ya mwaka 1961

12, 61 na C.A. namba 2 ya mwaka 1962

15, 20 na 55 ya mwaka 1963

16 na 65 ya mwaka 1964

2 of 1965

12, 24, 31 na 65 ya mwaka 1966

23 ya mwaka 1967

50 ya mwaka 1968

2 ya mwaka 1970

5, 15 na 26 ya mwaka 1971

2, 13 na 31 ya mwaka 1972

23 ya mwaka 1973

3 ya mwaka 1976

14 ya mwaka 1980

11 ya mwaka 1983

13 ya mwaka 1984

7 na 9 ya mwaka 1985

12 ya mwaka 1987

3 ya mwaka 1988

10 na 17 ya mwaka 1989

1, 5 na 17 ya mwaka 1990

19 ya mwaka 1992

1 ya mwaka 1993

13 ya mwaka 1994

3 ya mwaka 1995

31 ya mwaka 1997

4 na 12 ya mwaka 1998

10 ya mwaka 2001

9 ya mwaka 2002

25 ya mwaka 2002

4 ya mwaka 2004

19 ya mwaka 2004

8 ya mwaka 2006

19 ya mwaka 2007

Tangazo la Ser. Namba 478 ya mwaka 1962

Tangazo la Serikali Namba 222 ya mwaka 1971

Tangazo la Serikali Namba 67 ya mwaka 1972

Tangazo la Serikali Namba 15 ya mwaka 1981

---

## SEHEMU YA KWANZA MASHARTI YA KAWAIDA

---

### SURA YA KWANZA MASHARTI YA MWANZO

Jina fupi  
Sh. ya 1945  
No.21 f.2

Kutotumika

Kubakizwa  
kwa sheria  
Fulani  
Sheria Namba.  
49 ya 1955 k.  
2; R.L. Cap.  
500 s. 36

- 1.** Sheria hii itaitwa Sheria ya Kanuni za Adhabu, na itajulikana kama “Kanuni hii”.
- 2.** [Kutotumika kwa Sheria ya Kanuni ya Adhabu ya India.]
- 3.** (1) Hakuna kitu chochote katika Kanuni hii kitakachoathiri –
  - (a) kuwajibika, kushtakiwa, au adhabu kwa mtu kwa kosa dhidi ya Sheria ya kawaida au dhidi ya Sheria nyingine yoyote inayotumika Tanzania Bara tofauti na kanuni hii;
  - (b) kuwajibika kwa mtu ye yoyote kwa kushtakiwa au kuadhibiwa kwa kosa lolote chini ya masharti yoyote ya sheria yoyote inayotumika Tanzania Bara kuhusiana na mamlaka ya mahakama kutokana na vitendo vilivyofanyika nje ya mamlaka ya kawaida ya mahakama hizo ;
  - (c) uwezo wa mahakama yoyote kumpa adhabu mtu kwa kuidharau mahakama ; au
  - (d) uwezo wowote wa Rais kutoa msamaha au kupunguza adhabu aukufuta adhabu yote au sehemu ya adhabu au kuahirisha utimizaji wa hukumu yoyote iliyokwishatolewa au itakayotolewa.
- (2) Iwapo mtu atatenda kosa ambalo linaadhibiwa chini ya Kanuni hii na pia linaadhibiwa chini ya sheria nyingine yoyote, iliyotajwa chini ya kifungu hiki, mtu huyo hataadhibiwa kwa kosa hilo zaidi ya mara moja chini ya sheria hiyo na chini ya Kanuni hii . .

### SURA YA PILI TAFSIRI

Kanuni ya  
kawaida ya  
tafsiri  
Sheria Na. 14  
ya 1980 k. 3

Tafsiri  
R.L. sura. 500  
k. 8 na 36; R.L.  
Sura. 537  
jedwali la6.;  
RJ. Sura. 553  
Jedwali la 2.;  
Sheria na: 2 ya  
mwaka1965  
Jedwali la 24 la  
mwaka1966  
Jedwali la 2  
;50 la mwaka  
1968 Jedwali la  
1; 14 la mwaka  
1980 K. 4

4. Kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Tafsiri na ufanuzi mahsusini ya maneno yaliyo chini ya Kanuni hii, Kanuni hii itatafsiriwa kwa kuzingatia misingi ya tafsiri ambayo inaweza kutumika kwenye sheria nyingine yoyote, kwa kuzingatia hali halisi ya Tanzania na bila kutumia misingi yoyote ya tafsiri inayohusu sheria ya adhabu.

5. Katika kanuni hii, isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo- "mahakama" maana yake mahakama yenyе mamlaka ya kusikiliza kesi husika;  
"nyumba ya kuishi" inajumuisha nyumba yoyote au sehemu ya nyumba ambayo kwa wakati huu inatumwa na mwenye nyumba au na mpangaji wake kwa ajili ya makazi yake mwenyewe, familia yake, au watumishi wake au ye yoyote kati ya hao na hajjalishi kama mara kwa mara imekuwa haitumiki; jengo au sehemu ya jengo linalopakana au lililoko ndani ya nyumba ya kuishi litachukuliwa kuwa ni sehemu ya nyumba ya kuishi iwapo kutakuwa kuna mawasiliano kati ya jengo hilo au sehemu ya nyumba hiyo na nyumba ya kuishi, iwe mara baada ya, au kwa njia iliyofunika au iliyowazi kupitia kutoka sehemu moja kwenda nyingine, lakini sio vinginevyo;  
"dhara" maana yake ni dhara la mwilini, ugonjwa au ulemavu uwe wa kudumu au wa muda.  
" dhara ya hatari" maana yake ni dhara linalohatarisha maisha;  
"dhara kubwa" maana yake ni dhara ambalo linaweza kulemaza au ni dhara kubwa linaloweza kudhuru afya moja kwa moja au sehemu au kuleta kilema cha kudumu au kuleta jeraha lolote la kudumu au kudhuru sehemu yoyote ya nje au ndani ya mwili, kiungo au kudhuru akili;  
"shauri la kimahakama" litajumuisha shauri lolote ambalo litapelekwa mbele ya mahakama, baraza, tume au mtu au mtu ye yoyote ambaye au mbele yake ushahidi unaweza kuchukuliwa kwa kiapo;  
"kujuua" inapotumiwa kwa neno lolote litakuwa na maana na kuonyesha hali ya kufahamu tabia ya kitu hicho kilichotokea au kilichotumiwa;  
"serikali za mitaa" maana yake ni serikali za mitaa zilizoanzishwa kwa mujibu wa sheria;  
"kilema" maana yake ni kuharibu au kulemaza kwa kudumu sehemu yoyote ya kiungo cha nje au ndani,, kiungo au akili;  
"fedha" inajumuisha noti za benki, sarafu, hundi na hati ya idhini ya fedha na amri nyingine, idhini au maombi ya malipo ya fedha;  
"usiku" au "wakati wa usiku" maan yake ni kipindi kati ya saa moja jioni na saa kumi na mbili asubuhi;  
"kosa" maana yake ni kufanya kitendo au kujaribu kufanya kitendo na kinachokiuka sheria;  
"mtu" na "mmiliki" na maneno yanayofanana na hayo yanapotumika kuhusiana na mali yatajumuisha pia mashirika ya aina zote na ushirika wowote wa watu wanaoweza kumiliki mali, na pale inapotumika itahusisha pia Serikali;

"mtu aliyeajiriwa kwenye utumishi wa umma " maana yake ni mtu yeote anayefanya kazi katika mojawapo ya ofisi zifuatazo au ambaye anafanya shughuli za ofisi hizo , awe kama msaidizi au vinginevyo, yaani:-

- (i) ofisi yoyote ya umma, ikijumuisha ofisi ya Rais, na ofisi yoyote ambayo uwezo wa kumteua mtu au kumuondoa umewekwa kwa Rais au uko kwa Tume au Bodi ambayo Raisanakasimu mamlaka ya kazi zake alizopewa au kama imeanzishwa kwa mujibu wa sheria yoyote kwa madhumuni ya au kufanya uteuzi kwenye ofisi yoyote;
- (ii) ofisi yoyote ambayo, mtu ameteuliwa au kuchaguliwa kwa mujibu wa sheria yoyote;
- (iii) ofisi yoyote ya umma , ambayo mamlaka ya kumteua au kumwondoa imewekwa kwa mtu au watu wanaoshika ofisi za aina yeyote ikijumuisha zile zilizotajwa katika aya ya (i) au (ii) au
- (iv) ofisi yoyote ya msuluhishi au muamuzi katika shauri au jambo lolote lililopelekwa kwa msuluhishi kwa amri au uamuzi wa mahakama, au kwa mujibu wa sheria yoyote;

Na pia itamaanisha watu wafuatao:-

- (i) mlinzi wa amani;
- (ii) mjambe wa tume ya uchunguzi aliyechaguliwa chini au kwa mujibu wa sheria yoyote;
- (iii) mtu yeyote iliyejiriwa kufanya shughuli za mahakama;
- (iv) mjambe wa Jeshi la Kawaida la Jeshi la Ulinzi,, mjambe wa Jeshi la Kujenga Taifa, na mjambe mwengine yeyote wa Jeshi la Ulinzi wakati akiwa kazini;
- (v) mtu yeyote anayefanya kazi katika idara yoyote ya Serikali;
- (vi) mtu anayekaimu kama kiongozi wa dini yoyote ambaye anatimiza wajibu wake kwa mujibu wa mambo ya ndoa, au kuweka kumbukumbu za ndoa, au kwa mujibu wa kutengeneza na kuweka daftari au cheti cha ndoa, kuzaliwa, ubatizo, vifo, au mazishi na sio kwa jinsi nyingine yeyote;
- (vii) mjambe wa serikali za mitaa;
- (viii) diwani wa manispaa;
- (ix) mtu yeyote aliyeajiriwa na serikali za mitaa;
- (x) mtu yeyote aliyeajiriwa na aliye katika utumishi wa shirika lolote la umma lililoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika ya Umma ambalo si kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni ambayo inamilikiwa na Serikali au kampuni tanzu ya shirika la umma;.

Cap.257

Cap.212

"kumiliki", " kuwa katika umiliki wa kitu "au" kumiliki kitu"  
kunajumuisha:-

- (a) sio tu kumiliki kitu cha mtu binafsi bali pia kwa kuwa kuwa

- unamiliki au kitu kinachohusika kiko chini ya miliki au kuwa na kitu chochote mahali (kiwe kinamilikiwa na au kiko chini ya mtu binafsi au la] kwa matumizi ya mtu binafsi au mtu mwengine yejote;
- (b) iwapo kuna watu wawili au zaidi, na mmoja au zaidi ya mmoja kati yao kwa ufahamu na idhini ya wenzake anahodhi au kumiliki au wanahodhi au kumiliki, kutachukuliwa kuwa kimechukuliwa na kunahodhiwa au kumilikiwa na kila mmoja au wote kwa pamoja;
- "mali" itajumuisha pia kila kitu chenye uhai au kisicho na uhai ambacho kinaweza kumilikiwa;
- "umma" inamaanisha sio tu watu wote wa Tanzania Bara, lakini pia watu wanaoishi au wanaotumia sehemu yoyote husika au idadi yoyote ya watu hao na pia inajumuisha watu wengine ambao hawatambuliki kama itakavyoweza kuadhiriwa na mwenendo juu ya tabia au kitendo kinachohusika;
- "sehemu za umma" au "majengo ya umma" inajumuisha njia yoyote ya umma na jengo lolote, mahali au chombo chochote cha kusafiria ambacho kwa wakati huu, watu wana haki au wanaruhusiwa kuingia bila ya sharti au kwa sharti la kulipa chochote, na jengo lolote au mahali ambapo kwa wakati huu litatumia kwa ajili ya mikutano ya hadhara au ya mikutano ya kidini; au mikusanyiko au kwenye mahakama iliyo wazi;
- "njia ya umma" unajumuisha njia yoyoe ipitwayo, mahali pa soko, eneo mtaa, , daraja au barabara nyingineyo ambayo inaruhusiwa kutumiwa na watu;
- "hadharani pale inapotumika katika kitendo lina maana iwapo:-
- (a) kinatendwa mahali popote pa hadhara ambapo vyaweweza kuonekana na mtu yeyote iwapo mtu huyo yupo katika mahali pa hadhara; au
  - (b) kama kinatendeka mahali popote pasipokuwa pa hadhara ambapo kunauwezekano wa kuonekana na mtu yeyote aliyeko mahali pa hadhara;
  - (c) "toa tamshi" inajumuisha kutumia au kshughulika na kujaribu kutumia au kushughulikia na kumjaribu mtu yeyote kutumia ,kushughulikia au kikitenda juu ya kitu hicho;
- "dhamana yenyе thamani" inajumuisha na nyaraka yoyote ile ambayo ni mali ya mtu yeyote na ambayo ni ushahidi wa umiliki wa mali yoyote au haki ya mtu yeyote kudai au kupokea mali yake iliyopotea;
- "chombo" kinajumuisha meli, mashua na kila aina ya chombo kinachotumika kwenye mito, maziwa, majini au inajumuisha chombo cha usafiri wa anga;
- "jeraha" maana yake ni mchanjo au kutoboka ambako kunagawa au unatoboa sehemu yoyote ya nje ya mwili ; na sehemu yeyote ya nje ya mwili kwa madhumuni ya ufanuzi huu ambayo inaweza kuguswa bila ya kugawa au kutobowa na shemu nyingine ya mwili.

**SURA YA TATU**  
**MATUMIZI YA KANUNI HII YA ADHABU**

Mipaka ya  
Mamlaka za  
mahakama za  
Tanzania Bara  
Sheria Na. 31  
ya 1966  
Nyongeza ya  
Pili; Sheria Na.  
14 ya 1980 k. 5

Makosa  
yatendwayo  
kwa kiasi  
Fulani ndani ya  
mamlaka na  
kwa kiasi fulani  
nje ya  
mamlaka.

Kutokujua  
sheria

Kudai haki kwa  
nia njema

Uhusiano wa  
dhamira au nia

- 6.** Mamlaka ya Mahakama za Tanzania Bara kwa madhumuni ya kanuni hii, zitafikia mpaka;
- (a) sehemu yoyote ndani ya Tanzania Bara na sehemu yake ya bahari ;
  - (b) kosa lolote lililotendwa na raia ye yeyote wa Tanzania Bara katika sehemu yoyote nje ya Tanzania Bara; na
  - (c) kosa lolote litakalotendwa na mtu ye yeyote ndani ya ndege iliyosajiliwa Tanzania Bara.

- 7.** Endapo kitendo kitafanyika ndani ya mamlaka ya mahakama, kitakuwa ni kosa dhidi ya kanuni hii, na sehemu ya kitendo hicho kimetendwa ndani ya mamlaka na nje kidogo ya mamlaka ya mahakama kila mtu ambaye yupo ndani ya mamlaka ya mahakama ametenda sehemu ya kitendo hicho anawenza kushitakiwa na kuhukumiwa chini ya Kanuni hii kwa namna ile ile kana kwamba kitendo kile chote kilitendwa ndani ya mamlaka hayo.

**SURA YA NNE**  
**KANUNI ZA KUHUSU UWAJIBIKAJI WA KIJINAI**

- 8.** Kutokujua sheria hakuwezi kuwa ni sababu ya kusamehewa kwa kutenda au kutokutenda kitendo chochote ambacho kitakuwa ni kosa isipokuwa kujua sheria kwa mkosaji kutachukuliwa kwamba ni kielelezo cha kosa.

- 9.** Mtu hatawajibika kwa kosa la kijinai kutokana na na kosa linalohusiana na mali iwapo kitendo kilichofanyika au kilichoachwa kufanya naye kuhusiana na mali hiyo kilifanya kwa nia njema ya kudai haki na bila ya nia ya kuiba.

- 10.-(1)** Kulingana na masharti yaliyotajwa katika Kanuni hii kuhusiana na vitendo vya uzembe na kuacha kufanya, mtu hatawajibika kwa kosa la kijinai kwa kutenda au kuacha kutenda jambo ambalo limetokea bila ya idhini yake, au kwa tukio lililotokea kwa bahati mbaya.

- (2) Isipokuwa pale ambapo nia ya kusababisha matokeo fulani yametamkwa kuwa ni kielelezo kinachopelekea kutendeka kwa kosa, kwa ukamilifu wa kosa zima au sehemu ya kosa,kwa kutenda au kutotenda, matokeo yaliyokusudiwa kusababishwa na kutenda au kutotenda hayatahesabiwa.

(3) Isipokuwa kama imetamkwa vinginevyo, kwa nia ambayo mtu amemshawishi kutenda au kuacha kutenda kitendo, au kujenga dhamira, haitakuwa na umuhimu katika kuhusika kwake kwenye makosa ya kijinai.

Dhania isivyo  
kweli

**11.-**(1) Mtu ambaye anatenda au anaacha kutenda kitendo kwa nia njema na kwa sababu za msingi, lakini kwa kukosea, kwa kuamini kuwepo kwa hali yoyote ya vitu, hatawajibika kwa kosa la kijinai kwa kitendo au kutotenda zaidi ya kiwango kuliko kama hali halisi ya vitu ilikuwa kama alivyoamini.

(2) Kutumika kwa kanuni hii kunaweza kuondolewa kwa maelezo au masharti yasiyowazi kwenye sheria inayohusiana na jambo husika.

Kuchukuliwa  
kuwa na akili  
timamu

**12.** Kila mtu atachukuliwa kuwa na akili timamu, na atachukuliwa kuwa na akili timamu wakati wote mpaka pale itakapothibitishwa vinginevyo.

Ugonjwa wa  
akili  
Sheria Na. 31  
ya 1997  
Jedwali

**13.-**(1) Mtu hatawajibika kwa kutenda kosa la kijinai kwa kitendo au kuacha kutenda iwapo wakati wa kutenda kitendo hicho au kuacha kutenda alikuwa katika hali ya ugonjwa wowote unaoathiri akili yake ambapo:-

- (a) hawezি kujuu kitu anachokitenda;
- (b) hawezি kutambua kwamba hapaswi kutenda au kufanya jambo husika; au
- (c) hana uwezo wa kuzuia kitendo au kuacha kutenda.

(2) Mtu atachukuliwa kuwa ametenda kosa la jinai kwa kutenda au kutotenda kitendo ingawaje akili yake itakuwa imeathiriwa na magonjwa, kama ugonjwa ule haukumletea mojawapo au madhara yaliyotajwa ndani ya aya ya kifungu kidogo (1) kwa kufanya au kutokufanya.

Ulevi

**14.-**(1) Isipokuwa kama kimetamkwa katika kifungu hiki, kulewa hakutachukuliwa kuwa ni utetezi katika kosa lo lote la jinai.

(2) Kulewa kutakubaliwa kuwa utetezi kwa shitaka lo lote la jinai kama kwa sababu mtu atashitakiwa wakati wa kutenda au kutotendeka alikuwa hatambui kitu atendacho na:-

- (a) hali ya kulewa huko kulisababishwa bila ya hiari yake kwa makusudi au kwa kitendo cha uzembe wa mtu mwagine; au
- (b) mtu anayeshitakiwa kwa sababu ya ulevi , matatizo ya akili kwa muda au vinginevyo wakati anatenda au kuacha kutenda.

(3) Pale utetezi chini ya kifungu kidogo (2) utatolewa, na kama kesi itaangukia chini ya aya ya (a) ya kifungu kidogo hicho mshtakiwa atafutiwa mashitaka na kama kesi itaangukia kwenye aya ya (b) ya kifungu kidogo hicho masharti ya kanuni hii na ya Kanuni ya Mwenendo wa Jinai kuhusu wenda wazimu yatatumika.

(4) Kulewa kutachukuliwa maanani kwa madhumuni ya kutambua kama mtu aliyetenda kosa hilo alilifanya kwa kukusudia, maalum au vinginevyo, ambayo kama lisingetendeka lisingelichukuliwa kuwa ni kosa la jinai.

Sura ya 20

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "kulewa" kutachukuliwa kujumuisha hali iliyosababishwa na madawa ya kulevyo (nakotiki) au madawa yenye ulevi.

Umri mdogo  
Sheria Na. 4 ya  
1998 kif. 4

**15.-**(1) Mtu mwenye umri chini ya miaka kumi anachukuliwa kuwa hawezi kuwajibika kijinai kwa kutenda au kutotenda kosa.

(2) Mtu mwenye umri wa chini ya miaka kumi na mbili hatawajibika na kosa lolote la kijinai kwa kutenda au kutotenda jambo, isipokuwa kama itathibitishwa kwamba wakati wa kutenda au kuacha kutenda kitendo hicho alikuwa na uwezo wa kujuua kwamba hapaswi kukitenda au kuacha kukitenda.

(3) Mwanaume mwenye umri wa chini ya miaka kumi na mbili atachukuliwa kuwa hawezi kufanya tendo la ndoa.

Kinga ya  
jumla kwa  
Maafisa .  
Sheria Na 2 ya  
1970

**16.** Isipokuwa kama itaelezewa kwenye Kanuni hii, hakuna kitendo aujambo litakalofanywa au kuacha kufanya na afisa wa mahakama ata kama kufanya au kuacha kufanya au kuacha kufanya kwa makusudi ambacho kutimiza kazi zake zihusuzo mahakama,zitampeleke kutiwa hatiani kwa afisa wa mahakama kwa kutenda au kuacha kutenda..

Shurutisho.

**17.** Mtu hatawajibika kwa kosa la jinai kwa kosa kama kosa hilo limefanywa na wakosaji wawili au zaidi, na iwapo kitendo hicho kimetendwa au kimeachwa kutendwa kwa sababu tu kwa kipindi chote ambacho kitendo kikitendeka au kikiachwa kutendwa mtu huyo analazimishwa kukitenda au kuachakufanya kitendo kwa kutolewa vitisho na mkosaji mwengine au wakosaji wengine kwa kutishia kumuua papo hapo au kumtia dhara ya maumivu ya mwilini kama atakataa; lakini vitisho vya kumuumiza hapo baadaye hautachukuliwa kuwa ni utetezi wa kosa lolote.

Kulinda mtu  
au mali  
Sheria Na. 14  
ya 1980 kif. 6

**18.** Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 18A,, mtu hawezi kuwajibika kijinai kwa kitendo alichokifanya wakati wa kutimiza haki yake ya kujitetea au kumtetea mtu mwengine au kutetea mali kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi.

Haki ya  
kujilinda Sheria  
Na. 14 ya 1980  
kif. 7

**18A.-**(1) Kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hii kila mtu anayo haki ya:-

- (a) kujilinda ye ye binafsi au mtu mwengine dhidi ya kitendo chochote kinyume cha kisheria au shambulio au utumiaji nguvu dhidi ya mwili; au
- (b) kulinda mali yake au mali yoyote iliyo chini ya umiliki wake, himaya wake, au chini ya uangalizi wake au mali ya mtu mwengine yeyote dhidi ya kuchukuliwa isivyo halali au kuharibiwa aukufanyiwa fujo.

(2) Katika kifungu hiki, neno "mali ya mtu mwengine yeyote " itajumuisha mali yeyote inayomilikiwa na Serikali au Shirika la Umma au ya mwajiri au mali inayomilikiwa kwa pamoja

na jumiya inayoujumuisha watu chama cha ushirika au kijiji kilichosajiliwa au kisichosajiliwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa.

Kutumia nguvu  
katika kujilinda  
Sheria Na. . 14  
ya 1980 kif. 7

Pale haki ya  
kujilinda  
inapozidi na  
kusababisha  
kifo  
Sheria Na. 14  
ya 1980 kif. 7

**18B.-**(1) Katika kutumia haki ya kujilinda mwenyewe au kumtetea mtu mwingine au kutetea mali, mtu atatakiwa tu kutumia nguvu za kiasi zinazostahili ulinzi husika.

(2) Mtu atawajibika kuwa ametenda kosa la jinai kwa kosa lolote litakalotokana na matumizi ya nguvu kupita kiasi katika kujilinda au anapomlinda mtu mwingine au anapolinda mali.

(3) Mtu yeyote atakayesababisha kifo cha mtu mwingine kutookana na matumizi ya nguvu kupita kiasi katika kujilinda, anakuwa ametenda kosa la kuua bila kukusudia.

**18C.-**(1) Haki ya kujilinda au kumlinda mtu mwingine au kulinda mali itatumika kwa mtu yeyote ambaye katika kutumia haki hiyo, atasababisha kifo au dhara kubwa kwa mtu mwingine na mtu huyo atakayefanya , atakuwa amefanya hivyo kwa nia njema na akiamini alikuwa na sababu ya msingi kwamba kitendo chake kilistahili ili kuikoa maisha yake, kiungo chochote cha mwili wake au kuokoa maisha au kiungo chake au maisha au kiungo cha mtu mwingine au mali, katika hali ambayo:-

- (a) kitendo halali kilikuwa katika hali ambayo kinaweza kusababisha hofu ya kifo chake mwenyewe au kifo cha mtu mwingine kinaweza kusababishwa na matokeo ya kitendo hicho;
- (b) kitendo halali kilikuwa katika hali ambayo ambayo kinaweza kusababisha hofu kwamba dhara kwenye mwili wake au mwili wa mtu mwingine yanababishwa na matokeo ya kitendo hicho;
- (c) kitendo kinyume cha sheria kinachofanyika ni kwa nia ya kubaka au kufanya tendo la ndoa kinyume na maumbile;
- (d) kitendo kinyume cha sheria ni kwa nia ya kuteka nyara au kutorosha; au
- (e) kitendo kinyume cha sheria ni kuvunja na kuingia au ungang'anyi au kuchoma moto au kosa lolote la kijinai lenye kuhatarisha maisha au mali.

(2) Iwapo katika kutumia haki ya kujilinda kwa mujibu wa Kanuni hii, mtu anayetumia haki hii na yuko katika mazingira ambayo hawesi kujilinda kikamilifu bila ya kuleta madhara kwa mtu asiye na hatia au mali, haki yake ya kujilinda itajumuisha hatari hiyo inayoweza kutokea.

Kutumia nguvu  
katika  
kukamatwa

**19.** Iwapo mtu yeyote anashtakiwa kwa kosa la jinai linalotokana na kukamatwa ua kujaribu kumkamata mtu ambaye anapinga kukamatwa au anajaribu kuepuka kukamatwa, mahakama itaweza katika kutafakari kama njia zilizotumiwa zilikuwa zinafaau kiasi cha nguvu kilichotumiwa ili kumkamata mtu huyo zilikuwa kinafa, kwa itazingatia uzito wa kosa ambalo amefanya au lililofanywa na mtu huyo na mazingira ambapo kosa

hilo lilikuwa likifanywa au limefanywa na mtu huyo.

Shurutisho  
kutoka kwa  
mume

**20.** Mwanamke aliyeolewa hawezi kuepuka kuwajibika kwa kutenda kosa la jinai kwa kutenda au kuacha kufanya kitendo kwa sababu tu kwa kutenda au kutotendeka huko kumefanyika mbele ya mumewe wake, lakini kwenye shtaka dhidi ya mke kwa kosa lolote lisilokuwa la uhaini au la mauaji; utakuwa ni utetezi mzuri wa kuthibitisha kwamba kosa hilo lilifanywa mbele na kwa kushurutishwa na mumewake.

Mtu  
kutokuadhibiw  
a mara mbili  
kwa kosa  
lilelile  
Sheria Na. 49  
ya 1955 kif. 3

**21.** Mtu hawezi kuadhibiwa mara mbili, amachini ya vifungu vy  
kanuni hii au chini y masharti ya sheria nyingine yoyote ile, kwa kosa lile  
lile.

Wakosaji  
wakuu

### SURA YA TANO WASHIRIKI KWENYE MAKOSA

**22.-**(1) Pale ambapo kosa limetendeka, kila mmoja wa watu wafuatao watachukuliwa kwamba ameshiriki katika kutendeka kwa kosa hilo na watakuwa na hatia, na wanaweza kushtakiwa kwa kutenda ambao ni-

- (a) kila mtu ambaye anafanya kitendo au ambaye anaacha kufanya kitendo ambacho kinasababisha kosa;
- (b) kila mtu ambaye anafanya kitendo au anaacha kufanya kitendo kwa dhumuni la kumuwezesha au kumsaidia mtu mwingine kufatenda kosa hilo;
- (c) Kila mtu ambaye anamsaidia au anamshawishi mtu mwingine katika kutenda kosa;
- (d) Mtu yejote ambaye anamshauri au anamchukua mtu mwingine yejote kutenda kosa, katika mazingira yoyote anaweza kushtakiwa labda kwa kutenda kosa au kwa kushauri au kusaidia kutendeka kwa kosa.

(2) Kupatikana na hatia ya kushauri au kusaidia kutendeka kwa kosa kunafanya matokeo yale yale katika hali zote kama kupatikana na hatia ya kutenda kosa.

(3) Mtu yejote ambaye anasababisha mtu mwingine kutenda au kutotenda kitendo chochote cha namna ambayo, kama atakuwa amefanya kitendo yejote mwenyewe au kutofanya kitendo hicho kitapelekea kosa kwa upande wake, atakuwa na hatia ya kosa la namna hiyo hiyo na atapewa adhabu ile ile kana kwamba yejote mwenyewe ndiye ametenda kitendo hicho au ameacha kutenda

Makosa  
yanayotendwa

**23.** Pale watu wawili au zaidi wanakuwa na nia moja ya kutimiza

na wakosaji  
walioshirikiana  
katika shitaka  
lenye kusudio  
moja

Kumshawishi  
mwingine  
kutenda kosa

kusudio lisilo halali na kwa kuungana na mwenzake , na katika kutimiza kusudio hilo, kosa linatendeka kwa namna ambayo kutendeka kwa kosa hilo yalikuwa ni matokeo la kutimizwa kwa kusudio hilo, kila mmoja wao atachukuliwa kuwa ametenda kosa hilo.

**24.** Pale mtu anamshauri mtu mwingine kutenda kosa, na kosa likatendeka baada ya ushauri huo na mtu huyo alioutoa, haijalishi kama kosa lililotendeka ni sawa na lile aliloshauriwa au ni tofauti, au labda kosa hilo linatendwa katika namna aliyoshauriwa au katika namna tofauti, iliyotolewa katika namna mojawapo kwamba matendo yaliyopelekea kutendeka kwa kosa lililotendeka ni matokeo yamkini ya kutolewa kwa ushauri na kwa jinsi yoyote mtu aliyetoka ushauri atachukuliwa kumshauri mtu mwingine kutenda kosa ambalo amelitenda ye..

#### SURA YA SITA ADHABU

Aina za adhabu

**25.** Adhabu zifuatazo zinaweza kutolewa na mahakama:-

- (a) kifo;
- (b) kifungo;
- (c) kuchapwa viboko;
- (d) kutoza faini;
- (e) kunyang'anywa mali kama adhabu kwa kosa;
- (f) kulipa fidia;
- (g) dhamana kwa kutunza amani na kuwa na tabia njema, au kwa kuhudhuria kupewa hukumu;
- (h) adhabu nyingineyo yoyote inayotolewa na Kanuni hii au sheria nyingineyo yoyote.

Hukumu ya  
kifo  
Sheria Na. 55  
ya 1963  
Nyong. 6 Na.  
31 ya 1997  
Nyong; Na. 9  
ya 2002  
Nyong.

**26.-**(1) Pale mtu yeyote amehukumiwa kifo, hukumu hiyo itaelekeza kwamba mtu huyo anyongwe kwa kitanzi mpaka afe:

Isipokuwa kwamba, endapo mwanamke aliyehukumiwa adhabu ya kifo atakuwa mjamzito, mahakama itachunguza ukweli huo na, endapo mahakama itajiridhisha kuwa ni mjamzito adhabu itakayotolewa dhidi yake itakuwa ni kifungo cha maisha badala ya adhabu ya kifo.

(2) Adhabu ya kifo haitatamkwa au kuandikwa dhidi ya mtu yeyote ambaye, wakati wa kufanya kosa mtu huyo aliquwa chini ya umri wa miaka kumi na nane, lakini badala ya hukumu ya kifo, mahakama itamhukumu mtu huyo kuwekwa kizuizini wakati wa msamaha wa Rais, na ikiwa atahukumiwa hivyo atawajibika kuzuiwa katika sehemu hiyo na chini ya masharti ambayo Waziri mwenye dhamana juu ya mambo ya sheria atakavyoamuru, na wakati akiwa katika kizuizi hicho atahesabiwa kuwa katika uangalizi halali.

(3) Pale ambapo mtu amehukumiwa kuwekwa kizuizini wakati wa msamaha wa Rais kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2), jaji anayesimamia kesi hiyo atapeleka kwa Waziri mwenye dhamana juu ya mambo ya sheria

nakala ya maandishi ya ushahidi uliochukuliwa katika mwenendo wa kesi, ikiwa na ripoti ya maandishi yaliyosainiwa na yeye na yenyé mapendekezo au maoni juu ya jambo hilo kama atakavyoona inayafaa kufanya.

(4) Msimamizi Mkuu wa gereza au sehemu yoyote ambayo mtu mwenye umri chini ya miaka kumi na nane amewekwa kizuijini kwa maagizo ya Waziri chini ya kifungu kidogo cha (2), atalazimika kutayarisha ripoti ya maandishi kwa Waziri kuhusu hali, historia na tabia ya mtu huyo baada ya kumalizika kwa muda wa miaka kumi baada ya maagizo ya Waziri.

(5) Baada ya kupokea taarifa na kufanyia kazi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4), Waziri anaweza kuamuru mtu huyo aliye chini ya miaka kumi na nane kuachiliwa huru au vinginevyo kushughulikiwa kwa kwa masharti ya kubakia chini ya uangalizi mahali popote au mtu ye yoyote na kwa kuzingatia masharti mengine yoyote kwa ajili ya kuhakikisha usalama na hali ya maisha ya mtu huyo na umma kama Waziri atakavyoona inafaa.

Kifungo

**27.-(1) [Kimerukwa kwa mujibu wa kif.30 Sura ya 357].**

Sura 291

(2) Mtu anayewajibika kwa adhabu ya kifungo anaweza kuhukumiwa kulipa faini kama nyongeza au badala ya kifungo, au pale mahakama inapoamua chini ya Sheria ya Huduma za Jamii, huduma kwa jamii chini ya amri ya kutoa huduma kwa jamii.

Adhabu ya  
viboko  
Sura 90  
Sura.17  
Sura.11  
Nyongeza ya 6

**28.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Kima cha Chini cha Adhabu, pale katika kanuni hii inatamka kwamba mtu ye yoyote atahukumiwa adhabu ya viboko, adhabu hiyo, kama itatolewa, itatekelezwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Adhabu ya Viboko.

Faini  
Sheria Na. 13  
ya 1972  
Nyong.

**29.** Pale faini imetolewa chini ya sheria yoyote, pasipokuwa na kifungu maalum kuhusu faini katika sheria hiyo masharti yafuatayo yatatumika:-

- (a) pale ambapo hakuna kiwango cha fedha kimetajwa kitatozwa kiasi gani, kiasi cha faini kinachoweza kutozwa hakitakuwa na ukomo, lakini hakitakuwa kikubwa kupita kiasi;
- (b) katika kosa linaloaadhibiwa kwa adhabu ya faini au muda wa kifungo, utozaji wa faini au muda wa kifungo litakuwa ni jambo litakaloamuliwa na mahakama;
- (c) katika kosa adhabu yake ni kifungo vilevile faini kwa ambapo mkosaji amehukumiwa adhabu ya faini pamoja au bila ya kifungo na kwa kila kosa ambalo limetolewa adhabu ya faini tu na mkosaji akahukumiwa adhabu ya kulipa faini, mahakama inayopitisha hukumu hiyo inaweza kuamua -
  - (i) kuamuru katika hukumu yake kwamba kukikosekana malipo ya faini mkosaji atatumikia kifungo kwa muda fulani, ambapo kifungo hicho kitaongezwa kwenye adhabu nyininge ye yoyote ya kifungo ambacho

- amehukumiwa nacho au ambayo anaweza  
kuhukumiwa chini ya tahafifu ya adhabu; na  
(ii) kutoa hati ya kutoza kiasi cha faini kwenye mali  
isiyohamishika na inayohamishika ya mkosaji kwa  
kuishika na kuuza chini ya hati:

Isipokuwa kwamba iwapo hukumu inaelekeza kwamba mkosaji  
asipolipa faini atahukumiwa kifungo, na iwapo mkosaji huyo  
ametumikia kifungo hicho chote kwa kutokulipa, hakuna mahakama  
itakayotoa hati ya kushika na kuuza mali ya mkosaji isipokuwa kwa  
sababu maalum ambazo zitaandikwa kimaandishi kama itaonekana ni  
lazima kufanya hivyo;

- (d) muda wa kifungo ulioamriwa na mahakama kwa ajili ya  
kukosekana malipo ya kiasi chochote cha fedha  
kilichohukumiwa kulipwa baada ya kupatikana na hatia au kwa  
ajili ya kukosekana mali ya kuuzwa ili kutosheleza kiasi hicho  
cha fedha kitakuwa ni kipindi ambacho mahakama itaona kuwa  
inatenda haki juu ya shauri, lakini haitazidisha katika shauri  
lolote kikomo kilichowekwa cha viwango kifuatavyo:-

Faini isiyozisi Sh. 5,000/-

siku 14

Faini inayozidi Shs. 5,000/- lakini haizidi Shs.50,000/= miezi 2

Faini inayozidi Shs. 50,000/- Shs.100,000/= Miezi 6

Faini inayozid Shs. 100,000/- lakini haizidi 500,000/- miezi 12

Faini inayozidi shs. 500,000/-

Miezi 24 months

- (e) Kifungo ambacho kitatolewa kwa kushindwa kulipa faini  
kitakoma pale ambapo labda faini imelipwa au imetozwa kwa  
taratibu za sheria.

Kunyang'anyw  
a mali  
R.L. Sura ya  
400 kif. 15;  
R.L. Sura ya .  
500 kif. 12

**30.** Pale ambapo mtu yeyote amehukumiwa kwa kosa chini ya  
kifungu cha 111 au 112, mahakama inaweza, ikiwa ni nyongeza au badala ya  
, adhabu yoyote ambayo inaweza kutolewa, kuamuru mali yoyote  
kuchukuliwa na Jamhuri kwa mali yoyote inayohusika na utendaji wa kosa ,  
au iwapo mali hiyo haiwezi kuchukuliwa au kupatikana, kiasi cha fedha  
ambacho mahakama itakadiria kuwa ni thamani ya mali na malipo ya kiasi  
cha fedha kilichoamriwa kuchukuliwa kinawenza kufanywa kwa utaratibu  
ulio sawa na kwa kuzingatia mazingira sawa kama katika kesi ya kulipa  
faini.

Fidia  
Sura ya 20

**31.** Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 348 cha Sheria ya  
Mwenendo wa Makosa ya Jinai, mtu yeyote ambaye anapatikana na hatia ya  
kutenda kosa anaweza kuhukumiwa kulipa fidia kwa mtu yeyote  
aliyejeruhiwa na kosa lake na fidia hiyo inaweza kuwa ni nyongeza ya, au  
ni mbadala wa adhabu nyingine yeyote.

Gharama  
Sura ya 20

**32.** Kwa kuzingatia vikomo vilivyotolewa na kifungu cha 345 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, mahakama inaweza kumuamuru mtu yeyote aliyepatikana na hatia kwa kutenda kosa kulipa gharama na gharama zote zinayoambatana na mashitaka yote au sehemu ya mashitaka.

Dhamana kwa  
ahadi ya  
kutunza amani

**33.** Mtu ambaye amepatikana na hatia kwa kosa ambalo adhabu yake sio adhabu ya kifo anaweza, badala ya, au kwa nyongeza ya adhabu nyingine yoyote ambayo anastahili, anaweza kuamriwa kutoa ahadi mbele ya wadhamini au bila ya wadhamini ya dhamana ya kiasi cha fedha ambacho mahakama itaona kinafaa, ikimtaka kutunza amani na kuwa mwenye tabia njema kwa muda utakaopangwa na mahakama, na anaweza kuamriwa kufungwa gerezani hadi pale atakapotoa ahadi na wadhamini, kama atakavyo amriwa, ataingia katika; lakini kwamba kifungo kwa kutofuata dhamana hakitzidi kipindi cha mwaka mmoja, na hautakuwa, pamoja na muda uliowekwa wa kifungo, kama utakuwepo, kuongeza kwa kipindi kirefu kuliko kipindi kirefu ambacho ambacho angeweza kuhukumiwa kufungwa bila kulipa faini.

Kimefutwa

**34.** [Kimefutwa na Sheria Namba 5 ya mwaka 1961, kifungu cha 2.]

Adhabu ya  
jumla kwa  
makosa  
ambayo adhabu  
zake  
hazijafafanuliw  
a

**35.** Pale katika Kanuni hii hakuna adhabu iliyotamkwa kwa kosa lolote, kosa hilo litaadhibiwa kwa adhabu ya kifungo kisichozidi miaka miwili au kulipa faini au vyote viwili kwa pamoja.

Adhabu za  
pamoja  
isipokuwa  
kama  
itaamuriwa  
vinginevyo

**36.** Pale mtu baada ya kupatikana na hatia anahukumiwa kwa kosa lingine, aidha kabla ya hukumu kutolewa ya kosa la kwanza au kabla ya kumalizika kwa adhabu hiyo, tofauti na adhabu ya kifo au ya viboko ambayo imetolewa dhidi yake chini ya makosa yanayofuatana, adhabu hizo zitatekelezwa zote kwa pamoja na adhabu baada ya kumalizika kwa adhabu ya awali isipokuwa kama mahakama itaamuru iende pamoja na adhabu za awali au sehemu ya yeyote ya adhabu hiyo:

Isipokuwa kwama mahakama haitaamuru kwamba adhabu ya kifungo kwa kushindwa kulipa faini itekelezwe kwa wakati mmoja na adhabu iliyotangulia chini ya kifungu cha 29-(c)-(i) au sehemu yoyote ya adhabu hiyo.

Mfungwa  
aliyetoroka  
kutumika  
kifungo  
kisichoisha  
pale  
anapokamatwa.

**37.** Pale adhabu inatolewa kwa mujibu wa Kanuni hii dhidi ya mfungwa aliyetoroka adhabu, kama ni ya kifo, faini au ya viboko, kwa kizingatia masharti yaliyopo katika Kanuni hii, zitaanza kutumika mara moja na, iwapo ni adhabu ya kifungo, itaanza kutumika kwa kuzingatia masharti yafuatayo, yaani:-

(a) iwapo adhabu mpya ni kali zaidi ya adhabu ya awali ambayo mfungwa alikuwa anatumikia wakati anatoroka, adhabu mpya

- itaanza kutumika mara moja na atatumikia kipindi chote cha kifungo ambacho kilikuwa kimebaki wakati akitoroka baada ya kumalizika kutumikia kifungo chake kipy;
- (b) endapo adhabu mpya si kali kuliko kifungo alichokuwa akikitumikia wakati alipotoroka, adhabu mpya itaanza mara baada ya kutumikia adhabu ya kifungo kwa kipindi cha ziada ambacho ni sawa na sehemu ya adhabu ya kifungo cha zamani ambacho alikuwa bado hajamaliza wakati alipotoroka.

Kuachiwa bila  
masharti na  
kuachiwa na  
masharti  
Sheria Na. 5 ya  
1961

**38.-**(1) Pale mahakama ambayo imemtia mtu hatiani, ina maoni kuwa, kwa kuzingatia mazingira kosa na tabia ya mkosaji huyo, inaona kwamba haifai kutoa adhabu, na kwamba si sawa kutoa amri ya kumuweka mkosaji huyo chini ya uangalizi, mahakama inaweza kutoa amri ya kumuachia mtu huyo bila ya masharti au mahakama inaweza, kumuachia kwa sharti kwamba asitende kosa ndani ya muda utakaowekwa, ambao hautazidi miezi kumi na mbili toka tarehe ya amri hiyo.

(2) Amri ya kumuachia mtu kwa masharti kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) ambayo itajulikana kama “amri ya kuachia kwa sharti” na muda uliotajwa katika amri yoyote utajulikana kama “muda wa kuachiwa kwa sharti”.

(3) Kabla ya kutoa amri ya kuachiwa kwa sharti, mahakama itamueleza mkosaji kwa lugha ya kawaida kwamba kama atatenda kosa jingine ndani ya muda wa kuachiwa kwa masharti, atapewa adhabu kwa kosa alilolitenda mwanzoni.

(4) Pale amri ya kumuachia mkosaji inatolewa chini ya kifungu hiki, mahakama inaweza kumuamuru kulipa fidia ya hukumu iliyotolewa chini ya kifungu cha 31 au gharama zozote zilizoamriwa chini ya kifungu cha 32 cha Kanuni hii.

Kutenda kosa  
kwa mara  
nyingine  
Sh.1961 Na. 5  
kif.3

**38A.-**(1) Iwapo jaji au hakimu anaona kwamba mtu ambaye amri ya kufutiwa mashtaka kwa masharti ilitolewa dhidi yake au bila masharti amepatikana na hatia nyingine akiwa chini ya kipindi cha amri ya kufutiwa mashtaka kwa masharti, anaweza baada ya kupokea taarifa hiyo kwa maandishi na chini ya kiapo, kumtaka mtu huyo afike mahakamani katika sehemu na muda utakaotajwa au anaweza kutoa amri ya kukamatwa kwa mtu huyo.

(2) Hati ya kuitwa shaurini au hati ya kumkamata inayotolewa chini ya kifungu hiki itamtaka mtu huyo aliye na hatia kuhudhuria au kuletwa mbele ya mahakama ambayo ilitoa amri ya kuachiwa kwa sharti.

(3) Pale mtu ambaye ameachiliwa kwa sharti ametiwa hatiani na hakimu kwa kosa alilotenda ndani ya muda wa kuachiwa kwa masharti, hakimu anaweza kuamuru kuwekwa kwa mtu huyo mahabusu au kuamuru aachiliwe kwa dhamana, pamoja na wadhamini au bila ya wadhamini, mpaka atakapofikishwa au kuhudhuria mbele ya mahakama ambayo imetoa amri hiyo ya kuachiwa kwa masharti..

(4) Pale ambapo inathibitishwa kwa kiwango cha kuiridhisha mahakama ambayo imetoe amri ya kuachiwa kwa sharti kwamba mtu ambaye amri hiyo imetolewa amepatikana na hatia kwa kosa ambalo amelitenda ndani ya muda wa kuachiliwa kwa sharti, mahakama inaweza kutoa hukumu yoyote ambayo ingeliweza kutoa kwake iwapo mtu huyo amehukumiwa mara na mahakama hiyo kwa kosa la mwanzo.

(5) Pale mtu ambaye amri ya kuachiliwa kwa sharti imetolewa na hakimu dhidi yake, ametiwa hatiani na Mahakama kuu kwa kosa ambalo amelitenda ndani ya muda ambao alikuwa ameachiwa kwa sharti, Mahakama Kuu itatoa hukumu ambayo mahakama iliyotoa amri hiyo ya kuachiliwa kwa masharti itatolewa kana kwamba atakuwa ametiwa hatiani na mahakama ya kosa la mwanzo.

(6) Pale ambapo chini ya masharti ya kifungu hiki mtu ambaye ameachiwa kwa sharti anahukumiwa adhabu kwa kosa ambalo lilipelekea kutolewa kwa amri ya kuachiliwa kwa sharti, amri hiyo haitakuwa na nguvu.

Matokeo ya  
kupatikana na  
hatia na  
kuachiwa

**38B.-**(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (2), pale ambapo mtu anapatikana na hatia ya kutenda kosa na kuachiwa labda kabisa au kwa sharti chini ya masharti ya kifungu cha 38, kupatikana kwake na hatia kwa kosa hilo kutachukuliwa kuwa sio hatia kwa dhumuni lingine lolote tofauti na madhumini ya mashauri ambayo amri hiyo imetolewa na kwa mashauri yoyote yanayofuata ambayo yanaweza kuchukuliwa dhidi yake chini ya masharti ya kifungu cha 38A:

Alimradi kwamba pale ambapo mtu ambaye ameachiwa kwa sharti baadaye amehukumiwa chini ya kifungu cha 38A kwa kosa ambalo lilipelekea kutolewa kwa amri ya kuachiliwa, kifungu hiki kitakoma kutumika kutohuna na kosa hilo na atachukuliwa kwamba ametiwa hatiani kwenye tarehe ya hukumu hiyo.

(2) Hakuna chochote katika kifungu hiki ambacho kitaathiri:—

- (a) haki ya mtu ye yoyote ambaye amepatikana na hatia na kuachiwa kabisa au kwa sharti au kukata rufani dhidi ya kutiwa hatiani kwake au kuitegemea hukumu hiyo iwe kinga dhidi ya mashitaka yoyote yaliyotokea dhidi yake kwa kosa hilo hilo; au
- (b) kurejesha au kurudisha mali yoyote kama matokeo ya kutiwa hatiani kwa mtu huyo.

SEHEMU YA PILI  
MAKOSA YA JINAI

*Kigawo cha Kwanza – Makosa dhidi ya Amri za Serikali*

## SURA YA SABA

### UHAINI NA MAKOSA MENGINE DHIDI YA SERIKALI

Sheria ya Uhaini.  
Na.2 ya 1970  
Jedwali

**39.-**(1) Mtu yeyote ambaye yumo ndani ya Jamhuri ya Muungano

- (a) akiwa ndani ya Jamhuri ya Muungano au popote, anamuua au anajaribu kumuua Rais; au
- (b) akiwa ndani ya Jamhuri ya Muungano anaanzisha vita dhidi ya Jamhuri ya Muungano,

atakuwa na hatia ya kosa la uhaini na atawajibika kwa adhabu ya kifo.

(2) Mtu yeyote ambaye, yumo katika ndani ya Jamhuri ya Muungano, akiwa ndani ya Jamhuri ya Muungano au popote, anajenga nia kusababisha au kuwezesha kusababishwa, au anajenga nia ya kuchochea, anashawishi, shauri au kuusia mtu yeyote au kikundi cha watu kusababisha au kuwezesha kusababishwa yoyote kati ya matendo au malengo yafuatayo, yaani:-

- (a) kifo, kumlemaza au kumjeruhi, au kufungwa au kumzuia, Rais;
- (b) kumwondoa Rais madarakani isivyo halali kutoka katika wadhifa wake wa Urais au kumwondolea ufahari, heshima na jina la Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ya Jamhuri ya Muungano;
- (c) kupindua kwa njia zisizo halali, Serikali ya Jamhuri ya Muungano; au
- (d) kutishia Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Bunge na Mahakama ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano,

na kubainisha nia hiyo kwa kuchapisha maandishi or machapisho au kwa kitendo chochote cha siri kinachojionyesha cha hali yoyote, atakuwa na hatia ya kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifo.

(3) Mtu yeyote ambaye, yumo katika utii wa Jamhuri ya Muungano-

- (a) aliye na mshikamno na maadui wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au anawapa msaada au hifadhi ndani ya Jamhuri ya Muungano au kwingineko;
- (b) anachochea, aidha ndani ya Jamhuri ya Muungano au kwingineko, mtu yeyote aivamie Jamhuri ya Muungano kwa kutumia jeshi; au
- (c) anabeba silaha ndani ya Jamhuri ya Muungano kwa amri, kwa nia ya kutumia nguvu ya kuizua, kuilazimisha Serikali ya Jamhuri ya Muungano kubadilisha vigezo au ushawishi wake, au kwa nia ya kulazimisha au kuzuia au kutishia, Serikali ya Jamhuri ya Muungano,

atakuwa na hatia ya kosa la uhaini na atawajibika kwa adhabu ya kifo.

(4) Mtu yeyote ambaye, yumo katika utii wa Jamhuri ya Muungano, akiwa ndani ya Jamhuri ya Muungano au popote, kwa nia ya

kumsaidia adui wa Jamhuri ya Muungano anafanya kitendo chochote kinacholenga au kinachoweza kutoa msaada kwa adui huyo, au kuingilia kwa maelekezo Serikali ya Jamhuri ya Muungano, au kuzuia operesheni ya Majeshi ya Ulinzi au Jeshi la Polisi, au kuhtatarisha maisha, ana hatia ya kosa la uhaini na atawajibika kwa adhabu ya kifo.

Makosa ya uhaini.  
Sheria Na.. 2 ya  
1970

**40.** Mtu yejote ambaye atakuwa chini ya utii kwa Jamhuri ya Muungano, akiwa ndani ya Jamhuri ya Muungano au popote, kwa nia ya kutoa msaada kwa adui yejote wa Jamhuri ya Muungano, ana hatia ya kosa la uhaini kwa mujibu wa kifungu cha 39, na atawajibika kwa adhabu ya kifo.

Kuficha uhaini

**41.** Mtu yejote ambaye:-

- (a) anakuwa mficha uhaini au makosa ya kihaini; au
- (b) anafahamu kuwa mtu yejote ana nia ya kutenda kosa la uhaini au kufanya uhaini anashindwa kutoa taarifa pamoja na jitihada zote za afisa tawala au hakimu au afisa wa polisi , au anashindwa kutumia jitihada zake zote kuzuia kutendeka kwa kosa,

atakuwa na hatia ya kosa liitwalo “kuficha uhaini” na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha.

**42.** [Kimeachwa.]

Kudhamini  
shughuli za kivita.  
Sheria. Na. 2 ya  
1970

**43.** Mtu yejote ambaye bila ya mamlaka halali anabeba, au anafanya maandalizi ya kubeba, au kusaidia au kushauri kubeba au utayarishaji wa kubeba vifaa vya vita vyovjyote vile au shughuli za kivita dhidi ya mtu yejote au kikundi chochote, ndani ya Jamhuri ya Muungano, atakuwa ana hatia ya kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha.

**44.** [Kimebadilishwa na C.A. 2 ya 1962 kif. 36.]

Kuchocha Uasi  
R.L Sura. 500  
Kif. 8; Sher. Na.  
24 ya 1966  
Jedwali la Pili.

**45.** Mtu yejote ambaye, kwa kushauriwa anajaribu kutimiza kati ya madhumuni haya yafuatayo, yaani:-

- (a) kumshawishi afisa yejote wa Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza au Jeshi la Kujenga Taifa aache wajibu na utii wake juu ya Jamhuri; au
- (b) kumchochea mtu yejote kutenda kitendo cha uasi au kutenda kitendo chochote cha uhaini au cha uasi; au
- (c) kumchochea mtu yejote kufanya au kujitahidi kufanya mikusanyiko ya uasi,

Ana hatia ya kosa na anawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha.

Kuwasaidia  
Wanajeshi au  
maafisa wa polisi

**46.** Mtu yejote ambaye:-

- (a) anasaidia, anaelekeza au anashiriki katika tendo lolote la uasi

katika vitendo nya uasi  
Sher. Na. 24 ya 1966 Jedwali la Pili

- wa askari Polisi, askari Magereza au askari wa Jeshi la Kujenga Taifa; au
- (b) anachochea askari Polisi yeyote, askari Magereza yeyote au askari yeyote wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa kumshawishi atende kosa au kutotii amri halali inayotolewa na afisa mwandamizi , ana hatia ya kosa. .

Kuwashawishi wanajeshi au maofisa wa polisi kutoroka Sheria Na. 24 ya 1966 Nyong ya Pili.

**47.** Mtu yeyote ambaye kwa njia ya namna yoyote ile, moja kwa moja au vinginevyo:-

- (a) anamuwezesha au anamshawishi au anajaribu kumshawishi atoroke ; au
- (b) anamsaidia, anashawishi au ni mshiriki katika utoro wa; au
- (c) Kutokana na kuamini kwamba ni mtoroshaji , mfichaji au anasaidia kumficha,

Afisa yeyote wa Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza au Jeshi la Kujenga Taifa, ana hatia ya kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miezi sita.

Kusaidia mateka kwa vita kutoroka Sura. 500 Kif. 36

**48.** Mtu yeyote ambaye:-

- (a) kwa kujuua na akiwa na kufahamu anamsaidia adui wa Jamhuri ya Muungano ambaye ni mateka wa kivita, aidha mateka husika kuwa alikuwa ndani ya kizuizi cha gereza au alikuwa kwinginepo kwa mujibu wa utaratibu wa *parole*, atoroke kutoka katika gereza lake au sehemu ya kizuizi chake, au kutoka sehemu yake ya *parole* atoroke kutoka Tanzania Bara, atakuwa ametenda kosa, na anaweza kuhukumiwa kifungo cha maisha;
- (b) kwa uzembe na isivyo halali, anaruhusu kutoroka kwa mtu aliyetajwa katika aya (a) ana hatia ya kosa.

Tafsiri ya kitendo kinachoonyesha

**49.** Iwapo makosa yoyota yaliyotajwa katika Sura hii, pale kujitokeza kwa kitendo chochote cha siri kinachoonyesha nia ya kutekeleza azma yoyote ya kutenda kosa, kitendo chochote cha kula njama na mtu yeyote kwa nia ya kutimiza azma husika na kila kitendo chochote kinachofanywa kuendeleza azma hiyo inayofanywa na mtu yeyote anayehusika katika njama itachukuliwa kuwa ni kitendo kinachoonyesha na kubainisha nia.

Vimefutwa

**50.-54.** [Vimefutwa na Sheria Na. 3 ya mwaka 1976 kif. 55<sup>1</sup>]

Nia ya kufanya uchochezi Sheria Na 18 ya 1950 kif. 2; Sura 455

**55.-(1)** Nia ya kufanya uchochezi ni nia ya:-

- (a) ya kuleta chuki au kudharau au kuchocheza, kutopenda dhidi ya mamlaka halali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali yake;

Sura ya 229

<sup>1</sup> Angalizo: Vifungu 51, 52, 53, 54, 56, 57, 58, 63 na 63A vilitungwa upya katika Sheria ya Magazeti.

- au
- (b) kuwatia hamasa wakazi wowote wa Jamhuri ya Muungano ili kuleta mageuzi, kwa njia nyingine ya halali jambo lolote katika Jamhuri ya Muungano lililowekwa na sheria; au
- (c) kuleta chuki au kudharau au hamasa ovu ya kuwafanya dhidi ya utawala wa sheria katika Jamhuri ya Muungano; au
- (d) kupandisha hali ya kutoridhika au kudharau baina ya wakazi wa Jamhuri ya Muungano; au
- (e) kukuza hisia za nia mbaya na chuki baina ya aina mbali mbali za watu wa Jamhuri ya Muungano.
- (2) Kitendo, hotuba au tangazo halitahesabiwa kuwa ni la kichochezi kwa sababu tu linalenga katika:-
- (a) kuonyesha kwamba serikali imepotoka au imekosea katika mwenendo wake wowote; au
- (b) kuonyesha makosa au mapungufu katika serikali au Katiba ya Jamhuri ya Muungano au kama ilivyowekwa na sheria, au katika usimamiaji utoaji wa haki kwa lengo kurekebisha makosa hayo au upungufu huo; au
- (c) kuwashawishi wakati wowote wakazi wa Jamhuri ya Muungano kujaribu kwa njia ya halali kuleta megeuzo ya jambo lolote katika Jamhuri ya Muungano kama ilivyowekwa kwa sheria; au
- (d) kuonyesha, kwa nia ya kuvifuta, mambo yoyote yanayoleta au yenye mwelekeo wa kujenga hisia za nia mbaya na uadui baina ya aina mbali mbali za watu wa Jamhuri ya Muungano.
- (3) Katika kuamua endapo nia ya kitendo chochote kilifanywa au inayohusishwa na kitendo ilikuwa ya, maneno yoyote yatakayozungumzwa au nyaraka yoyote itakayo andikwa itahesabiwa kuwa ni ya uchochezi, na mtu ye yoyote atahesabiwa kuwa alinuia matokeo ambayo kwa hali ya kawaida yanatokana na kitendo chake kwa wakati na katika hali aliyoitenda mwenyewe

Vimefutwa

**56.-58.** [Vimefutwa na Sheria Namba 3 ya 1976 kif 55.]

Viapo visivyo  
halali ili kutenda  
makosa

**59.** Mtu ye yoyote ambaye:-

- (a) anatoa, au anakuwepo na kukubali, katika kutoa kiapo cha aina yoyote au kujihuisha katika maswala ya kiapo, inayoambatana na kumuunga mkono mtu ye yoyote anayeapishwa kutenda kosa lolote lenye adhabu ya kifo; au
- (b) anakula kiapo au anajihuisha, bila kulazimishwa kufanya hivyo,

Ana hatia ya kosa na anawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha.

Viapo vingine  
visivyo halali ili  
kutenda makosa

**60.** Mtu ye yoyote ambaye:-

- (a) anatoa, au anakuwepo na kukubali, kutoa kiapo cha aina yoyote au kujihuisha katika maswala ya kiapo, kwa malengo

ya kumzuia mtu anayeapishwa:-

- (i) kujihusisha na vitendo vya maasi au uchochezi;
  - (ii) kutenda kosa lolote ambalo adhabu yake si kifo;
  - (iii) kuvunja utulivu na amani ya umma;
  - (iv) kujiunga na chama chochote au shirikisho (muungano), linaloundwa kwa lengo la kufanya jambo lolote lililotajwa katika aya ndogo ya (i) hadi aya ya (iii) ya aya hii;
  - (v) kutii amri au elekezo kutoka katika kamati yoyote au kikundi cha watu ambacho hakikuanzishwa kihalali, au kutoka kwa kiongozi au kamanda au mtu yeyote asiye na mamlaka ya kisheria kuhusu jambo husika;
  - (vi) kushindwa kutoa taarifa au kutoa ushahidi dhidi ya wanachama, washiriki au mtu yeyote; au
  - (vii) kushindwa kuwataja au kuwezesha kugunduliwa kwa chama chochote kilichopo kinyume na sheria, au ushirika usio halali au kitendo chochote kinachovunja sheria, au vitendo vya ulishwaji viapo kinyume cha sheria au viapo haramu vilivyofanyika au ushiriki wa mtu yeyote katika uendeshaji wa viapo hivyo, au ushiriki wake au wa mtu mwingine yeyote katika viapo au ushiriki;
- (b) kula kiapo chochote husika au kujihusisha, bila kushurutishwa na mtu yeyote kufanya hivyo,

ana hatia ya kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

**61.** Mtu ambaye anakula kiapo au anatoa ahadi kama ilivyotajwa katika kifungu cha 60 hawezi kufanya kama utetezi wake kwa kudai kwamba alilazimishwa kufanya hivyo isipokuwa, ndani ya siku kumi na nne kuanzia siku alipokula kiapo hicho au, kama amezuiwa kwa nguvu au ugonjwa, ndani ya siku kumi na nne baada ya kuzuiwa huko anatamka kwa kiapo kwa kutoa taarifa mbele ya hakimu au, kama ni mtumishi wa jeshi la vita la Jamhuri ya Muungano katika Jeshi la Polisi, labda kwa taarifa hiyo au kwa taarifa mbele ya mkuu wake, yote anayoyajua kuhusu shauri hilo la kiapo ikiwa ni pamoja na watu waliokuwepo na mahali na muda ambao kiapo hicho kilifanyika;

**62.(1)** Mtu yeyote ambaye:-

- (a) bila ya ruhusa ya Waziri anayehusika na mambo ya ndani ya nchi anafundisha au anatoa mafunzo ya kijeshi kwa mtu mwingine yeyote juu ya kutumia silaha au kufanya mazoezi ya kivita au mwenendo wa kivita au kazi za kivita; au
- (b) anakuwapo kwenye mkutano wowote au mkusanyiko wa watu uliofanywa bila ruhusa ya Waziri anayehusika na mambo ya ndani ya nchi na kwa wa madhumuni ya kufundisha au kuchezesha kwatu mtu mwingine yeyote juu ya kutumia silaha au kufanya mazoezi au mwendo au kazi za kivita,

Kulazimishwa  
kama utetezi

Mafunzo ya  
kijeshi yasiyo  
halali .  
Sura ya 455 kif 20

atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya miaka saba.

- (2) Mtu yejote ambaye katika mkutano au mkusanyiko wowote uliofanywa bila ya ruhusa ya Waziri anayehusika na mambo ya ndani ya nchi anafundishwa au anachezeshwa kwata juu ya matumizi ya silaha au mwendo, au mabadiliko yoyote ya kazi za kivita au ambaye atakuwepo kwenye mkutano au mkusanyiko huo kwa makusudi ya kufundishwa au kuchezeshwa kwata mtu huyo atakuwa ana hatia ya kosa

Vimefutwa

**63. Vimefutwa na Sheria Na. 3 ya mwaka 1976 kifungu cha 55**

63.B.—(1) Mtu yejote ambaye katika mkusanyiko wowote atatoa maneno ambayo huenda yakaleta kutoridhika kati ya au wakazi wowote wa Jamhuri ya Muungano au kuleta hisia za chuki kati ya jamii mbalimbali za watu wa Jamhuri ya Muungano, mtu huyo atakuwa ametenda kosa na atawajibika kutoa faini isiyozidi shilingi elfu moja au kifungo cha muda usiozidi miezi kumi na mbili jela au vyote kwa pamoja;

Isipokuwa kwamba hakuna mtu atakayekuwa ametenda kosa chini ya masharti ya kifungu hiki ikiwa maneno yake aliyo yatoa yalikuwa tu kwa ajili ya moja au zaidi ya madhumuni yafuatayo, na uthibitisho huo utakuwa juu yake, hii ina maana kuwa ni:-

(a) kuonyesha kwamba Serikali imepotoshwa au imekosea katika mipango yake; au

(b) kutaja makosa au upungufu katika Serikali au sera za Serikali au Katiba ya Jamhuri ya Muungano kama ilivyo kisheria, au katika sheria yoyote au katika usimamiaji wa haki kwa kusudi la kutaka kusahihisha upungufu au makosa hayo;

(c) kushawishi wakazi wowote wa Jamhuri ya Muungano wajaribu kuleta mageuzi kwa njia ya halali ya jambo lolote katika Jamhuri ya Muungano; au

(d) kutaja kwa nia ya kuyaondosha mambo yoyote ambayo yameleta au yanaelekea kuleta chuki kati ya wakazi wowote wa Jamhuri ya Muungano au hisia ya chuki au uadui kati ya wakazi au jamii ya watu mbali mbali wa Jamhuri ya Muungano.

(2) kwa madhumuni ya kifungu hiki neno “mkusanyiko” lina maana ya

mkusanyiko wa watu saba au zaidi.

(3) Mtu hatashitakiwa kwa kosa chini ya kifungu hiki bila ya idhini ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

## SURA YA NANE

### MAKOSA YANAYOATHIRI MAHUSIANO NA NCHI ZA NJE NA UTULIVU WA NJE

Kimefutwa

**64.** Kimefutwa na Sheria Na. 3 ya mwaka 1976 kifungu cha 55.

Uandikishaji  
askari wa kivita  
kwa nchi za  
kigeni

**65.** Mtu yejote atakuwa ametenda kosa iwapo atatenda mojawapo ya matendo yafuatayo bila ruhusa ya Rais iwapo :-

- (a) atakayetayarisha au kufanya msafara wowote wa manowari au wa jeshi la vita kwenda kushambulia tawala za dola yoyote iliyio rafiki au atakayeshughulika na maandalio au kuweka au kusaidia au kuajiriwa katika cheo chochote katika msafara huo;
- (b) akiwa ni raia wa Tanzania, anakubali kufanya au kujihusisha na shughuli yoyote ya kijeshi la vita au ya kimanowari ya dola yoyote ngeni iliyoko katika vita au ama ni raia wa Jamhuri ya Muungano au siyo raia wa Jamhuri ya Muungano, atakayeshawishi; mtu mwingine yoyote kufanya au kujishughulisha na kazi za kijeshi au za kimanowari za dola hiyo ngeni iliyokwishatajwa;
- (c) akiwa ni raia wa Jamhuri ya Muungano, kuingia au kujipakia katika chombo chochote kwa nia ya kundoka katika Jamhuri ya Muungano kwa kusudi la kufanya kazi za kijeshi au za kimanowari za dola ngeni yoyote iliyio katika vita na dola ya kirafiki; raia au si raia wa Tanzania, atamshawishi mtu yejote mwingine kutoka au kuingia katika chombo chochote kwa nia ya kuondoka Tanzania na kwa kusudi kama hilo;
- (d) akiwa ni nahodha au mmiliki wa chombo akijua kama chombo chake kinapakia au kujishughulisha katika kupakia au chombo hicho kuna mtu ambaye si halali ; au
- (e) atakayeunda, kukubali kuunda, kuundisha, kutayarisha, kusafirisha au kuruhusu kusafirisha chombo chochote au atakayetoa ujumbe wowote kwa chombo chochote, kwa nia au kwa kujua au kuna sababu ya kutosha kuamini kwamba chombo hicho au ujumbe huo utatumika katika kazi za kivita au za kimanowari za dola ngeni iliyio katika vita na dola yoyote ya kirafiki;

Isipokuwa kwamba mtu anayeunda, kuundisha au kutayarisha chombo kwa namna mojawapo katika hizo zilizokwisha tajwa, anafanya hivyo kwa kutimiza mkataba uliofanywa kabla ya kuanza vita kama hivyo vilivyokwisha semwa , hatawajibika kwa adhabu yoyote katika adhabu

zilizotajwa katika kifungu hiki kuhusu uundaji huo au utayarishaji huo iwapo:-

- (i) kwa Rais kutoa ilani ya kuonyesha kutopendelea upande wowote katika vita, ye ye atatoa mara moja kwa Waziri anayehusika na mambo ya ndani habari za uundaji, uundishaji au utayarishaji wa chombo hicho na kupasha habari zote za mkataba na mambo yote yanayohusu kufanywa au kuwa yatafanywa chini ya mkataba huo kama zitakavyotakiwa na Waziri huyo ; na
- (ii) anatoa dhamana na kuchukua au kuruhusu kuchukuliwa hatua zozote, kama zipo, kama zitakavyoelezwa na Waziri anayehusika na mambo ya ndani ili kuhakikisha kwamba chombo hicho hakiwezi kuchukuliwa, au kusafirishwa au kuondolewa bila ya ruhusa ya Rais mpaka mwisho wa vita hivyo..

**66. (1) Mtu ye yote ambaye:-**

Uharamia  
Sheria Na. 14 ya  
1980 kif. 8

- (a) anatenda kitendo cha ukatili dhidi ya meli au chombo kilichosajiliwa Tanzania au dhidi ya watu au mali iliyo ndani ya chombo; au
- (b) akiwa ni raia wa Tanzania anatenda kitendo chochote kinyume na sheria cha kikatili dhidi ya chombo chochote; au
- (c) kwa kujitolea akashiriki kwenye shambulio la chombo au ndege kwa nia ya kutenda kitendo chochote kilichotajwa kwenye aya ya (a) au (b),  
atakuwa ametenda kosa linaloitwa “uharamia” na akipatikana na hatia atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha.

(2) Hakuna mashtaka chini ya kifungu hiki yataakayoanzishwa bila idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

**SURA YA TISA**

**MIKUSANYIKO ISIYO HALALI NA GHASIA NA MAKOSA  
MENGINE DHIDI YA UTULIVU WA UMMA**

Vimefutwa

**67-73. (Vimefutwa na Sheria ya mwaka 1954 Na. 11 Kif;33)**

Maana ya  
mkusanyiko usio  
halali na ghasia

**74.(1) Wakati ambapo watu watatu au zaidi wanakusanyika kwa nia ya kutaka kutenda  
kosa, au wakiwa wamekusanyika kwa kutimiza madhumuni fulani kwa**

pamoja, wakajiweka katika hali ambayo itawafanya watu walio jirani wawe na sababu ya kuogopa kwamba watu hao waliokusanyika watavunja amani, au kwa kukusanyika kwao kutachochea, bila ya sababu ya maana, watu wengine wavunje amani, mkusanyiko huo utakuwa mkusanyiko usio halali.

(2) Haijalishi kama mkusanyiko wa mwanzo ulikuwa halali iwapo katika kukusanyika walijiweka kwa madhumuni ya pamoja kwa namna iliyokwisha tajwa katika kifungu kidogo cha (1).

(3) Mkusanyiko usio halali unapoanza kutimiliza madhumuni ya mkusanyiko kwa njia ya kuvunja amani na vitisho kwa umma, mkusanyiko huo utaitwa ghasia na watu waliokusanyika watasemwa kuwa wamekusanyika kwa ajili ya ghasia.

Adhabu ya  
mkusanyiko usio  
halali

**75.** Mtu yejote atakayeshiriki katika mkusanyiko usio halali atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha mwaka mmoja.

Adhabu ya  
kushiriki katika  
ghasia

**76.** Mtu yejote atakayeshiriki katika ghasia anatenda kosa

Kutoa tamko kwa  
wafanya ghasia  
kutawanyika  
Sura ya 500 kif.  
7; Sura 356 kif.  
11 (13)

**77.** Hakimu yejote au, kama hayupo, afisa wa polisi wa au aliye juu ya cheo cha muauzi au akida wa jeshi la vita la Jamhuri ya Muungano, atakayeona watu kumi na mbili au zaidi wamekusanyika kwa ajili ya ghasia ana wasiwasi kuwa ghasia inataka kufanywa na watu kumi na mbili au zaidi, au anaweza kutoa au kutolesha ilani kwa jina la Rais, kwa namna atakayoona yafaa, kuwaamrisha wafanyaji ghasia hao au watu waliokusanyika watawanyike kwa amani.

Kutawanyika kwa  
wafanya ghasia  
baada ya tamko  
kutolewa  
Sheria Na. 25 ya  
2002 Jedwali.

**78.** (1) Iwapo utapita muda kuisha baada ya tamko kutolewa au baada ya tamko hilo kufanya, ikazuiwa kwa nguvu, na watu kumi na mbili au zaidi wataendelea kukusanyika pamoja kwa ghasia, mtu yejote aliyepewa mamlaka ya kutoa ilani hiyo, au afisa wa polisi yejote, au mtu mwingine yoyote kwa niaba ya afisa huyo anaweza kumsaidia ili kuwatawanya watu hao wanaoendelea kukusanyika au kuwakamata wote au mmoja wao, na mtu yoyote atakayekaidi, anaweza kutumia nguvu zote zitakazolazimu kushinda ukaidi huo, na hatakabiliwa na mashitaka yoyote ya jinai au madai kwa kudhuru au kuua mtu yejote katika kutumia nguvu hizo.

(2) Licha ya kifungu kidogo cha (1), hakuna maombi ya mapitio yanayoweza kufanya kuhusiana na utangulizi au amri ya muda au amri ya mahakama, isipokuwa kama maamuzi hayo au amri hiyo itamaliza kabisa shauri hilo

Ghasia baada ya  
tamko.

**79.** (1) Iwapo tamko limetolewa ya kuwaamrisha watu waliojihuisha katika ghasia au waliokusanyika kwa ajili ya kufanya ghasia, kutawanywa

kila mtu ambaye anashiriki au anaendelea kushiriki katika ghasia au mkusanyiko huo baada ya kuisha muda wa kufaa toka tamko litolewe kufanya ghasia au mkusanyiko atatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka mitano.

(2) Licha ya kifungu kidogo cha (1), hakuna maombi ya mapitio yanayoweza kufanyika kuhusiana na utangulizi au amri ya muda au amri ya mahakama, isipokuwa kama maamuzi hayo au amri hiyo itamaliza kabisa shauri hilo

Kuzuia au  
kupinga utoaji wa  
tamko

**80.** Mtu yejote ambaye kwa kutumia nguvu anazuia au anapotosha utoaji wa tamko kama ilivyo katika kifungu cha 77 atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi; na kama utoaji ilani utazuiwa, kila mtu ambaye ataendelea kushiriki katika ghasia hiyo au mkusanyiko huo huku akijua kwamba ilani juu ya jambo hilo imezuiwa kwa nguvu mtu huyo atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka mitano.

Wafanya ghasia  
kubomoa  
majengo n.k.

**81.** Mtu yejote ambaye amekusanyika na wengine kinyume cha sheria kwa kufanya ghasia au kubomoa au kuharibu, au kuanza kubomoa au kuharibu jengo lolote, njia ya reli yoyote, mtambo au matengenezo yoyote atakuwa anatenda kosa na kila mmoja atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha.

Wafanya ghasia  
kuharibu  
majengo n.k.

**82.** Mtu yejote ambaye amekusanyika na wengine kufanya ghasia kinyume cha sheria anaharibu kitu chochote kilivyotajwa katika kifungu cha 81 atakuwa ametenda kosa na kila mmoja atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Kuingilia kwa  
ghasia reli,  
magari n.k.

**83.** Watu watakaokusanyika kwa ghasia na bila ya kibali halali na kutumia nguvu wakazuia au kupinga upakiasi au upakuaji katika reli yoyote, gari au chombo chochote au uweki au usafirishaji wa gari; au utwekaji au kusafiri kwa bahari kwa chombo chochote bila ya uhalali na kwa nguvu wakajipakia relini, garini au chomboni kwa nia ya kufanya hayo watakuwa wametenda kosa.

Kutembea na  
silaha hadharani

**84.** Mtu yejote anayetembea na silaha katika hadhara bila ya jambo la halali linaloruhusiwa kisheria kwa namna ambayo inaweza kuleta utisho kwa mtu yejote mtu huyo anatenda kosa na silaha yake yawezza kuhodhiwa.

Kuingia kwa  
nguvu

**85.** Mtu yejote ambaye kwa ajili ya kutaka kumiliki ataiingia katika ardhi yoyote au makao yoyote kwa nguvu aidha nguvu hizo zilikuwa za mabavu zilitumika kwa mtu mwengine au ni za kutishia au kuvunja nyumba yoyote au ni kwa kukusanya idadi ya watu isiyo kawaida mtu huyo atatenda kosa liitwalo kuingia kwa nguvu na, kwa ajili ya kifungu hiki haidhuru kuwa

anaruhusiwa kuingia kwenye ardhi hiyo au la:

Isipokuwa kwamba mtu ataingia katika ardhi au makao ambayo ni mali yake lakini yamo katika ulinzi wa mtumishi wake au mlinzi wake hatakuwa ametenda kosa la kuingia kwa nguvu.

Kuzuia kwa  
nguvu

**86.** Mtu yejote ambaye atakuwa anamiliki ardhi bila ya haki yoyote na anamiliki ardhi hiyo kwa namna ambayo huenda ikaleta uvunjifu wa amani au kusababisha woga wa uvunjifu wa amani juu ya mtu mwenye haki kisheria kumiliki ardhi hiyo, mtu huyo anatenda kosa la kuzuia kwa nguvu.

Mapigano

**87.** Mtu yejote ambaye atapigana mahali pa hadhara atakuwa amekosa na atahukumiwa kifungo cha miezi sita au kutozwa faini isiyozidi shilingi mia tano.

Kuchocha  
mapigano ya  
wawili

**88.** Mtu yejote ambaye anachochea mtu mwingine kwa mapigano ya watu wawili, au kuchocha mtu mwingine afanye mapigano ya watu wawili mtu huyo atakuwa ametenda kosa.

Lugha chafu,  
mzozo, na  
kutishia kutumia  
wa nguvu.  
Sheria Na. 48 ya  
1948 kif. 2; 14 ya  
1950 kif. 9; 49 ya  
1955 kif. 7; na  
Sheria Na. 12 ya  
1962

**89.—(1)** Mtu yejote ambaye-

- (a) anatumia lugha chafu, ya matusi au ya usafihi kwa mtu mwingine yoyote kwa namna ambayo huenda ikaleta uvunjifu wa amani; au
- (b) anazozana au, kwa namna nyingine yoyote, ataleta fujo kwa namna ambayo huenda ikaleta uvunjifu wa amani, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miezi sita.

2) Mtu yejote ambaye-

- (a) kwa kusudi la kutaka kutishia au kumsumbuu mtu mwingine anatishia kuchoma nyumba au kuivunja au kuharibu nyumba yoyote; au
- (b) kwa kusudi la kumshitunga mtu yejote atafyatua bunduki au atatenda jambo lolote la kuivunja amani, atakuwa aetenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha mwaka mmoja na kama kitendo kitakuwa kimetendeka usiku mtuhumiwa atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka miwili.

Kuvinjari au  
kuzonga.  
Sheria Na. 49 ya  
1955 kif: 8; G.N.  
Na. 236 ya 1961

**89 A.—(1)** Mtu yejote anayevinjari au kuzonga nyumba yoyote au mahali popote, au anakaribia nyumba yoyote au mahali popote kwa nia ya:-

- (a) kumzuia mtu yejote mwingine asifanye tendo ambalo ni halali kisheria; au
- (b) kumlazimisha mtu yejote mwingine kufanya kitendo ambacho anaweza sheria kujizuia, atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miezi sita;

Isipokuwa kwamba masharti ya kifungu hiki hayatatumika katika

kuvinjari au kuzonga ambako ni halali kwa mujibu wa sheria zinazohusu vyama vya wafanyakazi au migogoro yao.

2) Mtu hawezu kushitakiwa kwa kosa chini ya kifungu hiki bila ya idhini ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashitaka.

Kutishia  
Sheria Na.5 ya  
1961 kif cha 4;  
G.N. Na. 236 ya  
mwaka 1961

**89B**—(1) Mtu yeote ambaye kwa dhuluma na bila ya mamlaka ya sheria anamtishia mtu yeote mwengine kwa nia ya kutaka kumlazimisha mtu huyo:-

- (a) kuacha kufanya kitendo chochote ambacho ni haki yake kukifanya; au
- (b) afanye kitendo chochote ambacho ana haki asikifanye, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha mwaka mmoja.

(2) Katika kifungu hiki -

“kutishia” maana yake ni kusababisha akili ya mtu kupata madhara au kwa mtu yeote katika ukoo wake au mtu anayemtegemea au utumiaji wa nguvu kwa mtu yeote au uharibifu wa mali;

“dhara” linajumuisha madhara kwa mtu kuhusu biashara, kazi, ajira au njia nyingine ya kupatia pesa na pia inajumuisha kitendo chochote kinachowenza kushitakiwa.

(3) Mtu hawezu kushitakiwa kwa kosa chini ya kifungu hiki bila ya idhini ya maandishi ya Mkurugenzi wa mashitaka.

Kushawishi watu  
wasisaidie  
mipango ya  
kujitolea  
Sheria Na.. 61 ya  
1962 kif cha . 2

**89C**—(1) Mtu yeote ambaye, kwa nia ya kukinza, kuzuia, au kupinga mpango wowote wa kujitolea au aina yoyote ya mpango wa kujitolea uliokubaliwa na Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya , anamshawishi au kujaribu kumshawishi mtu yeote aliyejitlea kufanya kazi zake, au kusaidia kufanya hivyo, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kwa faini isiyozidi shilingi elfu moja au kifungo cha muda usiozidi miezi sita au vyote kwa pamoja

(2) Katika mashitaka yoyote kwa kosa lililofanywa dhidi ya kifungu hiki shahada ya Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya, kama itakavyokuwa, kwamba mpango wa kujitolea uliotajwa au ulioelezwa ulikubaliwa na yeze katika tarehe iliyotajwa au kwa mipango ya kujitolea ya namna hiyo iliyelezwa ilikubaliwa na yeze katika tarehe iliyotajwa au kabla ya tarehe hiyo, basi shahada hiyo itakuwa ni ushahidi uliokamilika wa matukio hayo.

Mkusanyiko kwa  
madhumuni ya  
kufanya magendo

**90.** Watu wawili au zaidi ambao wanakusanyika pamoja kwa lengo la kuteremsha, kuchukua au kuficha bidhaa yoyote iliyolazimu kulipia ushuru

wa forodha na ipasiwayo kuhodhiwa chini ya sheria inayohusu ushuru wa forodha watakuwa watatenda kosa na kila mmoja wao atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka miwili .

---

*Sehemu ndogo ya II.—Makosa dhidi ya Usimamiaji Mamlaka ya Halali.*

---

## SURA YA KUMI

### KUTUMIA MADARAKA VIBAYA

Vimefutwa

91-93 [Vimefutwa na Sheria Na. 19 ya mwaka 1958 kifungu cha 15]

Maafisa  
wanaosimamia  
mali ya watu kwa  
kazi maalum.

**94.** Mtu yejote ambaye, ameajiriwa kwenye utumishi wa umma, na kwa ajili ya utumishi wake amepewa kazi za kimahakama au za kusimamia mali ya aina fulani, au anaendesha kiwanda chochote, biashara au kazi maalum, na akiwa amepata au anayo, moja kwa moja au si moja kwa moja, ana masilahi binafsi katika mali hiyo, kiwanda, biashara au atafanya kazi hiyo kwa ajili ya mali, kiwanda, biashara, au kazi ambayo anayo, hayo masilahi ndani yake au kwa ajili ya mwenendo wa mtu yejote anayehusika na kazi hiyo, atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha mwaka mmoja.

Madai ya uongo  
ya maofisa

**95.** Mtu yejote ambaye, ameajiriwa kwenye utumishi wa umma ambaye katika cheo chake atatakiwa au kutoa kumbukumbu au taarifa kuhusu kiasi chochote ambacho kimelipwa na kinadaiwa kuwa kimelipwa kwake au kwa mtu mwingine yejote au kuhusu jambo jingine lolote ambalo linahitaji kuthibitishwa kwa ajili ya malipo yoyote ya fedha au utoaji wa bidhaa kwa mtu yejote, atatoa kumbukumbu au taarifa kuhusu jambo lolote analolijua, la uongo kuhusu taarifa yoyote atakuwa ametenda kosa.

Kutumia vibaya  
madaraka G.N.  
Na. 236 ya 1961

**96.** (1) Mtu yejote ambaye ameajiriwa kwenye utumishi wa umma anayetenda au kuamrisha kitendwe kwa kutumia vibaya madaraka ya kazi yake, kitendo chochote cha dhuluma ambayo kitazuia haki ya mwingine atakuwa ametenda kosa.

(2) Iwapo kitendo hicho kitatendwa au kuamriwa kwa ajili ya faida, mtu atakayetiwa hatiani kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka mitatu.

(3) Uendeshaji wa mashitaka kwa kosa lolote chini ya kifungu hiki

hautaanzishwa ila kwa idhini ya Mkurugenzi wa Mashitaka.

Maafisa wa serikali kutoa shahada za uongo

**97.** Mtu yelete ambaye anaruhusiwa au anatakiwa na sheria kutoa shahada yoyote inayohusu jambo lolote ambalo, kwa msingi huo shahada ya mtu yelete inaweza kuathirika, anatoa shahada ambayo kwa uelewa wake ni ya uwongo katika jambo la msingi atakuwa anatenda kosa.

Matumizi yasiyoruhusiwa ya viapo vya nje ya makakama

**98.** Mtu yelete anayetoea kiapo au anayetoea tamko la dhati, au uthibitisho au kiapo, kuhusu jambo lolote ambalo kwa sheria hana mamlaka yoyote ya kulifanya anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha mwaka mmoja:

Isipokuwa kwamba kifungu hiki hakitatumika kwa kiapo au tamko, uthibitisho, au utoaji wa hati ya kiapo unaofanywa mbele ya hakimu, korona au mlinzi wa amani katika jambo lolote linalohusiana na utunzaji wa amani au adhabu ya makosa au lihusikalo na uchunguzi juu ya vifo vya ghafla, si kwa ajili ya kiapo, tamko, uthibitisho au utoaji wa hati ya kiapo au kwa ajili ya madhumuni mengine ni halali chini ya sheria za nchi nyngine, au kwa ajili ya kuthibitisha uhalali wa hati ambayo inakusudiwa kutumiwa katika nchi nyngine.

Matumizi ya uongo ya mamlaka Sura ya 11 Jedwali

**99.** Mtu yelete ambaye-

(a) si afisa wa kimahakama, anajipa mamlaka ya kutenda kama afisa wa makakama;

(b) bila ya mamlaka akajifanya ni mtu mwenye mamlaka na sheria kulisha kiapo au anafanya uthibitisho wa aina yoyote au kufanya kitendo kingine chochote kihusikacho na watu ambacho kinaweza tu kufanya na watu walioruhusiwa na sheria kufanya hivyo;

(c) anajitokeza kuwa ni mtu aliyeruhusiwa kisheria kutia saini hati inayothibitisha yaliyomo kwenye daftari yoyote au kumbukumbu iliyowekwa na mamlaka ya halali, au inayothibitisha kweli yoyote au tukio, na kutia saini hati hiyo kama kwamba ameruhusiwa kufanya hivyo, ambapo haruhusiwi, na anajua kwamba, haruhusiwi kufanya hivyo, atakuwa anatenda kosa.

**100.** Mtu yelete ambaye-

(a) anajifanya kuwa ndiye mtu aliye katika utumishi wa umma katika wakati ambao anataka kufanya tendo lolote au kuhudhuria mahali popote kwa sababu ya kazi yake; au

(b) anajiwakilisha kwa uwongo kuwa ni mtu aliye katika utumishi wa umma, na anajitia kufanya kitu chochote au kuhudhuria mahali popote kwa madhumuni ya kufanya kitendo chochote kwa mujibu wa kazi hiyo,

atakuwa ametenda kosa.

**101.** Yeyote ambaye atatoa kitisho chochote cha kumjeruhi mtu yelete

Kujifanya mtumishi wa umma

Kutishia kuwajeruhi

watumishi wa wa umma aliye katika utumishi wa umma, au kutoa kitisho hicho kwa mtu yeote ambaye anaamini kwamba anahuksika naye, kwa madhumuni ya kumshawishi mtu huyo kufanya kitendo chochote au kuvumilia au kuchelewesha kufanya kitendo chochote kinachohusika katika kutekeleza kazi za umma za mtu huyo, atakuwa ametend kosa.

### SURA YA KUMI NA MOJA MAKOSA YANAYOHUSU USIMAMIAJI WA HAKI

Ushahidi wa uwongo na kushawishi kusema uwongo Sheria Na. 55 ya mwaka 1963 Jedwali la 6

**102.**-(1) Mtu yeote ambaye, katika kesi yeote, au kwa ajili ya kaunzisha kesi yeote, kwa kujuu akitoa ushahidi wa uwongo kuhusu jambo lolote ambalo ni muhimu kwa hoja yeote inayotegemea kesi hiyo au inayokusudiwa kutolewa katika kesi hiyo, atakuwa ametenda kosa la kusema uwongo na itakuwa sio muhimu:-

- (a) kama ikiwa ushahidi umetolewa kwa kiapo au la;
- (b) kuwa mtu anayetoa ushahidi na akalazimika kuongea ukweli ikijiidhinisha kwenye fomu na sherehe ambazo zinazotumika kusimamia kiapo au kwa namna nyingine vinambana yeye;
- (c) kama ushahidi wa uwongo umetolewa kwa mdomo au kwa maandishi;
- (d) kama mahakama au baraza limekamilika kama inavyotakiwa au lipo mahali panapotakiwa au sivyo, iwapo inafanya kama mahakama au baraza katika kesi ambazo zinatolewa ushahidi huo;
- (e) kama mtu huyo anayetoa ushahidi huo ni shahidi anayefaa au sivyo, au kwamba ushahidi huo unakubalika katika kesi hiyo au sivyo.

(2) Mtu yeote ambaye atasaidia, atashiriki, atashauri, atatuma, au atashawishi mtu mwingine kutoa ushahidi wa uwongo, atakuwa ametenda kosa la kushawishi ushahidi wa uwongo.

**103.** Mtu yeote ambaye, ameapishwa kama mkalimani katika kesi, kwa makusudi akatoa maelezo muhimu katika kesi hiyo huku akijua kuwa ni ya uwongo, au ambayo haamini kuwa ni ya kweli, atakuwa ametenda kosa la ushahidi wa uwongo.

Maelezo ya uwongo ya wakalimani

Adhabu kwa ushahidi wa uwongo

**104.** Mtu yeote anayetenda kosa la kutoa ushahidi wa uwongo au kushawishi ushahidi wa uwongo atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Ushahidi juu ya shitaka la kutoa ushahidi wa uwongo

**105.** Mahakama haitamhukumu mtu aliye shahiwishi ushahidi wa uwongo ushahidi wa mtu mmoja kuhusu uwongo wa habari yoyote inayodaiwa kuwa ni ya uwongo.

Kutunga ushahidi

**106.** Mtu yeote ambaye, kwa kusudi la kudanganya baraza lolote katika kesi yoyote-

- (a) anatunga ushahidi wa uwongo kwa njia yeote nyingine

- isiyokuwa na ushahidi wa uwongo au ya kushawishi ushahidi  
wa uwongo; au
- (b) kwa kujuia anatumia ushahidi huo wa kutunga,  
Atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka  
saba.
- 107.** Mtu yeyote anayeapa uwongo au kufanya uthibitisho au kutamka  
tamko mbele ya mtu yeyote anayeruhusiwa kutoa kiapo juu ya jambo  
lolote lihusulo watu katika hali ambayo kiapo cha uwongo au matamshi ya  
uwongo, kama kikitendwa katika kesi kingelikuwa ni sawa na kutoa  
ushahidi wa uwongo, atakuwa ametenda kosa.
- 108.** Mtu yeyote anayefanya hadaa, udanganyifu, au kwa makusudi  
anatoa au anadhihirisha maelezo yoyote, ishara au maandishi ya uwongo,  
kwa mtu yeyote anayeitwa au atakayeitwa kuwa shahidi katika kesi  
yejote, kwa kusudi la kutoa na kuthibitisha ushahidi wa ushahidi wa mtu  
huyo, atakuwa ametenda kosa.
- 109.** Mtu yeyote ambaye, kwa kujuia kwamba kitabu chochote, nyaraka  
au kitu cha namna yoyote kinaweza kuhitajika kwenye ushahidi katika  
kesi, kwa makusidi akakiondoa au kukiharibu au kukifanya kisisomeke au  
kisitambulike kwenye ushahidi, atakuwa ametenda kosa.
- 110.** Mtu yeyote ambaye-
- (a) anakula njama na mtu mwingine yeyote kumsingizia mtu  
yejote kwa kosa lolote la jinai au kufanya jambo lolote ili  
kuzuia, kukingga, kukaidi au kupotosha njia ya haki; au
  - (b) kwa kusudi la kuzuia njia halisi ya haki, anamshawishi,  
anamzuia au anamkataza mtu yeyote anayeruhusiwa kihalali  
kuhudhuria mahakama na kutoa ushahidi akiwa ni shahidi,  
kwa kuhudhuria na kutoa ushahidi huo, au kujaribu kufanya  
hivyo,
- atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka  
mitano.
- 111.** Mtu yeyote ambaye anaomba, anapokea, au anakubali au anajaribu  
kupokea au kupata mali yoyote kwa kujinufaisha yeye mwenyewe au mtu  
mwingine yeyote kutokana na mapatano yoyote au kwa kufahamu kwamba  
ataffilisha au kuficha kosa, au ataepuka au kukomesha, au kuchelewesha  
shitaka la kosa au ushahidi mwingine uliopo, atakuwa ametenda kosa.
- 112.** Mtu yeyote ambaye, ameletwa au anajisingizia kuleta shitaka, dhidi  
ya mtu mwingine lihusikalo na shitaka la jinai ambalo lipo chini ya sheria  
yojote kwa ajili ya adhabu kwa kosa ambalo limetendwa au limesemwa  
kuwa alimetendwa na yeye, likaleta shitaka hilo bila ya amri au idhini ya  
mahakama ambayo shitaka hilo analipeleka au atalipeleka, atakuwa  
ametenda kosa

**113. Mtu yeyote ambaye-**

- (a) anatangaza kutoa zawadi kwa kurejesha mali yoyote ambayo imeibiwa au imepotea, na katika kutoa zawadi hiyo ametumia maneno ikionyesha kwamba hakuna maswali yatakayouliwa, au huyo mtu anayetoa mali hiyo hatakamatwa au kudhuriwa; au
- (b) anatangaza hadharani kumrejesha mtu yeyote ambaye atanunua au ametanguliza malipo ya fedha kwa njia ya kukopa kwa ajili ya mali yoyote iliyoibwa au kupotea, mali hiyo iliyolipwa au kutanguliwa au kiasi kingine chochote cha fedha au zawadi kwa ajili ya kurejeshwa kwa mali, au
- (c) anachapisha au anatangaza ahadi kama hiyo, kama ilivyotajwa katika aya ya (a) au (b),  
atakuwa ametenda kosa.

**114.-(1) Mtu yeyote ambaye:-**

- (a) ndani ya eneo au mpaka wa eneo ambalo kesi yeyote inafanyika au kutaka kufanyika, anaonyesha ukosefu wa nidhamu kwa matamshi au tabia, kwenye kesi yoyote, ndani ya jingo au mahali jirani ya jengo hilo ambamo kesi hiyo inasikilizwa au inafanyika, au mbele ya mtu yeyote ambaye anaisikiliza kesi hiyo;
- (b) baada ya kuitwa kutoa ushahidi katika kesi akakosa kuhudhuria au, amehudhuria lakini akakataa kuapishwa au kuthibitishwa, au baada ya kuapishwa au kuthibitishwa, akakataa bila ya kutoa sababu zozote za halali kujibu swalii au kutoa nyaraka zozote au kitu chochote, au kubaki chumbani ambamo kesi hiyo inasikilizwa , baada ya mashahidi kuamriwa kutoka chumbani; au
- (c) analeta pingamizi au fujo wakati kesi inasikilizwa;
- (d) wakati kesi hiyo ikiahirishwa, atatangaza au kuchapisha au kutumia matamshi au maandishi ambayo yatakuwa ya uongo kuhusu kesi hiyo, au kuweza kumleta mtu yeyote kwa ajili ya kumtetea yeye au dhidi ya wahusika wengine kwenye kesi, au yanayokusudiwa kupunguza mamlaka ya mtu yeyote ambaye kesi hiyo inasikilizwa mbele yake;
- (e) atatangaza habari za ushahidi uliochukuliwa kwenye kesi yoyote iliyoamriwa iendeshwe faraghani;
- (f) anajaribu kumuqingilia au kumshawishi shahidi katika kesi ya aidha kabla au baada ya kutoa ushahidi huo uhusikao na kesi;
- (g) anamfukuza mtumishi kwa sababu ametoa ushahidi kwa niaba ya wahusika katika kesi;
- (h) anachukua kimakosa ardhi au mali nyingine kutoka kwa mtu mwininge ambaye punde tu mahakama imemmilikisha ardhi hiyo au mali;
- (i) kwa makosa anammiliki wa mtoto kutoka kwa mtu mwininge

yejote ambaye amepata umiliki wa kumtunza mtoto kwa amri ya mahakama;

- (j) ana namna ya kulipa fidia au gharama au kiasi kingine chochote kwenye kesi za madai au kesi za jinai inazotolewa dhidi yake na mahakama ya mwanzo, kwa kusudi anakataa au kudharau baada ya kupewa notisi ya kumtaka alipe kuhusiana na amri ya malipo mengine yoyote aidha au la kwa awamu; au
  - (k) ametenda kitendo kingine chochote cha kutoheshimu kazi za mahakama au kwa mtu mwingine yejote ambaye kesi imesikilizwa au kuchukuliwa,
- (l) ametenda kosa la kudharau taratibu za mahakama atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miezi sita na faini ambayo haitazidi shilingi elfu tano.

(2) Wakati ambapo kosa lolote litatendeka kinyume aya za (a), (b), (c), (d), au (k) za kifungu kidogo cha (1) limefanyika machoni mwa mahakama, mahakama inaweza ikamuweka mkosaji kizuizini, na wakati wowote kabla ya mahakama haijaanza siku hiyo, kumhukumu mkosaji kulipa faini ya shilingi elfu nne au akishindwa kulipa, atafungwa mwezi moja.

(3) Masharti ya kifungu hiki yatahesabiwa kuwa ni ziada, na si kwamba ni uwezo wa Mahakama Kuu kutoa adhabu kwa kosa la kudharau mahakama.

(4) Aya ya (b) ya kifungu kidogo cha (1) kinaanza kutumika kuhusiana na muendelezo wa kesi kwenye mahakama ya Wilaya ambapo ushahidi haujatolewa kwa kiapo au kuthibitishwa kama vile marejesho kwa mtu anayehusika au anayethibitishwa yanajumuisha marejesho kwa mtu ambaye alihitajika na mahakama kutoa ushahidi kuhusiana na muendelezo wa kesi.

Kuzuia au  
kukinga  
uwasilishaji au  
utekelezaji wa  
hati Sheria Na. 5  
ya 1961 kif. 6

#### **114A. Mtu yejote ambaye-**

- (a) kwa makusudi anakinga au kwa kujua anazuia au kwa njia yoyote anaingilia au anapinga, uwasilishaji uliopelekwa kwa kuitwa shaurini yeye mwenyewe au mtu mwingine yejote, kwa notisi, amri, hati ya kukamata au hati nyingineyo ambayo imetolewa na mahakama iliyotolewa kwake yeye mwenyewe au kwa mtu mwingine, kama itakavyokuwa;
- (b) kwa makusudi anakinga, au kwa kujua anazuia, au kwa kuingilia au kuzuia utekelezaji wa hati yoyote ya kuitwa shaurini, notisi, amri, hati ya kukamatia au hati nyinginezo ambazo zinatolewa na mahakama kwake mwenyewe au kwa mtu mwingine yejote aliyeruhusiwa kihalali katika utekelezaji wa kazi hiyo; au
- (c) anatoroka ili kuepuka kupewa amri yoyote ya kuitwa shaurini, amri, notisi au hati ya kukamatia au hati nyingineyo ambayo imetolewa na mahakama,

atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha muda

usiozidi mwaka mmoja.

**SURA YA KUMI NA MBILI**  
**KUOKOA, KUTOROKA NA KUWAKINGA WATUMISHI WA MAHAKAMA**

Kuokoa      **115.-**(1) Mtu yeyote ambaye atamtoa kwa nguvu au atajaribu kumtoa mtu yeyote kwenye ulinzi wa halali-

- (a) iwapo mtu huyo mwingine amehukumumiwa kifo au kifungo cha maisha, au ameshitakiwa kwa kosa linalostahili adhabu ya kifo au kifungo cha maisha, atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha;
  - (b) iwapo mtu huyo mwingine amefungwa gerezani kwa shitaka au amehukumiwa kwa kosa lingine mbali na yale yaliyotajwa kwenye aya ya (a), atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba;
  - (c) katika kesi nyingine yoyote, atakuwa ametenda kosa
- (2) Iwapo mtu aliyeokolewa yumo katika uangalizi wa mtu binafsi, mkosaji lazima apashwe habari ya ukweli huo kwamba mtu aliyetolewa yumo katika ulinzi huo.

Kutoroka  
kwenye  
kifungo halali  
**116.** Mtu yeyote ambaye, anatoroka kutoka kwenye kifungo halali, atakuwa ametenda kosa.

Kutokuhudhuri  
kazi za kifungo  
cha nje  
**116A.-**(1) Iwapo mtu yeyote ambaye ameruhisiwa kufanya kazi nje ya gereza, kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Magereza, anakosa kuhudhuria katika saa iliyowekwa, au kutokuwepo kwenye kazi yake, atakuwa ametenda kosa mpaka pale atakapoitosheleza mahakama kwamba alikuwa na sababu za msingi na udhuru halali wa kutokuhudhuria huko.

(2) Adhabu ya kifungo ambayo inatolewa kwa kosa dhidi ya kifungu kidogo cha (1) itakuwa ni nyongeza ya adhabu ya kifungo chochote ambacho mtu huyo alishahukumiwa na kile ambacho atapaswa kukitumikia chini ya Sheria ya Magereza.

Kusaidia  
wafungwa  
kutoroka  
**117.** Mtu ambaye-

- (a) anamsaidia mfungwa kutoroka au kujaribu kutoroka kwenye kifungo halali; au
- (b) anapeleka kitu chochote au kufanya kitu chochote kupelekwa ndani ya gereza kwa kusudi la kumwezesha mfungwa kutoroka, atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Uondoshaji n.k  
wa mali yoyote  
iliyokamatwa  
kihalali  
**118.** Mtu yeyote ambaye, mali yoyote itakuwa imewekwa au imechukuliwa kwa utaratibu wa mamlaka ya mahakama yoyote, kwa kujua, na kwa kusudi la kuzuia au kupinga tanzi au utaratibu, amepokea ameiondoa, amezuia, ameficha au ameuza mali hiyo, atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa

adhabu ya kifungo cha miaka mitatu.

Kimefutwa

**119.** [Kimefutwa na Sheria Na. 5 ya mwaka 1961 kif. 7.]

**SURA YA KUMI NA TATU**  
**MAKOSA MADOGOMADOGO DHIDI YA MAMLAKA YA UMMA**

Udanganyifu  
na uvunjaji  
uaminifu kwa  
watumishi wa  
umma.  
Sheria Na. 2 ya  
mwaka 1972  
Jedwali.

Kuupuza  
wajibu wa  
kikazi

Kutoa taarifa za  
uwongo kwa  
watumishi wa  
umma

Kutokutii  
wajibu wa  
kisheria

Kutokutii amri  
za halali

**120.** Mtu yejote aliyeajiriwa katika utumishi wa ummai ambaye katika kufanya wajibu wa kazi zake, atatenda kosa la udanganyifu wowote au uvunjaji uaminifu ambao utadhuru umma, iwe udanganyifu huo au uvunjaji uaminifu huo ungekuwa ni jinai au sivyo kama ungetendwa dhidi ya mtu binafsi, atatenda kosa na atawajibika kifungo cha miaka saba.

**121.** Mtu aliyeajiriwa katika utumishi wa umma ambaye, kwa makusudi anapuuza wajibu wake ambao inamlazimu kutimiza kwa mujibu wa sheria za jumuiya ya madola au sheria yoyote, isipokuwa kama ufanyakaji wa wajibu wakeI atakuwa katika hatari kuliko yule mtu hodari wa kawaida na kitendo kinaweza kudhaniwa kukubaliwa, atakuwa ametenda kosa.

**122.** Mtu yejote ambaye anatoa taarifa yoyote kwa mtumishi wa umma kwa kujua au kwa kuamini kwamba taarifa hiyo ni ya uwongo, kwa kusudi la kumfanya mtumishi huyo, au kwa kuamini kwamba inaweza kumfanya mtumishi huyo -

- (a) kufanya au kutokufanya jambo lolote ambalo linampasa alifanye au asilifanye kama angejua hali ya ukweli wa taarifa inayotolewa; au
- (b) kutumia uwezo halali wa mtumishi huyo ili kumdharaau au kumuudhi mtu yejote,

atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miezi sita au faini ya shilingi elfu moja au vyote kwa pamoja.

**123.** Mtu ambaye, kwa makusudi, anavunja sheria yoyote kwa kutenda kitendo chochote ambacho kinatakazwa na sheria au kwa kuacha kutenda kitendo chochote ambacho kinatakiwa kufanya ambacho kinahusisha umma au sehemu yoyote ya umma, atakuwa ametenda kosa na atawajibika, isipokuwa ikionekana kama adhabu tofauti inatolewa na sheria hiyo au nyingine kwa kutokutii, atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka miwili.

**124.** Mtu ambaye hatii amri yoyote, hati, au amri inayowekwa ipasavyo, kutolewa au inayotokana na mahakama, mtumishi wa umma au mtu aliyeruhusiwa kufanya kazi ya umma kwa niaba yake, anatenda kosa na, isipokuwa kama adhabu nyingine yoyote itatolewa au sheria nyingine yejote itatoa adhabu ya kutokutii atahukumiwa kifungo cha miaka miwili.

Kimefutwa

**124A.** [Kimefutwa na Sheria Na. 15 ya mwaka 1971 kif. 9.]

*Kigawo cha Tatu – Makosa yanayodhuru umma kwa ujumla*

**SURA YA KUMI NA NNE**  
**MAKOSA YANAYOHUSIANA NA DINI NA MAZISHI**

Fedheha  
kwenye dini

**125.** Mtu yejote ambaye atavunja, kuharibu na kuchafua mahali popote pa kuabudia au kitu chochote kinachoitwa kitakatifu na watu wa aina yejote kwa madhumuni ya kufedhehesha dini ya kundi lolote la watu au kwa kufahamu kuwa kundi lolote la watu linataka kufanya uharibifu, hasara au uchafuzi kama fedheha kwa dini atakuwa ametenda kosa.

Kufanya fujo  
kwenye  
mkusanyiko ya  
dini.

**126.** Mtu yejote ambaye kwa hiari yake ataleta fujo kwenye mkusanyiko wowote ambaa umekusanyika kihalali kufanya ibada au sherehe za dini ametenda kosa.

Kuingia  
kwenye  
mazishi au  
sehemu  
nyingine bila  
idhini.

**127.** Mtu yejote ambaye, kwa madhumuni ya kuumiza imani za mtu yejote au kufedhesha dini ya mtu yejote, au kwa kufahamu kuwa imani ya mtu yejote inaweza kuumizwa, au dini ya mtu mwingine iko hatarini kufedhehesawa, ametenda kosa la kuingia kwenye eneo la kuabudia bila ruhusa eneo la makaburi matakatifu au kwenye eneo lolote ambalo limetengwa kwa ajili ya mazishi au kama bohari ya mabaki ya maiti, au atafanya dhuluma yejote kwa maiti ya binadamu au atafanya fujo kwa watu wowote waliokusanyika kwa ajili ya mazishi, atakuwa ametenda kosa.

Kuzuia mwili  
wa mtu  
aliyekufa  
kuzikwa.  
Sheria Na. 5 ya  
mwaka 1963  
kif. 2

**128.** Mtu yejote ambaye bila halali anazuia mazishi ya mwili wa mtu yejote aliyekufa au mtu ambaye, bila mamlaka halali kwa niaba hiyo au vinginevyo kulingana na kanuni iliyowekwa na Waziri anayehusika na afya (ambayo unamuongoza Waziri aliyepewa mamlaka kufanya) anafukua kaburi, anapasua, au anafanya uharibifu wowote kwenye mwili wa mtu yejote aliyekufa au ambaye, anawajibika kufanya maiti ya mtu yejote izikwe, kwa hiari yake na bila kupewa idhini na mamlaka halali anapuuza kutimiza wajibu wake kwa makusudi , atakuwa ametenda kosa.

Kutamka  
maneno kwa  
nia ya kuudhi  
imani ya dini.

**129.** Mtu yejote ambaye kwa dhamira ya kuudhi imani ya mtu yejote ya dini yake akatamka maneno yejote au akafanya sauti yejote itakayosikiwa na mtu huyo au akafanya ishara mbele ya macho ya mtu huyo atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha mwaka moja.

**SURA YA KUMI NA TANO**  
**MAKOSA DHIDI YA UTU**

Tafsiri ya  
mwanamke.

**129A.** Katika Sura hii “mwanamke” maana yaje ni mtu yejote wa jinsia ya kike na, isipokuwa kama muktadha utataka vinginevyo bila kujali umri.

**130.-**(1) Ni kosa kwa mtu wa jinsia ya kiume kumbaka msichana au mwanamke.

(2) Mtu wa jinsia ya kiume atakuwa ametenda kosa la kubaka kama atakuwa amefanya tendo la ndoa na msichana au mwanamke chini ya mazingira ambayo yanadondokea kwenye maelezo yafutayo:

- (a) ambaye si mke wake, au awe mke wake ambaye ametengana nae bila ridhaa yake wakati wa tendo la ndoa;
- (b) kwa ridhaa yake, pale ambapo ridha yake imepatikana kwa kutumia nguvu, vitisho, au kwa kumuogopesha au kumtishia kumuua au kumuumiza au akiwa amezuiliwa isivyo halali;
- (c) kwa ridhaa yake pale ambapo ridhaa yake imepatikana wakati ambaao alikutwa hana akili timamu au akiwa amelewa kwa kushawishiwa na madawa ya kulevyo, kitu au vitu ambavyo amepewa na mtu au watu wengine isipokuwa ikithibitika kuwa kulikuwa na ridhaa mwanzoni kati yao wawili;
- (d) kwa ridhaa yake pale ambapo mwanamume alijua kuwa yeye si mume wake, na kuwa ridhaa ilitolewa kwa sababu alifanywa kuamini kuwa yeye ni mwanamume mwingine, ambaye yeye mwenyewe, anaamini kuwa ameolewa nae kihalali;
- (e) kwa ridhaa au bila ya ridhaa akiwa chini ya umri wa miaka kumi na nane, isipokuwa kama mwanamke ni mke wake ambaye ana umri wa miaka kumi na tano au zaidi na hajatengana na mumewe.

(3) Mtu yeyote-

- (a) akiwa mtu wa mamlaka, kuchukulia kigezo cha nafasi yake ya mamlaka, na anatenda kosa la kubaka kwa msichana au mwanamke wa mahusiano ya kiofisi au kwa kukosea anamzuia na kumbaka msichana au mwanamke;
  - (b) akiwa kwenye uongozi au kuwa mionganini mwa wafanyakazi wa mahabusu au sehemu nyingine yeyote ya uangalizi, iliyoundwa kisheria au kwa taasisi ya wanawake au watoto kwa kuchukulia kigezo cha nafasi yake na kutenda kosa la kubaka msichana yeyote au mwanamke mfanyakazi mwenzie wa magereza, sehemu ya matunzo au taasisi.
  - (c) akiwa kwenye uongozi au mfanyakazi wa hospitali, kuchukulia kigezo cha nafasi yake na kutenda kosa la kubaka msichana au mwanamke;
  - (d) akiwa mganga wa kienyeji kuchukulia kigezo cha nafasi yake na anatenda kosa la kubaka msichana au mwanamke ambaye ni mteja wake kwa nia ya kupata uponyaji;
  - (e) akiwa kiongozi wa dini kuchukulia kigezo cha nafasi yake na kutenda kosa la kubaka msichana au mwanamke.
- (4) Kwa madhumuni ya kuthibitisha kosa la kubaka-
- (a) mpenyo japokuwa ni mdogo unatosha kuthibitisha tendo la ndoa muhimu katika kosa; na

- (b) ushahidi wa kukataa kama vile majeraha yanayoonekana kwenye mwili sio muhimu kuthibitisha kuwa tendo la ndoa lilitendeka bila ridhaa.
- (5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki wanandoa watachukuliwa kuwa wametengana hata kama kutengena kwao kumepangwa na familia au ndugu wa ukoo.

Adhabu ya kubaka.  
Sheria Na. 4 ya mwaka 1998  
kif. 6

**131.-**(1) Mtu yejote atakayetenda kosa la kubaka, isipokuwa kwenye kesi ambazo zimeelezewa kwenye kifungu kidogo cha (2) kilichobadilishwa, atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha, na kwa kila kesi ambayo kifungo chake hakipungui miaka thelathini pamoja na adhabu ya viboko na faini, na atatakiwa kulipa fidia ya kiasi ambacho kitatamkwa na mahakama, kwa mtu ambaye ametendewa kosa hilo na kwa majeraha aliyoypata.

(2) Bila ya kuathiri vifungu vya sheria yejote, pale ambapo kosa limetendeka na mvulana wa umri wa miaka kumi na nane au pungufu, atatakiwa—

- (a) kama mkosaji kwa mara ya kwanza, atahukumiwa adhabu ya viboko tu;
- (b) kama mkosaji kwa mara ya pili, atahukumiwa kifungo cha kipindi cha miezi kumi na mbili na adhabu ya viboko;
- (c) kama ni mkosaji kwa mara ya tatu na ni mkosaji mhalifu, atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1).

(3) Bila ya kujali masharti yaliyopita ya kifungu hiki mtu yejote atakayetenda kosa la kubaka msichana wa chini ya umri wa miaka kumi atawajibika kwa kwa adhabu ya kifungo cha maisha.

Sheria Na.19  
ya mwaka  
2007, kif. 8

**131A. -** (1) Pale ambapo kosa la kubaka limetendwa na mtu mmoja au zaidi , katika kikundi cha watu, kila mmoja katika kikundi hicho atafanya au kusaidia kufanya kosa atachukuliwa kuwa ametenda kosa la kubaka kwa kikundi.

(2) Kila mtu ambaye ana hatia ya kubaka kwa kikundi, atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha, bila kujali alitenda gani alishiriki katika kubaka.

Kujaribu kubaka  
Sheria Na. 4 ya  
1998 kifungu cha.  
8

**132.-**(1) Mtu yejote ambaye atajaribu kubaka anatenda kosa la jaribio la kubaka, na isipokuwa kwa maelezo yaliyopo kwenye kifungu kidogo cha (3), akipatikana na hatia atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha, na wakati mwengine atawajibika kwa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka thelathini pamoja na au bila adhabu ya viboko.

(2) Mtu anajaribu kubaka iwapo, kwa nia ya kufanya ngono isiyo halali na msichana yejote au mwanamke, na akadhihirisha nia yake kwa-

- (a) kumtishia msichana huyo au mwanamke kwa nia ya ngono;
- (b) akiwa ni mtu mwenye madaraka au ushawishi kwa msichana au mwanamke huyo, kutenda kitendo chochote cha kumtishia

- kwa ajili ya ngono;
- (c) anafanya udanganyifu kwa nia ya kupata idhini yake;
  - (d) anajifanya kuwa yeye ni mume wa msichana au mwanamke huyo, na msichana ama mwanamke huyo anawekwa kwenye hali ambayo, bila ya idhini yake anaweza akaingiliwa kimwili
- (3) Pale mtu anapotenda kosa la kujaribu kubaka kwa kuonyesha nia yake kama ilivyoainishwa kwenye aya ya (c) au (d), atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha na wakati mwingine kifungo kisichopungua miaka kumi.

Kutorosha

**133.** Mtu yejote ambaye kwa nia ya kumuoa au kufanya ngono na mwanamke wa umri wowoe au kumfanya aolewe au kufanya ngono na mtu mwingine yejote, anamchukua mwanamke huyo au kumzuia bila ya ridhaa yake, atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa kifungo cha miaka saba.

Kutorosha  
mwanamke wa  
umri wa chini ya  
miaka kumi na  
sita

**134.** Mtu yejote ambaye kinyume cha sheria anamchukua mwanamke ambaye hajaolewa wa umri chini ya miaka kumi na sita kutoka katika ulinzi au uangalizi wa wazazi wake au mtu mwingine mwenye uangalizi wa halali na madaraka juu ya msichana huyo na akamchukua bila ya ridhaa ya wazazi wake au ya huyo mtu mwingine atakuwa ametenda kosa.

Kujamiihana na  
shambulio la aibu  
kwa mwanawake  
Sheria Na. 47 ya  
1954 kif. 3;  
Sheria Na. 4 ya  
1998 kif.. 9

**135.-**(1) Mtu yejote ambaye kwa makusudi ya kusababisha shambulio la kijinsia la aibu kwa kutoa maneno au sauti, kuonyesha vitendo au kutoa maneno, au kuonyesha ishara yoyote ambayo itaonekana na mtu mwingine atakuwa ametenda kosa la shambulio la kijinsia na akipatikana na hatia atawajibika na kifungo kisichozidi miaka mitano au faini isiyozidi laki tatu au vyote viwili, kifungo na faini.

(2) Endapo kosa la shambulio la kijinsia chini ya kifungu hiki litamhusu mvulana au msichana wa umri wa chini ya miaka kumi na nane, haitakuwa kinga kumshitaki mvulana au msichana huyo aliridhia kitendo kilichosababisha shambulio la kijinsia.

Kimefutwa

**136.** [Kimefutwa na Sheria Na. 4 ya mwaka 1998 Kif. 10.]

Kunajisi majuha  
au punguani

**137.** Mtu yejote ambaye, akijua kwamba mwanamke ni juha au punguani na akajaribu kufanya naye ngono kinyume katika mazingira ambayo si ya kubaka, lakini kwa kudhihirika kuwa mtu huyo wakati wa kutenda kosa hilo alijua kuwa mwanamke huyo alikuwa juha au punguani, atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne, pamoja na , au bila adhabu ya viboko.

Mume kumnajisi  
mkewe aliye chini  
ya umri wa miaka  
kumi na tano n.k  
Sheria. Na. 4 ya  
1954; Sheria Na..  
4 ya 1998 kif. 11

**138.-**(1) Mtu yejote ambaye ameoa msichana aliye na umri wa chini ya miaka kumi na tano, na akafanya naye ngono au akajaribu kufanya naye ngono kwa ridhaa au bila ridhaa ya msichana huyo, kabla hajafikisha umri wa miaka kumi na tano atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi.

- (2) Mtu yejote ambaye ni mzazi au mlezi wa msichana aliye na umri wa chini ya miaka kumi na tano akimwachia msichana huyo au akamruhusu kwa nia kwamba msichana huyo akiwa na umri wa chini ya miaka kumi na tano aingiliwe kimwili na mume wake kwa idhini au bila idhini ya msichana huyo, au kwa ridhaa yake, lakini bado yuko chini ya miaka kumi na tano atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi.
- (3) Mtu yejote ambaye anachukua au anajaribu kumchukuwa msichana aliyeolewa chini ya miaka kumi na tano kwa lengo la kufanya ngono na mume wake, kwa ridhaa yake au bila ridhaa ya msichana huyo, akiwa chini ya miaka kumi na tano atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi.
- (4) Haitakuwa kinga kwa mtu anayeshtakiwa chini ya kifungu kidogo cha (3) kwamba mtu aliyemchukua mwanamke huyo ni mume wake.
- (5) Kutakuwa na kinga kushtakiwa chini ya kifungu hiki-
- (a) iwapo mwanamke aliyetendewa kosa hilo ataonekana na mahakama kuwa amefikia umri wa miaka kumi na tano; au
- (b) iwapo mahakama itaona kwamba mtu aliyeshtakiwa alikuwa na kila sababu za kumfanya aamini na aliamini kwamba msichana huyo alikuwa na umri wa zaidi ya miaka kumi na tano,

- (6) Hakuna kitu katika kifungu hiki kitakachokuwa ni kosa kwa mwaafrika au muasia atakayeoa au atakayeruhusu ndoa ya msichana aliye chini ya umri wa miaka kumi na tano kufuatana na desturi za kabilia au dini iwapo haikukusudiwa kuwa ndoa hiyo itafanyika kwa msichana kufanya tendo la ndoa na mumewe huyo kufanya ngono na mume huyo kabla ya kufikia umri wa miaka kumi na tano au kumfanya kuwa amekosa kwa kutoa au kupokea zawadi kwa ajili ya ndoa hiyo au wakati wa sherehe za ndoa hiyo.

Vitendo nya  
shambulio kubwa  
la aibu kati ya  
watu  
Sheria Na. 4 ya  
1998 kif. 12

**138A.** Mtu yejote ambaye atatenda hadharani au kwa kificho au atakayefanya jambo au kuwa mshirika au kushirikiana na mtu yejote kufanya shambulio la aibu, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kwa adhabu ya kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitano au faini isiyopungua shillini laki moja na isiyozidi laki tatu; ila endapo kosa limetendwa na mtu mwenye umri wa miaka kumi na nane au zaidi dhidi ya mtu yejote mwenye umri wa chini ya miaka kumi na nane, mwanafunzi wa shule ya msingi au mwanafunzi wa shule ya sekondari mhalifu atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka isiyopungua kumi , pamoja na adhabu ya viboko, na pia ataamriwa kulipa fidia ya kiasi cha fedha kitakachoamuliwa na mahakama kwa yule aliyetendewa kosa hilo kwa ajili ya madhara yaliyosababishwa na mtu huyo.

Kuwatumia  
watoto kwa ngono  
Sheria Na. 4 ya  
1998 kif. 12

- 138B.-(1)** Mtu yejote ambaye-
- (a) akiwa anafahamu anamruhusu mtoto yejote kuwa kwenye sehemu yoyote kwa nia ya kumsababisha mtoto kudhalilishwa kijinsia au kushiriki kwa namna yoyote katika matendo ya ngono au maonyesho ya ngono;
  - (b) anajifanya kuwa ni kuwadi wa mtoto kwa nia ya kufanya ngono au namna yoyote ya udhalilishaji kwa ngono, au maonyesho ya ngono;
  - (c) anamlaghai mtu kuwa yeye ni mteja wa mtoto kwa nia ya ngono au aina yejote ya udhalilishaji wa kijinsia, au maonyesho ya ngono, kwa njia ya matangazo au kwa kutumia vyombo vya habari, matangazo kwa njia ya mdomo au namna nyingine zinazofanana na hizo;
  - (d) anatumia vibaya uwezo wake au mahusiano yake aliyonayo kwa mtoto, akamlaghai mtoto kufanya matendo ya ngono au namna yoyote ya udhalilishaji wa kijinsia au maonyesho ya

kudhalilisha ya ngono;

- (e) anamtishia, au akitumia nguvu kwa mtoto, kwa nia ya kumlazimisha mtoto kufanya ngono au kwa namna yoyote ya kumdhalilisha mtoto kwa ngono au maonyesho ya ngono;
- (f) anampa mtoto au wazazi wake fedha, vitu au mafao mengine kwa nia ya kumkuwadia mtoto huyo afanye ngono au namna yoyote ya udhalilishaji wa ngono au maonyesho ya ngono,

Atatenda kosa la kumtumia mtoto kwenye matendo ya ngono na atawajibika kwa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka mitano jela na kisichozidi miaka ishirini.

Matumizi Mabaya  
ya Ngono  
Sheria Na. 4 ya  
1998 kif. 12

**138C.-**(1) Mtu yeyote ambaye kwa nia ya kujitosheleza haja yake ya ngono, anafanya jambo lolote kwa kutumia sehemu zake za siri au sehemu yoyote ya mwili wa binadamu au kifaa chochote au tundu lolote au sehemu yoyote ya mtu mwingine, iwe ni kitendo kisichopelikea kubaka chini ya kifungu cha 130, atakuwa ametenda kosa la udhalilishaji kwa ngono endapo atakuwa ameyatenda hayo kwa mazingira yanayoangukia chini ya maelezo yafuatayo, kwa kusema kwamba-

- (a) bila ya ridhaa ya mtu huyo mwingine;
- (b) kwa ridhaa ya mtu mwingine ikiwa ridhaa hiyo imepatikana kwa kushurutishwa, vitisho au kumuweka mtu huyo kwenye uoga wa kuuwawa au kuumizwa ikiwa mtu huyo alikuwa amefungiwa kunyume cha sheria;
- (c) kwa ridhaa ya mtu mwingine ikiwa ridhaa hiyo imepatikana wakati mtu huyo mwingine alikuwa ana matatizo ya akili au alikuwa amelewa pombe au madawa au kitu chochote

(2) Mtu yeyote ambaye-

- (a) anatenda kosa kubwa la kudhalilisha la kijinsia akipatikana na hatia atawajibika kwa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka kumi na tano na kisichozidi miaka thelathini, pamoja na adhabu ya viboko, na pia atatakiwa kulipa fidia ya kiasi kitakachoamriwa na mahakama kwa mtu yeyote ambaye kosa lililotendeka na kwa maumivu aliyyasababisha mtu huyo;
- (b) anatenda kosa kubwa la udhalilishaji wa kijinsia kwa mtu aliye chini ya umri wa miaka kumi na tano;

akipatikana na hatia awajibika kwa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka ishirini na kisichozidi miaka thelathini , na pia ataamriwa kulipa fidia ya kiasi kitakachoamuliwa na mahakama kwa mtu yejote aliyetendewa kosa hilo na maumivu alirosababishiwa mtu huyo.

Shambulio la  
Aibu .  
Sheria Na. 4 ya  
1998 kif. 12

**138D.-**(1) Mtu yejote ambaye kwa kukusudia anamshambulia au anatumia nguvu kutenda kosa la kijinai anamdhalilisha mtu mwingine kwa makusudi au kwa kutumia kosa la jinai au kumdhalilisha mtu huyo kimapenzi, kwa kutumia maneno au vitendo atakuwa ametenda kosa la kudhalilisha kwa mapenzi na akipatikana na hatia awajibika kwa adhabu ya kifungo kisichozidi miaka mitano jela au faini isiyozidi Shilingi laki mbili au vyote kwa pamoja, na anaweza pia akaamriwa kulipa fidia ya kiasi kitakachoamriwa na mahakama kwa mtu aliyetendewa kosa hilo na kwa madhara au maumivu alirosababishiwa mtu huyo.

(2) Mtu yejote, mwenye nia ya kumdhalilisha mwanamke na kutoa neno lolote, kwa kutumia sauti yoyote au ishara, au kuonyesha kitu chochote ikiwemo kiungo chochote cha kike au cha kiume, kwa nia kwamba maneno hayo au sauti hiyo isikike, au ishara au kifaa hicho kionekane na mwanamke au kuingilia faragha ya mwanamke, atakuwa ametenda kosa la udhalilishaji wa kijinsia.

(3) Ili kuondoa mashaka, matendo ya ngono yatakayosababishwa kwa maneno au matendo na mtu aliye na madaraka katika sehemu ya kazi au sehemu nyingine yoyote, atakuwa ametenda kosa la udhalilishaji wa kijinsia.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki udhalilishaji unaweza kujumuisha vitendo vyovoyote ambavyo chini ya kifungu cha 130 havimaanishi ubakaji .

(5) Hakuna shtaka kwa kosa chini ya kifungu hiki litaanzishwa au kuendelea ikiwa lalamiko hilo litafanywa na mlalamikaji wakati wowote baada ya siku sitini tangu kutokea tukio liliosababisha kosa.

Uwakala wa  
ukahaba.  
Sheria ya No: 47  
ya 1954 kif. 3; 49  
ya 1955 kif. 9;  
Na. 4 ya 1998;  
kif: 13

**139.-**(1) Mtu yejote ambaye-

(a) analeta au anajaribu kuleta mtu yejote, ikiwa ni mwanamke au mwanaume wa umri wowote, kwa idhini au bila ya idhini yake kuwa kahaba, ndani ya Jamhuri ya Muungano au nje ya Jamhuri ya Muungano;

- (b) anamsababisha, au anajaribu kusababisha mtu yejote mwenye umri chini ya miaka kumi na nane, kuondoka katika Jamhuri ya Muungano, au bila ya ridhaa ikiwa ni kwa au bila ya idhini ya mtu huyo, au bila ya idhini kwa nia ya kumsaidia ajihusishe na ngono zisizo halali na mtu yejote nje ya Jamhuri ya Muungano, au akimuondoa au kujaribu kumuondoa kutoka katika Jamhuri ya Muungano, mtu huyo, kwa ridhaa yake au bila ridhaa yake kwa nia hiyo;
- (c) anasababisha, au kujaribu kusababisha, mtu yejote wa umri wowote, kuondoka katika Jamhuri ya Muungano, kwa ridhaa au bila ridhaa yake, kwa nia ya kwamba mtu huyo atakuwa anaishi au anakwenda kwenye danguro, mahali popote au atamuondoa au kujaribu kumuondoa mtu huyo kutoka katika Jamhuri ya Muungano, kwa ridhaa au bila ridhaa yake kwa nia hiyo;
- (d) anamleta, au anajaribu kumleta katika Jamhuri ya Muungano mtu yejote mwenye umri wa chini ya miaka kumi na nane kwa nia ya kumshirikisha kwenye ngono haramu na mtu yejote hapa ndani au nje ya Jamhuri ya Muungano;
- (e) anasababisha, au anajaribu kusababisha mtu yejote wa umri wowote, kwa ridhaa au bila ridhaa ya mtu huyo, kuondoka kwenye maskani yake anayoishi katika Jamhuri ya Muungano ambayo si danguro, kwa nia ya kumhusisha mtu huyo na ukahaba, kuishi au kuhudhuria mara kwa mara kwenye danguro, ndani au nje ya Jamhuri ya Muungano;;
- (f) anamfungia mtu yejote bila ridhaa ya mtu huyo kwenye danguro lolote au sehemu yoyote kwa nia ya kufanya ngono haramu au udhalilishaji wa ngono kwa mtu huyo,

atakuwa ametenda kosa la ukuwadi na akipatikana na hatia atawajibika kwa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka kumi na kisichozidi miaka ishirini au faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyoziding shillingi laki tatu, au vyote kwa pamoja.

**139A.-(1) Mtu yejote ambaye-**

- (a) anajihuisha na kitendo cha kununua, kuuza or kumbadilisha mtu yejote kwa fedha au kwa makuballiano mengine;
- (b) kwa nia ya kusaidia, kuwezesha au kushawishi ununuzi au uuzaji au ubadilishaji au uwekaji wa mtu yejote kwa ajili ya

kulipwa fedha au kwa malipo mengine-

- (i) anapanga, au anasaidia, mtoto kusafiri ndani au nje ya Jamhuri ya Muungano bila ridhaa ya wazazi wake au walezi wake; au
- (ii) anachukua hati ya kiapo kutoka kwa mwanamke mjamzito kwa makubaliano ya fedha au kitu kingine, kwa ajili ya kumchukua mtoto huyo ambaye hajazaliwa baada ya kuzaliwa; kutoka kwa mwanamke huyo; au
- (iii) anamwajiri mwanamke au mtu na mkewe kwa ajili ya kuzaa watoto; au
- (iv) ikiwa ni mtu anayehusika na uandikishaji wa vizazi, kwa kufahamu, anaruhusu kusaidia taarifia yoyote ya kuzaliwa; au
- (v) anajihuisha na anachukua watoto kutoka kwenye mahospitali, hifadhi za wanawake, kliniki, shule za awali, vituo vya chekechea au kwenye taasisi yoyote ya watoto au vituo vya ustawi wa jamii kwa kutumia fedha au makubaliano mengine au kumchukua mtoto kwa kumuasilii kutoka kwenye taasisi hizo au vituo, kwa kumtishia mama wa mtoto au mtu mwengine yejote; au
- (vi) anajifanya mama au anasaidia mtu mwengine kujifanya mama wa mtoto huyo,

atakuwa ametenda kosa la kusafirisha watu kwa magendo na akipatikana na hatia atawajibika kwa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka ishirini na kisichozi miaka thelathini na faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi laki tatu au vyote kwa pamoja na kwa nyongeza ataamriwa kulipa fidia kwa kiasi kitakachoamriwa na mahakama, kwa yule mtu aliyotendewa kosa hilo.

(2) Katika kifungu hiki “mtoto” maana yake ni mtu yejote mwenye umri wa chini ya miaka kumi na nane.

Uwakala wa  
Ubakaji  
Sheria Na. 49 ya  
1955 s. 7; Sheria  
Na. 4 ya 1998  
kif.. 15; 9 ya 2002  
Jedwali

**140. Mtu yejote ambaye-**

- (a) kwa vitisho au kutishia anamsababisha au anajaribu kumsababisha msichana yejote au mwanamke yejote kujihuisha na ngono haramu ndani au nje ya Tanzania, au
- (b) kwa kujisingizia au kwa kusema uongo anamsababisha , msichana yejote au mwanamke kufanya ngono haramu popote

nchini au nje ya Jamhuri ya Muungano ; au

- (c) anatumia, anasimamia, anasababisha, kuchukuliwa na msichana au mwanamke madawa ya kulevya au kitu chochote kwa nia ya kumpoteza fahamu au kupungukiwa nguvu ili mtu yejote aweze kumfanyia vitendo vya ngono haramu msichana au mwanamke huyo;

atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua shillingi laki moja na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichopungua miaka kumi jela na kisichozidi miaka ishirini jela au vyote kwa pamoja na ataamriwa kulipa kiasi kitakachoamriwa na mahakama.

Mwenye nyumba  
n.k. kuruhusu  
kunajisiwa kwa  
msichana wa  
chini ya miaka  
kumi na tano  
kwenye nyumba  
yake

**141.** Mtu yejote ambaye akiwa ni mwenye nyumba au mkazi wa nyumba anaangalia au anafanya au kusaidia kuangalia au kutunza nyumba hiyo, atamshawishi au anajua msichana wa umri wa chini ya miaka kumi na tano kuja mara kwa mara au kuwepo hapo nyumbani kwa madhumuni ya kujihusisha na ngono na mwanaume yejote ikiwa ngono hiyo ilikusudiwa kufanywa na mwanaume yejote, atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya miaka mitano :

Isipokuwa kwamba itakuwa ni utetezi wa kutosha chini ya shitaka chini ya kifungu hiki iwapo itabainishwa mbele ya mahakama kwamba alikuwa na sababu ya kutosha kumsababisha aamini na anaamini kwamba msichana huyo alikuwa na umri unaozidi miaka kumi na mbili.

Mwenye nyumba  
kuruhusu  
kunajisiwa  
msichana wa umri  
chini ya miaka  
kumi na sita  
kwenye nyumba  
yake

**142.** Mtu yejote ambaye, akiwa ni mwenye nyumba au mkazi wa nyumba hiyo au anaangalia au anafanya au kusaidia kuangalia au kuitunza nyumba hiyo, akimshawishi au kwa kuja msichana wa umri wa juu ya miaka kumi na tano na chini ya miaka kumi na sita kuja mara kwa mara au kuwepo hapo nyumbani kwa madhumuni ya kujihusisha na ngono na mwanaume kinyume cha sheria, iwapo ngono hiyo imekusudiwa na mwanaume fulani au mwanaume yejote, atakuwa ametenda kosa

Isipokuwa kwamba itakuwa ni utetezi wa kutosha kwa shtaka lolote chini ya kifungu hiki iwapo itabainishwa mbele ya mahakama iliyopelekewa shtaka hilo kwamba mtu huyo aliyeshtakiwa alikuwa na sababu ya kutosha iliyomsababisha aamini na aliamini kwamba msichana huyo alikuwa na umri wa zaidi ya miaka kumi na sita

Kuzuia katika jengo lolote au katika danguro kwa nia fulani

**143.-**(1) Mtu yejote ambaye atamzuia mwanamke bila ridhaa yake-

(a) katika au kwenye jengo lolote kwa makusudi ya kutaka afanyiwe vitendo vya ngono kinyume cha sheria na mwanaume yejote, iwe mwanaumume fulani au yejote; au

(b) katika danguro lolote,

ametenda kosa

(2) Wakati ambapo mwanamke atakuwa kwenye jengo lolote kwa nia ya kutenda ngono kinyume cha sheria au yuko kwenye danguro lolote, mtu atachukuliwa kuwa amemfungia hapo endapo, kwa dhamira ya kumlazimisha au kumshawishi kubakia kwenye eneo la jengo hilo au kwenye danguro hilo, mtu huyo akimvua nguo au kitu kingine alichonacho au endapo nguo hizo zimeazimwa au amepewa kwa maelekezo ya mtu huyo, na mtu huyo akamtishia kumchukulia hatua za kisheria endapo ataondoka na nguo hizo alizoazimwa au kupewa.

(3) Hakuna hatua za kisheria, za madai au jinai, zitakazochukuliwa dhidi ya mwanamke aliyetajwa na kifungu hiki kwa kuchukua au kupatikana akiwa na nguo au mavazi ambayo yalikuwa muhimu kumwezesha kuondoka kwenye jengo au danguro hilo.

Uwezo wa  
Kupekuu.  
Sheria Na. 55 ya  
1963 Jedwali la  
sita

**144.-**(1) Iwapo hakimu ataona baada ya kupata taarifa iliyotolewa kwake kwa kiapo na mzazi, ndugu au mlezi wa mwanamke au mtu mwingine yejote ambaye, kwa maoni ya hakimu, ana nia njema kwenye maslahi ya mwanamke au mtu kuwa kuna sababu za msingi za kuhisi kuwa mwanamke huyo amezuiwa kinyume cha utu wa kibinadamu ndani ya eneo la mamlaka ya hakimu huyo, hakimu huyo anaweza akatoa hati ya kuruhusu mtu huyo aliyetajwa kutafutwa, na kama akipatikana, kumchukua na kumfungia kwenye sehemu salama mpaka atakapofikishwa mbele ya hakimu huyo; na hakimu ambaye mwanamke huyo atafikishwa kwake anaweza akafikishwa kwa wazazi au walezi wake, au vinginevyo akashughulikia swala hilo kulingana na hali inavyohitaji au kuruhusu.

(2) Hakimu anayetoea hati, kwa hati hiyo au hati nyingine, inayosababisha mtu yejote anayetuhumiwa kwa kumfungia isivyo halali mwanamke, kukamatwa na kupelekwa mbele ya hakimu na taratibu za kumuadhibu mtu huyo kwa mujibu wa sheria zichukuliwe.

(3) Mwanamke anachukuliwa kuwa anafungiwa kinyume cha nia njema kama mwanamke huyo atashikiliwa kwa nia ya kufanya ngono kinyume cha sheria na mwanaume maaalum au mwanaume yejote; na:-

(a) ikiwa ana umri wa chini ya miaka kumi na sita;

(b) iwapo ana umri wa zaidi ya miaka kumi na sita na chini ya

miaka kumi na nane, akifungiwa bila ridhaa yake au kinyume na matakwa ya yejote kati ya wazazi wake au mtu yejote mwenye mamlaka kisheria ya kumuangalia au kumuongoza; au

(c) iwapo atakuwa na umri wa zaidi ya miaka kumi na nane na akafungiwa bila ridhaa yake.

(4) Mtu yejote aliyeruhusiwa kwa hati chini ya kifungu hiki kumtafuta mwanamke huyo aliyefungiwa anaweza kuingia (kama ikibidi kwa nguvu) nyumba yoyote, jengo au sehemu yoyote iliyotajwa kwenye hati hiyo, na anaweza kumtoa kutoka kwenye nyumba, jengo au sehemu hiyo.

Mwanamume  
kuishi kwa pato la  
la ukahaba au  
ukowadi

**145.-**(1) Mwanaume ambaye-

- - (a) kwa kufahamu anaishi kwa kutegemea kipato au sehemu ya kipato chake anakipata kutokana na biashara ya ukahaba; au
  - (b) kwenye sehemu yoyote ya umma anashawishi au kutongoza kwa nia ya uasherati,

ametenda kosa na endapo ni kosa la pili au zaidi, au kwa kupatikana na hatia zinazofuatana chini ya kifungu hiki mahakama inaweza kwa nyongeza ya adhabu itakazotoa akamhukumu mtuhumiwa adhabu ya viboko.

(2) Pale ambapo mwanamume anadhihirika kuishi au kuwa na mahusiano na kahaba, au ikidhihirika kuwa anamuamuru, anatoa maelekezo au ana ushawishi juu ya mienendo ya kahaba kwa namna inayoonyesha kuwa anasaidia, anashawishi au anamlazimisha mwanamke huyo kufanya ukahaba na mtu mwagine yejote, asipoiridhisha mahakama vinginevyo, attachukuliwa kuwa anajua anaishi kwa kutegemea kipato kutokana na ukahaba.

Mwanamke  
anayeishi  
kutokana na , au  
kwa kusaidia.

**146A.** Mwanamke ambaye akiwa anafahamu anaishi akiwa akitegemea kipato chake au sehemu ya kipato chake kutokana na ukahaba, kwa ajili ya kuishi, ana mamlaka, au anashawishi juu ya mwenendo wa kahaba kwa namna hiyo ili kuonyesha kuwa anasaidia, anashawishi au kumlazimisha mwanamke huyo kufanya ukahaba na mtu yejote, anatenda kosa.

Uwezo wa  
kupekua

**147.** Iwapo hakimu atajulishwa kwa taarifa itakayotolewa kwa kiapo kuwa kuna sababu za kuhisi kuwa nyumba yoyote, au sehemu ya nyumba

inatumika na mwanamke kwa kufanya ukahaba, au na mtu yeyote anayeishi au anayetembelea nyumba hiyo anajulikana kuwa anaishi kwa kutegemea kipato chake chote au sehemu ya kipato chake kwa ukahaba, au ana mamlaka, anaelekeza au kushawishi juu ya mwenendo wa kahaba, hakimu anaweza akatoa hati kuidhinisha polisi yeyote kuingia na kupekua na kumkamata mtu huyo.

Kumiliki danguro **148.** Mtu yeyote ambaye ametenga nyumba, chumba, vyumba au sehemu yoyote kwa nia ya ukahaba, atanenda kosa

Njama ya  
kushawishi  
kujamiihana  
kusiko halali  
Sheria . Na. 47 ya  
1954 kif . 3

**149.** Mtu yeyote akishirikiana na mtu mwingine kumshawishi mwanamke yeyote, kwa udanganyifu au kwa njia za kulaghai anamruhusu mwanaume kufanya ngono isivyo halali na mwanamke huyo atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka mitatu..

Kujaribu kutoa  
mimba

**150.** Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya mwanamke, kuharibu mimba iwe mwanamke huyo ana mtoto au hana, kinyume cha sheria akamlisha au akamfanya ale sumu au kitu kingine cha kudhuru au akatumia nguvu ya namna yoyote au akatumia njia nyingine yoyote au namna nyingine, mtu huyo atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne .

Kusababisha  
kuharibika  
mimba

**151.** Mwanamke akiwa na mtoto, ambaye ana nia ya kutaka kutoa mimba kinyume cha sheria akala sumu au kitu kingine cha kudhuru au akatumia nguvu ya namna yoyote au akatumia njia nyingine iwayo au akaruhusu kutumiwa kwa kitu kama hicho au kufanyiwa kama hivyo, mwananamke huyo atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Kutoa dawa au  
vifaa vya kutoa  
mimba

**152.** Mtu yeyote ambaye anatoa au anampa mtu yeyote kitu chochote, akijua kwamba kinakusudiwa kutumika kinyume cha sheria kumfanya mwanamke aharibu mimba, iwe mwanamke huyo ana mtoto au hana, mtu huyo atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka mitatu .

Ufahamu kuhusu  
umri wa  
mwanamke si  
muhimu

**153.** Isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo, kosa lolote litakalotendwa kwa mwanamke au msichana chini ya umri uliotajwa halitatiliwa maanani kama mshtakiwa alikuwa hajui kuwa mwanamke huyo alikuwa chini ya umri huo au kuwa aliamini kwamba hakuwa chini ya umri huo.

Makosa ya  
kinyume cha  
maumbile  
Sheria Na. 47 ya  
1954 kif. 3; Na. 4  
ya 1998 kif. 16

**154.-(1) Mtu yeyote ambaye-**

- (a) anamuingilia mtu yeyote kinyume cha maumbile au,
- (b) anamuingilia mnyama kimwili au
- (c) anamruhusu mwanaume kumuingilia yeze mwanaume au  
mwanimke kinyume cha maumbile,

atakuwa ametenda kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha  
na wakati mwengine kifungo kisichopungua miaka thelathini .

(2) Ikiwa kosa limetendwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha  
kifungu hiki dhidi ya mtoto wa chini ya miaka kumi, mkosaji atawajibika  
kwa adhabu ya kifungo cha maisha.

Kujaribu kujamiiiana  
kinyume cha  
maumbile  
Sheria Na. 47 ya  
1954 kif. 3; Sheria  
Na. 4 ya 1998 kif;  
17

Shambulio la aibu  
kwa wavulana wa  
chini ya miaka  
kumi na nne  
Sheria Na. 10 ya  
1959 kif. 3; Na. 4  
ya 1998 kif. 18

Matendo ya aibu  
baina ya  
wanaume  
Sheria Na. 47 ya  
1954 kif. 3

Mwanaume  
kujamiiiana na  
maharimu  
Sheria Na. 4 ya  
1998 kif. 19

**155** Mtu yeyote ambaye atajaribu kutenda kosa mojawapo katika makosa  
yalijotajwa katika kifungu cha 154 atakuwa ametenda kosa na akipatikana  
na hatia atawajibika kwa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka ishirini .

**156.-(1)** Mtu yeyote ambaye atamfanya shambulio la aibu kinyume cha  
sheria kijana wa umri wa chini ya miaka kumi na nne, anatenda kosa na  
kustahili adhabu ya kifungo cha maisha jela.

(2) Iwapo shitaka la shambulio la aibu chini ya kifungu hiki  
linahusu mtoto wa kiume wa chini ya miaka kumi na nne, haitakuwa ni  
utetezi kwa shtaka hilo kuonyesha kwamba alikubali kitendo hicho cha  
aibu.

**157** Mwanamume yeyote ambaye, iwe hadharani au katika faragha  
anatenda kitendo chochote cha aibu pamoja na mwanaume mwengine au  
anamfanya mwanaume mwengine kufanya kitendo hicho na yeze au  
anajaribu kufanya kitendo hicho na mwanaume yeze mwenyewe au  
mwanaume mwengine, iwe hadharani au katika faragha, mwanaume huyo  
atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka  
mitano.

**158.-(1)** Mwanaume yeyote ambaye amekatazwa kufanya ngono na  
mwanamke yeyote ambaye anamjua kuwa ni mjukuu wake, binti yake, dada  
yake au mama yake, mwanaume huyo atakuwa amekosa na akipatikana na  
hatia atastahili adhabu-

- (a) iwapo mwanamke wa na umri wa chini ya miaka kumi na nane, mwanamume huyo atahukumiwa kifungo kisichopungua miaka thelathini;
- (b) iwapo mwanamke wa umri wa miaka kumi na nane au zaidi, mwanamume huyo atahukumiwa kifungo kisichopungua miaka ishirini;
- (2) Haitakuwa ni utetezi kwamba kitendo cha ngono kilifanywa kwa ridhaa ya mwanamke huyo.
- (3) Mwanaume atakayejaribu kutenda kosa chini ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa.

Amri ya ulezi

**159.** Mtu yejote akipatikana na hatia chini ya kifungu cha 158 katika mahakama yoyote dhidi ya mwanamke wa chini ya miaka ishirini na moja, mahakama inaweza kubadilisha ulezi yake dhidi ya mwanamke huyo, na ikiwa mkosaji ni mlezi wa mwanamke huyo, mahakama itamuondoa kwenye ulezi huo, na kwenye hali kama hiyo mahakama inaweza ikamteua mtu au watu kuwa mlezi au walezi wa mwanamke huyo wakati akiwa hajafikia utu uzima.

Isipokuwa kwamba, Mahakama Kuu wakati wowote inaweza ikabertilisha au ikasitisha amri ya uteuzi wa ulezi na kumteua mtu mwingine yejote kuwa mlezi au namna nyingine yoyote.

Wanawake  
kujamiihana na  
maharimu.  
Sheria Na. 4  
ya1998 kif. 20

**160.** Mwanamke yejote mwenye umri wa zaidi ya miaka kumi na nane ambaye anaridhia na anamruhusu babu yake, baba yake, kaka yake au mtoto wake wa kiume kujamiihana naye (akijua kwamba huyo ni babu, baba, kaka au mtoto wake kama itakavyokuwa) atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha au kifungo kisichopungua miaka thelathini na pia anaweza kuamriwa kulipa fidia ya kiasi kitakachoamriwa na mahakama kwa yule aliyetendewa kosa hilo:

Isipokuwa kwamba iwapo mwanaume ni wa umri wa chini ya miaka kumi, kifungo kisichopungua miaka thelathini .

Adhabu ya  
Makosa ya Ngon  
Sheria Na. 9, Sura  
ya 101 ya 2002  
Jedwali

**160A.** Pale ambapo mtu yejote anahukumiwa kwa kosa lolote la kujamiina lililoainishwa chini ya Sura ya XV ya Sheria hii, kama ilivyorekebishwa na Sheria dhidi ya Makosa ya Kujamiihana, mahakama itamhukumu mtu huyo kifungo kama kilivyoainishwa na Sura hiyo.

Kipimo cha undugu

**161.** Katika kifungu cha 158 na 160 maneno “kaka” na “dada” yanajumuisha kaka wa baba mmoja au mama mmoja tu na dada wa baba mmoja au mama mmja, na masharti ya vifungu hivyo yaliyotajwa yatatumika iwe ndugu ambaye ametenda kosa na mtendaji wa kosa hawatambuliki au haujulikani kwa ndoa halali.

Idhini ya  
Mkurugenzi wa  
Mashtaka G.N.  
Na. 236 ya 1961

**162.** Hakuna mashitaka chini ya vifungu vya 158 na 160 ya Sheria hii yataanzishwa bila idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

### SURA YA KUMI NA SITA MAKOSA YANAYOHUSINA NA NDOA NA WAJIBU WA MAMBO YA NYUMBANI

Ndoa ya hadaa

**163.** Mtu yeoyote ambaye kwa makusudi na kwa kulaghai anamfanya mwanamke yeoyote ambaye hakuolewa kihalali na yeeye aamini kwamba ameolewa naye kihalali na akakaa naye kinyumba au akamwingilia mwanamke huyo huku akiamini kuwa ni mume wake amekosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi .

Kimefutwa

**164.** [Kimefutwa na Sheria Na. 5 ya mwaka 1971 kif. 166(2).]

Sherehe ya ndoa  
iliyofanyika  
kihadaa bila ya  
ndoa halali

**165.** Mtu yeoyote ambaye bila uaminifu au kwa nia ya kuhadaa anafanya sherehe ya ndoa huku akijua kwamba ndoa hiyo si ya halali, mtu huyo atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka mitano.

Kutelekeza  
watoto

**166.** Mtu yeoyote ambaye, ni mzazi au mlezi au mtu mwengine mwenye uangalizi au utunzaji halali wa mtoto yeoyote mwenye umri usiozidi miaka kumi na nne, hali ana uwezo, wa kumuhudumia mtoto, kwa kuamua au kinyume cha sheria, au bila ya sababu za msingi atakataa kumhudumia, na akamtelekeza mtoto bila msaada, atakuwa ametenda kosa.

Kupuuza kutoa  
chakula n.k kwa  
watoto

**167.** Mtu yeoyote ambaye, ni mzazi au mlezi au mtu mwengine mwenye uangalizi au utunzaji halali wa mtoto yeoyote mwenye umri usiozidi miaka kumi na nne na asiyehiweza, akakataa au kupuuza (hali ya kuwa anaweza kufanya) kumpa chakula cha kutosha, nguo, malazi na mahitaji mengine ya lazima kwa maisha ya mtoto kiasi cha kumdhuru kiafya mtoto huyo,

atakuwa ametenda kosa.

Tajiri kutompatia  
mtumishi wake au  
mwanagenzi  
wake mahitaji

Kuiba mtoto

**168.** Mtu yejote ambaye ameruhusiwa kisheria, akiwa ni mwajiri mwanaume au mwanamke, kumpa mkurufunzi yejote au mtumishi wake chakula, nguo au malazi yaliyolazimu, akakataa kwa makusudi kumpa vitu hivyo, au kinyume cha sheria na kwa nia mbaya akamfanya mkurufunzi huyo au mtumishi apate madhara yoyote ya mwilini kiasi cha kuhatarisha maisha yake au kiasi cha kuwa afya yake imedhurikia au huenda ikadhirika daima mtu huyo atakuwa ametenda kosa

**169.-**(1) Mtu yejote ambaye, kwa nia ya kumyang'anya mzazi yejote, mlezi au mtu mwingine mwenye uangalizi au utunzaji halali wa mtoto aliye chini ya miaka kumi na nne, kutoka mikononi mwake-

- (a) anamchukua, au anamrubuni au anamzuia mtoto huyo kwa nguvu; au
- (b) anampokea au anamficha mtoto huyo hali akijua kwamba mtoto huyo amechukuliwa kwa nguvu au kurubuniwa au kuzuiwa,

atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

- (2) Itakuwa ni utetezi chini ya kifungu hiki, kudhihirisha kwamba mtuhumiwa anayedai kwa nia njema ana haki ya kuwa na mtoto huyo au iwapo mtoto huyo alizaliwa nnje ya ndoa, akidai kuwa yeje ni mama wa mtoto huyo au anadai kuwa ni baba wa mtoto huyo.

Ukatili kwa  
Watoto  
Sheria Na. 4 ya  
1998 kif. 21; 10  
ya 2001 Jedwali.

**169A.-**(1) Mtu yejote ambaye, ni muangalizi, anawajibu au usimamizi wa mtu yejote mwenye umri wa chini ya miaka kumi na nane akimtesa au akimtelekeza mtu huyo au akisababisha tohara kwa mwanamke au akimtahiri au kusababisha tohara hiyo ifanyike au kusababisha mtu huyo adhalilishwe, ateswe, au atelekezwe kwa namna ambayo itamsababishia maumivu au madhara kwa afya yake, pamoja na maumivu au kuharibu uwezo wake wa kuona, kusikia au kiungo chochote cha mwili au akili, atakuwa ametenda kosa la ukatili kwa mtoto.

- (2) Mtu yejote ambaye atapatikana na kwa kutenda kosa la ukatili kwa mtoto atawajibika kwa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka mitano na kisichozidi miaka kumi na tano au faini isiyozidi laki tatu au vyote kwa pamoja, na kuamriwa kulipa fidia ya kiasi kitakachoamuliwa na mahakama kwa yule aliyetendewa kosa hilo kwa mauvu aliyoسابيشا mtu huyo.

**SURA YA KUMI NA SABA  
ADHA NA MAKOSA DHIDI YA AFYA NA HALI INAYOFAA**

Adha za kawaida

**170.-**(1) Mtu yeyote ambaye atatenda kitendo kisichoruhusiwa na sheria au kuacha kutenda wajibu wake wa sheria na kwa kufanya hivyo akasababisha madhara ya kawaida au hatari au usumbufu, au akakinga au kusababisha taabu kwa umma katika kutumia haki zao za kawaida, mtu huyo atakuwa ametenda kosa la “adha za kawaida” na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha mwaka mmoja.

(2) Itakuwa si swala la msingi kwamba kutenda au kutotenda kulikolalamikiwa kumepelekeea usumbufu kwa idadi kubwa ya watu wale wasiopata usumbufu, lakini ule ukweli kwamba kutenda au kutotenda huko kulisaidia baadhi ya watu kupigania haki zao watu hao wanaweza kuonyesha kwamba si adha kwa umma .

Nyumba za  
Kamari

**171.-**(1) Mtu yeyote mwenye nyumba au ni mkazi au anatumia nyumba yoyote, chumba au sehemu yoyote, ambaye anafungua, anaweka au anatumia mahali hapo kwa madhumuni ya kuchezesha kamari isivyo halali na mtu yeyote mwenye nyumba au mkazi wa nyumba yoyote, chumba au mahali popote ambaye anajua na ataruhusu mahali hapo kufunguliwa, kuwekwa au kutumiwa kwa madhumuni ya kamari, mtu huyo yeyote kwa madhumuni, na mtu huyo mwingine ambaye anaangalia au anatunza au kwa namna nyingine yeyote anasaidia kufanya biashara kwenye nyumba yeyote, chumba au mahali pa wazi, palipowekwa aya kutumika kwa madhumuni hayo atakuwa ameweka nyumba ya kamari ya kawaida.

(2) Katika kifungu hiki “kamari isiyo halali” maana yake ni mchezo wowote wa kubahatisha ambao bahati ya kupata ni kidogo kwa wachezaji wowote kujumuisha mweka fedha au mtu mwingine au watu ambao wanasmamia mchezo au dhidi ya wachezaji wengine, wanacheza au kuweka dau.

(3) Mtu yeyote ambaye atakuwa nyumba ya kuchenza kamari atakuwa ametenda kosa

(4) Mtu yeyote ambaye hajatajwa katika watu walioitajwa katika kifungu kidogo cha (1) ambaye ataonekana katika nyumba ya kuchenza kamari, atachukuliwa kuwa amekuwemo humo kwa madhumuni ya kuchenza kamari hadi itakapodhahirika vinginevyo, atakuwa ametenda kosa na atawajibika kulipa

faini ya shilingi mia moja kwa kosa la kwanza, na kwa makosa mengine yatakayofuata faini ya shilingi mia nne au kifungo cha miezi mitatu au vyote, kifungo na faini.

Katazo la mpango  
wa piramidi.  
Sheria No. 8 ya  
2006

**171A-(1)** Mtu ambaye anaongoza au anasimamia mpango wa piramidi atakuwa ametenda kosa

- (2) “mpango wa piramidi” maana yake ni mpango au hila ambapo mtu:
  - (a) anamuahidi mtu mwingine au watu iwapo-
    - (i) malipo ya kiasi maalum cha fedha;
    - (ii) kutoa kiasi fulani cha dhamana yenye thamani; au
  - (iii) kumtaka mtu mwingine au watu wengine kulipa kiasi maalum cha fedha au kutoa kiasi fulani cha dhamana yenye thamani,

mtu huyo atastahili kupokea kiasi cha fedha au kiasi cha dhamana yenye thamani ambayo, kwa kuzingatia malipo ya kibashara, ni kubwa kuliko fedha au dhamana yenye thamani iliyotolewa au iliyorudishwa kwenye uwekezaji wa fedha au dhamana hizo za thamani zilizotolewa;

- (b) kufanya malipo yoyote kwa manufaa ya kuendeleza au kwa waendelezaji, au kwa faida ya washiriki kwenye mpango huo
- (3) Mtu atakayepatikana na hatia ya kukiuka kifungu (1), atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichozidi miaka mitano .
- (4) Kifungu hiki kitatumika kwenye aina yoyote ya mpango ambapo-
  - (a) matazamio ya washiriki kwenye mpango unaopokea malipo au manufaa mengine kati ya haya yafuatayo-
    - (i) kuanzishwa na mtu yeyote au mtu mwingine ambaye anakuwa mshiriki kwenye mpango;
    - (ii) mwendelezo wa ushiriki kwa washiriki kwenye mpango;
    - (iii) kuendeleza, kuhamisha au mabadiliko mengine ya hali ya washiriki kwenye mpango;
    - (iv) usambazaji wa mali au huduma na mtu yeyote kwa au kwa watu wengine;
    - (v) uchukuaji wa mali au huduma kwa mtu yeyote;
- (b) mali au huduma au vyote, vitakuwa-
  - (i) vinatolewa na mtu anayeanzisha mpango huo au, endapo mpango huo unaanzishwa na watu wawili au zaidi wanaotenda kwa ridhaa ya mmoja au zaidi;

- (ii) ilimradi kwa watu wengine walio chini ya utaratibu utakaohudhuriwa na washiriki, ikiwa ni kwa nafasi ya wakala wa mwanzishaji au mmoja wa waanzishaji au kwa nafasi nyingine yoyote;
  - (iii) imetumika kwa nia ya kusambaza mali yoyote au huduma kwa watu wengine chini ya mpango.
  - (iv) iliyosambazwa na muanzishaji au mionganoni mwa waanzishaji au kwa watu waliofahamishwa kwa mtu huyo au waanzishaji wengine (au mwajiriwa au wakala wake au wao) kwa washiriki.
- (5) Kwa ajili ya kifungu kidogo cha (2), mwanzishaji atachukuliwa kuwa na ushiriki endapo atamtunukia mshiriki huyo haki inayotambulika kisheria.
- (6) Kifungu hiki hakitatumika kwenye mpango wowote -
  - (a) ambao mwanzishaji au mionganoni mwa waanzishaji au washiriki wanafanya au wanatakiwa kufanya uwekezaji wa kibiasara ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzingatia sheria zilizopo; au
  - (b) vinginevyo vinaangukia ndani ya mpango uliotolewa msamaha.
- (7) Waziri anaweza, kwa kutoa amri itakayochapishwa kwenye gazeti la Serikali, kusamehe mpango wowote wa namna iliyoelezewa kwenye Kanuni, kutokana na utekelezaji wa kifungu hiki.

Katazo dhidi ya  
ushawishi  
Sheria Na.8  
ya 2006  
Jedw

- 171B.-(1)** Mtu yeyote anayeshawishi au kujaribu kushawishi mtu yeyote -
  - (a) kufanya malipo yoyote kwa ajili ya manufaa ya mwanzishaji au mionganoni mwa waanzishaji au, kwa ajili ya manufaa ya mshiriki yeyote kwenye mpango huo; au
  - (b) kuwa mshiriki na kufanya malipo yoyote kwa ajili ya manufaa ya mwanzishaji au, kwa ajili ya manufaa ya mshiriki yeyote kwenye mpango huo,

Atakuwa ametenda kosa na akipatatikana na hatia atapaswa kulipa faini isiyozidi milioni tano au kifungo kisichozidi miaka mitano.

(2) Wakati wa kuamua endapo ushawishi au kujaribu kushawishi

kumefanyika kwa kushikilia mategemeo, itatosha iwapo mategemeo yatakuwa sehemu muhimu ya ushawishi

- (3) iwapo kosa limetendwa na mshiriki yejote, kila mwanzilishi wa mpango huo atawajibika kwa kosa hilo kutendeka.
- (4) iwapo mtu atashtakiwa kwa kosa kuhusiana na tangazo, itakuwa kinga kwa mtu huyo kudhihirisha kwamba, yeje ni mtu ambaye biashara yake ni ya kuchapisha au kuandaa machapisho kwenye matangazo, na kwamba anapokea matangazo kwa ajili ya kuchapisha kama biashara yake na hakuju, na hakuwa na sababu ya kuhisi kwamba machapisho hayo ni makosa.
- (5) iwapo mwanzishaji atashtakiwa kwa sababu ya kosa lililotendwa na mtu mwingine kulingana na kifungu kidogo cha (4), itakuwa kinga kwa mtu huyo kuthibitisha kwamba kitendo kilichopeleke kosa kilifanyika bila ridhaa.

Fasiri  
Sheria No.8  
ya 2006 Jedw.

- 171C.-**(1) Kwa madhumuni ya vifungu vya 171A na 171B, isipokuwa kama itahitajika vinginevyo:-  
“bidhaa” inajumuisha mali yenze maelezo yoyote na haki ya au ziada iliyo kwenye mali yoyote;  
“washiriki” kuhusiana na mpango, inamaanisha mtu ambaye si mwanzilishi au yejote mionganoni mwa waanzilishi ambao ameshiriki kwenye mpango.  
“mpango” unamaanisha utaratibu uliofanywa kuhusiana na ufanyaji shughuli ikiwa utaratibu huo umefanywa wote au kwa sehemu kwa maandishi au bila maandishi  
(2) Marejeo kwenye utoaji au usambazaji wa bidhaa utatasfsiriwa kujumuisha marejeo kwenye kutoa au kuhamisha haki au ziada.

Nyumba za  
kupingiana

- 172.-**(1) Nyumba yoyote , chumba au sehemu itaitwa nyumba ya kupingia na kama itatumika kwa moja ya matumizi yafuatayo ambayo ni:-  
(a) kwa nia ya kupingiana humo kati ya mtu aliyekimbilia kwenye eneo hilo na:-  
(i) mmiliki, mtumiaji au mtunzaji wa sehemu hiyo, au mtu yejote anayetumia sehemu hiyo;  
(ii) mtu yejote aliyeanzisha au kuajiriwa na, au anayekaimu kwa niaba ya anayemiliki, anayeishi au kutunza au mtu anayetumia sehemu hiyo; au

- (iii) mtu yelete anayetunza au kusimamia, au kwa namna yoyote inavyofanywa biashara, katika sehemu hiyo;
- (b) kwa madhumuni ya fedha au mali itakayolipwa au kupokelewa mahali hapo na au kwa niaba ya mmiliki, mtumiaji au mtunzaji au mtu anayetumia sehemu hiyo kwa faida:-
- (i) kwa uhakika, kwa kutekeleza , kuahidi au makubaliano ya dhahiri au ya baadae, kulipa au kutoa kiasi chochote cha fedha au mali nyingine au tukio lolote au matumizi mengine ya au yanayohusiana na mashindano ya mbio za farasi au mashindano ya mbio nyingine, kupigana, mchezo au zoezi; au
- (ii) Kwa kupata malipo au kutoa kwa mtu mwingine kiasi chochote cha fedha au mali nyingine kwa tukio lolote au matumizi ya dharura.

(2) Mtu yelete ambaye mmiliki wa nyumba au mkazi wa nyumba yoyote, chumba au sehemu, ambaye kwa kujua na kwa makusudi ataruhusu mahali hapo pafunguliwe, pawekwe au kutumiwa kuwa ni nyumba ya mapingiano na mtu mwingine, au ambaye anatumia au kuisimamia au kusaidia kuendesha shughuli za biashara ya kipingiana mtu huyo atakuwa ametenda kosa na atahukumiwa adhabu ya kifungo cha mwaka mmoja jela.

Isipokuwa kwamba haitakuwa kosa kutumia totelezi (mtambo wa hesabu) kwa klabu ya; mbio, ya gymkhana au ya michezo inayotambulika na Serikali kwenye mkuutano wowote wa hadhara, kwa idhini ya Mkuu wa Polisi na; katika sharti hili neno “totelezi” lina maana ya chombo cha kuchanganya, mashine au kitu kingine chochote chenye asili au mpango unaowezesha idadi ya watu kipingiana wenyewe kwa kufuata mwenendo kama huo.

Kimefutwa

**173.** [Kimefutwa na Sheria Na. 23 ya1967 k. 25.]

Kimefutwa

**173A.** [Kimefutwa na R.L. Sura. 440 k. 16.]

Barua  
zinazofuatana,  
Sheria . Na. 32 ya  
1951

**173B.-**(1) Mtu yelete ambaye anatumia au kusababisha kutumwa barua zinazofuatana au atakayetuma au kupokea kiasi chochote cha fedha kuhusiana na barua zinazofuatana atakuwa ametenda kosa na atatakiwa kulipa faini ya shilingi elfu nne au kifungo kisichozidi miezi sita jela au vyote faini na kifungo.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki “Barua Zinazofuatana” maana yake ni nyaraka inayoandikwa kwa mtu mmoja kwa mtu mwingine ikimtaka yeye:-

Maana ya  
mtunzaji wa  
majengo.

- (a) kwamba anatakiwa kutuma waraka wenyewe ujumbe kama huo kwa watu wengine; na
- (b) Kwamba anatakiwa awakilishe fedha au kitu chenye thamani ya fedha kwa mtu au kwa anuani iliyonyeshwa kwenye waraka uliotangulia

- 174.** Mtu yeyote ambaye anaonekana, anatenda au anajiweka kama bwana mwenye nyumba au bibi mwenye nyumba au mtu mwenye dhamana ya kuangalia au kusimamia nyumba yeyote ya namna hiyo au chumba au vyumba au mahali kama ilivyotajwa katika vifungu vya 171 na 172 mtu huyo atahesabiwa kuwa ni mtunzaji wa nyumba hiyo, hata kama ni mtunzaji au si mtunzaji wa nyumba hiyo.

Upitishaji wa  
Matangazo ya  
Kinyaa . Sheria  
No. 3 ya 1995  
Sch.

**175.-(1)** Mtu yeyote ambaye:-

- (a) kwa madhumuni au kwa njia ya biashara au kwa madhumuni ya kusambaza au kuonyesha hadharani, anatengeneza, anatoa au anakuwa nacho mikononi mwake, maandishi, michoro, makaratasi ya matangazo, picha, nembo, picha, filamu au kitu kingine chochote kinachowezza kuharibu utu wa mtu;
- (b) kwa madhumuni yaliyotajwa kwenye aya ya (a) anachukua, anasafirisha au kuingiza vitu kama hivyo, au kwa namna yoyote iwayo akaeneza katika mzunguko kimoja wapo katika hivyo vilivyotajwa; au
- (c) anafanya au anashiriki katika biashara yoyote, iwe kwa hadhara au kwa siri au anajihuisha na vitu hivyo kwa namna yoyote iwayo au kuvigawanya au kuvionyesha hadharani au kufanya biashara ya kuviazimishaa vitu hivyo;
- (d) anatangaza au anajulisha kwa namna yoyote ile iwayo ikiwa ni kwa nia ya kusaidia usambazaji wa, au usafirishaji kwenye jambo kama hilo, kwamba mtu huyo anajihuisha kwenye matukio yanayozungumziwa na kifungu hiki, au kutangaza au kufanya mtu kujua, au kutoka kwake anawezesha vitu hivyo aidha kupatikana moja kwa moja, au kupitia mtu mwingine; au
- (e) anaonyesha hadharani maonyesho au michezo isiyofaa au michezo unaoelekea kuharibu maadili,

atakuwa ametenda kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka miwili au faini ya shilingi laki mbili.

(2) Ikiwa makosa yaliyotajwa katika aya ya (a), (b), (c) au (d) ya kifungu kidogo cha (1), tendo lolote linalounda kosa litakalotendwa Tanzania bara, utendaji wa tendoo hilo litatosha kumfanya mtuhumiwa shitaka lake kusikilizwa Tanzania Bara.

- (3) Mahakama, wakati wa kumtia hatiani mtu huyo kwa kosa lililomo kwenye kifungu hiki, inaweza kuamuru kitu chochote kinachomilikiwa au kilichotumika kwa ajili ya kosa hilo, kuharibiwa.
- (4) Mahakama inaweza, baada ya kupokea maombi ya waendesha mashitaka wa serikali, kuamuru kuharibiwa kwa kitu chochote chenye kuvunja maadili hata kama mtu huyo ametiwa hatiani au ameachiwa huru chini ya masharti ya kifungu hiki kuhusu kitu hicho cha aibu.

Wavivu na  
wazembe..  
Sheria Nos  
49 ya 1962;  
11 ya 1983  
Jedwali

176 Mtu yejote kati ya watu wafuatao:-

- (a) Malaya mzoefu atakayefanya vitendo vya aibu mbele ya hadhara au kuzurura au kushawishi mahali popote pa hadhara kwa ajili ya kufanya umalaya;
- (b) mtu anayetangatanga au anayejiweka katika mahali popote pa hadhara kwa kuomba au kukusanya sadaka, kumtuma au kumhimiza mtoto kufanya hivyo;
- (c) mtu anayecheza kamari kwa fedha au thamani ya fedha katika mahali pa hadhara;
- (d) mtu anayetangaza nje ya nchi na kujaribu kupata au kukusanya sadaka kwa kuonyesha majeraha au kilema;
- (e) mtu anayejiweka, mbele ya hadhara katika hali ambayo inapelekea uvunjifu wa amani;
- (f) mtu anayetenda kitendo cha aibu mbele ya hadhara bila ya udhuru wa halali; na
- (g) mtu anayeshawishi kwa mambo yasiyokuwa ya kimaadili mahali pa hadhara;
- (h) mtu mwenye afya kamili ambaye hajishughulishi katika kazi

yoyote ya uzalishaji na hana namna yoyote inayoonekana waziwazi ya kujikimu; au

- (i) mtu aliyeajiriwa chini ya ajira halali inayotambulika ambaye, bila udhuru halali, anapatikana akichezacheza au kufanya mzaha wakati wa muda wa kazi,

atahesabiwa kuwa ni mtu mvivu na mzembe na atapaswa kulipwa faini isiyozidi shilingi mia tano au kifungo kisichozidi miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

Mahala pa  
kuhifadhi  
makahaba.  
Sheria No. 49 ya  
1962 s. 3

**176A.** Mtu yejote akiwa ni muuza kilabu ya pombe, hoteli, nyumba, duka, chumba au mahali pengine panapofikiwa na watu mara kwa mara kwa ajili ya kununua au kunywa viburudisho vya namna yoyote, anayeruhusu au kukubali kwa makusudi makahaba wa kawaida kukusanyika na kubaki katika jengo lake kwa ajili ya ukahaba, mtu huyo atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi mia tano au, iwapo ni kosa la mara ya pili na kuendelea atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu moja

Wazembe na  
Wazururaji,  
Sheria Nos.  
3 ya 1950 s. 2;  
10 ya 1959 s. 4;  
49 ya 1962 s. 4;  
G.N. No. 73 ya  
1965

**177 Yeyote mionganoni mwa watu wafuata-**

- (a) mtu aliyepatikana na makosa kwa mujibu wa fungu la 176 baada ya kuwa alipata kuonekana na makosa zamani ya kuwa mzembe na mzururaji;
- (b) mtu anayetangatanga kwa ukusanyaji sadaka au kujaribu kupata mchango au msaada wa namna yoyote kwa njia ya kujisingizia au hadaa;
- (c) mtu aliyetuhumiwa au mwizi mashuhuri ambaye hana njia zinazoonekana bayana za kupata maisha na hawezi kujieleza sawa sawa;
- (d) mtu anakayeonekana ndani au kwenye au karibu na nyumba yoyote au katika njia au barabara yoyote au mahali popote karibu na njia au barabara, au katika mahali popote pa hadhara katika wakati na hali ambayo yapeleke kana kwamba mtu huyo yupo hapo kwa jambo lisilo halali au la kikorofi;
- (e) mtu ambaye bila ya ruhusa ya maandishi ya Mkuu wa Wilaya au ikiwa ni manispali au mji, afisa mkuu wa polisi wa manispaa hiyo au mji huo, atakusanya au kuomba michango ya fedha ya jambo lolote katika mahali popote pa hadhara

ndani ya wilaya hiyo, manispaa au mji huo.

atahesabiwa kuwa ni muhuni na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miezi mitatu jela, na kwa kila kosa litakalofuata kifungo cha mwaka mmoja jela.

Isipokuwa kwamba aya ya (e) ya fungu hili haitamhusu-

- (a) mtu ye yeyote ambaye au yule ambaye ni mwakilishi wa taasis amepata ruhusa kwa maandishi kutoka kwa Mkuu wa Jeshi la polisi, kukusanya au kuomba michango ya fedha kwa ajili ya mambo ya dini au misaada; au
- (b) mtu ye yeyote aliyeruhusiwa kukusanya au kuomba mchango wa fedha kwa mujibu wa sheria yoyote, zikiwemo sheria za miji zinayotumika hapa Tanzania Bara

Isipokuwa kwamba kwa madhumuni ya aya ya (e) ya kifungu hiki ufanuzi wa neno la “mahali pa hadhara” katika fungu la 5 la kanuni hii halitahesabiwa kuchanganya mahali popote panapotambulikana kuwa ni mahali pa kuabudia

Kuacha kutoa hesabu ya fedha iliyokusanywa kwa matumizi ya Umma No. 3 of 1950 s. 3; Act No. 2 of 1972 Sch.

**177A.** Kwa mujibu wa masharti ya sheria nyingine yoyote, zikiwemo sheria za miji, mtu ye yeyote awe amepata idhini ya maandishi kama ilivyotajwa katika sharti lililo mwishoni mwa kifungu cha 177 au hakupata au ameruhusiwa kama ilivyo katika aya ya (a) na (b) ya sharti hilo la kwanza na, ambaye baada ya kukusanya au kutuma kukusanya fedha ya michano katika Tanzania Bara ataacha kutoa hesabu sahihi na kamili ya fedha yote aliyopokea katika michango hiyo na namna alivyo zitumia, kumpelekeea Mkuu wa Wilaya au afisa wa polisi, manispaa au miji ikitakiwa nao, au kutangaza hesabu hiyo katika gazeti litakalochaguliwa na Mkuu wa wilaya au afisa wa polisi, mtu huyo atakuwa amekosa na kwa kosa la kwanza atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka miwili jela na kwa makosa yatakayofuata, kifungo cha miaka mitatu.

Makosa yanayohu su uvaaji wa vazi rasmi bila mamlaka R.L. Sura 455 kif. 23; G.Ns. Na. 478 ya 1962; 73 ya 1965

**178.-**(1) Mtu ye yeyote ambaye hatumikii jeshi la Ulinzi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wala jeshi lolote la polisi lililowekwa kwa sheria, akivaa bila ruhusa ya Raisi vazi rasmi la jeshi lolote katika hayo yaliyotajwa au vazi lolote linalofanana na vazi rasmi hilo au kuwa na alama ya kiaskari au alama yoyote ya dhahiri ya hilo vazi rasmi, atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha mwezi mmoja jela au faini ya shilingi mia mbili.

Isipokuwa kwamba hakuna kitu chochote katika fungu hili kitakachomzuia mtu ye yeyote kuvala vazi rasmi lolote au vazi katika michezo

ya tamasha inayochezwa mahali popote ambapo michezo hiyo yaruhusiwa kuchezwa hadharani, au katika ukumbi unaochezwa muziki au sarakasi au wakati anapoigiza au kuwakilisha jeshi kwa nia njema.

(2) Mtu yejote ambaye bila halali anavaa vazi rasmi la jeshi lolote miengoni mwa majeshi yaliyotajwa kwenye kifungu kidogo cha (1) hapo juu, au vazi lolote linalofanana na hilo vazi rasmi, au kuwa na alama ya kiaskari au alama yoyote ya dhahiri ya hilo vazi kwa namna au hali ambayo huenda ikaleta dharau juu ya vazi hilo rasmi, au kumuajiri mtu mwininge kuva vazi rasmi hilo au nguo kama hiyo, mtu huyo amekosa na atapaswa adhabu ya kufungo cha miezi mitatu au faini ya shilingi mia nne.

- (3) Mtu yejote ambaye akiwa hayumo katika utumishi wa Jeshi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wala hakupata kupokea ruhusa ya maandishi kutoka kwa mkuu wa polisi kufanya hivyo, anaingiza au anauza au anamiliki kwa ajili ya kuuza vazi rasmi lolote kama ilivyotangulia kutajwa, au vifungo au beji zinazohusu vazi rasmi hilo, atakuwa ametenda kosa na atawajika kwa adhabu ya kifungo cha miezi sita au faini ya shilingi elfu mbili.
- (4) Mtu anakayepatikana na makosa chini ya fungu hili, vazi rasmi, nguo, kifungo, beji au kitu chochote ambacho kwacho kimefanyiwa kosa kitahodhiwa isipokuwa kama itaamriwa vingine na mahakama.

Kitendo cha  
uzembe ambacho  
kinaweza kueneza  
maambukizo

**179.** Mtu yejote ambaye bila halali au kwa uzembe anatenda kitendo chochote ambacho kinaweza kueneza na ambacho anajua au ana sababu za kuamini kinaweza kueneza maambukizo ya maradhi ya hatari kwa maisha ya watu, atakuwa ametenda kosa.

Kuchanganya na  
kitu kingine  
chakula au  
kinywaji  
kinachokusudiwa  
kuuzwa

180. Mtu yejote ambaye anachanganya na kitu kingine chakula au kinywaji chochote kiasi cha kukifanya chakula hicho au kinywaji hicho kiwe na madhara kwa kutumika kama chakula au kinywaji, hali akijua kwamba huenda chakula hicho au kinywaji hicho kikauzwa kuwa chakula au kinywaji, atakuwa ametenda kosa.

Kughushi chakula  
au kinywaji  
kinachokusudiwa  
kuuzwa

181. Mtu yejote ambaye anauza, anatembeza, au anatoa nje kwa ajili ya kuuza, chakula au kinywaji chochote ambacho kimefanywa kidhuru na kimekuwa na madhara au kuwa katika hali isiyofaa kwa chakula au kinywaji, hali akijua au kuwa na sababu ya kuamini kwamba chakula hicho au kinywaji hicho kina madhara kwa kutumika kama chakula au kinywaji, atakuwa ametenda kosa.

- Kughushi madawa      182. Mtu yejote ambaye anaghushi dawa yoyote au anafanya matayarisho ya dawa kwa utaratibu au kwa namna ambayo itapunguza nguvu au kugeuza kazi ya dawa hiyo au matayarisho hayo ya utibabu au kuifanya idhuru, akikusudia kwamba dawa hiyo itauzwa au kutumika kwa ajili ya matibabu kama kwamba haikugushiwa, atakuwa ametenda kosa.
- Kuuza madawa yaliyoghushiwa      183. Mtu yejote ambaye akijua dawa yoyote au matayarisho ya utibabu yameghushiwa kwa namna ambayo inapunguza nguvu yake au imageuza kazi yake, kuwa na madhara, akaiza dawa hiyo au kuitembeza au kuitoa nje kwa kuuza au kuitoa katika kituo chochote cha afya kwa ajili ya matibabu ya mtu yejote asiejua kama imeghushiwa, atakuwa ametenda kosa.
- Kuchafua maji      184 Mtu yejote ambaye kwa makusudi anaharibu au anachafua maji kwenye chemchem ya watu au birika, kiasi cha kuyafanya maji hayo yapunguze ufaaji wake kwa matumizi ya kawaida yaliyokusudiwa, atakuwa ametenda kosa.
- Kuchafua hewa      185. Mtu yejote ambaye kwa makusudi anachafua hewa ya mahali popote kiasi cha kuifanya hewa hiyo iwe na madhara kwa afya ya watu kwa ujumla wanaokaa au kufanya kazi jirani na mahali hapo au wanaopita njia ya watu wote, atakuwa ametenda kosa.
- Biashara mbaya      **186** Mtu yejote ambaye kwa madhumuni ya biashara au madhumuni mengine, atafanya kelele nyingi au harufu mbaya ya kudhuru afya katika maeneo na mazingira na kuudhi idadi kubwa ya watu wanaotumia haki zao za kawaida, atakuwa ametenda kosa na atapaswa adhabu ilioainishwa na kifungu kidogo cha (1) cha fungu la 170.
- SURA YA KUMI NA NANE  
KASHIFA
- Vimefutwa      **187.-194.** [Vimefutwa na Sheria Na. 3 ya 1976 kif. 55<sup>3</sup>.]  
SURA YA KUMI NA TISA  
MAKOSA YA KUHODHI BIDHAA NA YANAYOHUSIANA
- Kuhodhi Bidhaa Sheria Na.. 11 ya 1983 Jedwali Na.. 12 ya 1987 kif. 23      **194A.**-(1) Mtu yejote, ikiwa ameruhusiwa au hajaruhusiwa kufanya biashara ya kuuza bidhaa ya namna yoyote atakuwa ametenda kosa la kuhodhi bidhaa chini ya kifungu jiki iwapo, sio mtengenezaji au mzalishaji wa bidhaa hiyo na-
- (a) anapatikana na bidhaa hiyo ikiwa na thamani ya milioni moja

au pungufu, na ikiwa bidhaa hiyo inahitajika na jamii kwenye eneo husika, kwa namna ambayo itachukuliwa kuwa haijaonyeshwa au kuhifadhiwa kwa ajili ya mauzo halali au matumizi halali au kupatikana kwa ajili ya kununuliwa na mtu yejote kwa malipo ya bei halali;

- (b) anauza au anatoa bidhaa yoyote kwa ajili ya kuuza kwa bei au kwa makubaliano ambayo si halali kisheria au ambayo kwa kuzingatia hali halisi, si ya kawaida; au
- (c) wakati wa kufanya biashara ya kuuza bidhaa yoyote, anajihuisha na uuzaaji ambaa una nia au unaweza-
- (j) anasababisha upungufu wa upatikanaji wa bidhaa hiyo; au
  - (iii) anaongeza upungufu uliopo wa upatikanaji wa bidhaa yoyote; au
  - (iv) anasababisha isivyo halali kupanda au kushuka kwa bei ya kawaida au bei ya bidhaa yoyote inayokubalika kibiashara; au
  - (v) anaharibu usambazaji halali wa bidhaa kwa wanunuvi wa eneo husika na akipatikana na hatia atawajibika kwa adhabu ya kifungo kisichozidi miaka kumi na nne au faini isiyozidi shilingi laki moja au vyote kwa pamoja; na mahakama inaweza, kwa nyongeza kuagiza kwamba bidhaa hizo zitaifishwe na Serikali, isipokuwa pale ambapo mtu mwingine atairidhisha mahakama kwamba baadhi ya bidhaa hizo zinamilikiwa naye na si za mtuhumiwa, na mtu huyo hakutenda kosa chini ya kifungu hiki.

Sura ya.229

---

<sup>3</sup> Kwa makosa yanayohusiana na kashfa ambayo mwanzoni yalikuwa chini ya kifungu cha 184 hadi kifungu cha 194 , angalia Sheria ya Magazeti , Sura ya 229

- (2) kwa madhumuni ya kifungu hiki–
  - (a) mtu atachukuliwa kuwa amehifadhi bidhaa ya aina yoyote mahali popote kama ni mmiliki wa kiasi chochote cha bidhaa hiyo;
  - (b) “mtu” anajumuishwa pia mwajiriwa yejote au wakala wa mtuhumiwa (ikiwa ajira au uwakala wa mtu huyo ni wa

kisheria au si wakisheria) na endapo mwajiriwa atatuhumiwa kwa kosa chini ya aya hii, kifungu kidogo cha (3) kitatumika vivyo hivyo kwa mwajiriwa au wakala kama kinavyotumika ikiwa mtuhumiwa ni mwajiri au endapo ni wakala;

- (c) ikiwa ameruhusiwa au hajaruhusiwa kufanya biashara, mtu atachukuliwa kuwa anafanya biashara ya kuuza bidhaa za aina yoyote endapo, wakati uhalifu unasadikiwa kutendeka au muda uliotangulia au muda uliofuata tarehe ambayo kosa linadhaniwa kutendeka, mtu huyo alikuwa na kiasi fulani cha bidhaa hiyo kwenye mazingira ambayo yanadhaniwa kwamba mtu huyo alikusudia kuiuza bidhaa hiyo au yeze mwenyewe kujifanya muuzaji wa bidhaa hiyo.
- (3) Ikiwa mtu atashtakiwa kwa kosa chini ya kifungu hiki, atakuwa na utetezi mzuri akithibitisha kwamba-
  - (a) kulikuwa hakuna upungufu kwenye usambazaji wa bidhaa hiyo kwenye eneo husika;
  - (b) uhifadhi wa kiasi cha bidhaa hiyo husika haukudhamiria au kuweza kusababisha upungufu wowote kwenye usambazaji wa bidhaa hiyo kwenye eneo husika;
  - (c) bidhaa iliyokutwa kwenye eneo lolote chini ya usimamizi au uongozi wa mtu huyo siyo yake na kwamba hana haki ya kuihamisha kwa namna yoyote na aliishauri mamlaka zinazochunguza suala hilo mapema kuhusu utambulisho wa mwenye mali hiyo;
  - (d) bidhaa inayomilikiwa na mtu huyo au ikiwa ana haki ya kuihamisha, wakati amepatikana na mali hiyo, alikuwa na uwezo kisheria wa kuuza au vinginevyo kuihamisha kwenda kwa mtu mwingine;
  - (e) bidhaa aliyoihodhi ilikuwa ni kwa ajili ya matumizi yake halali au kwa ajili ya matumizi yanayohusiana na biashara yake halali; au
  - (f) aliweka bidhaa hiyo kwenye ghalaa kama kinga anayoichukua kwa familia yake dhidi ya upungufu wa chakula au njaa au ili kutimiza matakwa ya mambo yake muhimu ya baadae.
- (4) Kiwango cha mtuhumiwa kuthibitisha maelezo au mazingira yaliyowekwa na kifungu kidogo cha (3) kitakuwa katika uwiano wa mashaka.

*Kigawo cha Nne. – Makosa kuhusu Watu*

**SURA YA ISHIRINI**  
**KUUWA KWA KUKUSUDIA NA KUUWA BILA KUKUSUDIA**

Kuuwa bila  
kukusudia

**195.-**(1) Mtu yeoyote ambaye, kwa kitendo kisicho halali au kuacha kutenda , anasababisha kifo cha mtu mwingine, ana hatia ya kuua bila kukusudia.

(2) Kuacha kutenda isivyo halali ni kuacha kutenda ambako kunasababisha kuzembea kutimiza wajibu unaohusika na hifadhi ya maisha au afya, iwe kutofanya hivyo kumeandamana au hakukuandamana na kusudi la kusababisha kifo au maumivu ya mwili.

Kuuwa kwa  
kukusudia

**196.** Mtu yeoyote ambaye, kwa dhamira ya uovu, anasababisha kifo cha mtu mwingine kwa kitendo kisicho halali au kuacha kutenda ana hatia ya kuua kwa kukusudia.

Adhabu ya kuua  
kwa kukusudia

**197.** Mtu ambaye amepatikana na hatia ya kosa la kuuwa kwa kukusudia atahukumiwa adhabu ya kifo

.

Adhabu ya kuua  
bila kukusudia

**198.** Mtu yeoyote ambaye anatenda kosa la kuuwa bila kukusudia atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha.

Hatia kwa kosa  
la kuua mtoto  
mchanga katika  
baadhi ya kesi

**199.** Pale ambapo mwanamke kwa kitendo chochote cha makusudi au kuacha kutenda kitendo hicho amesababisha kifo cha mtoto wake mwenye umri wa chini ya miezi kumi na mbili, lakini wakati wa kitendo hicho mama huyo alikuwa hajapona kutokana na kuzaa mtoto huyo na kwa sababu hiyo au kwa sababu inayohusiana na unyonyeshaji baada ya kuzaa mtoto huyo akili yake ilidhurika, bila kujali kwamba mazingira yalikuwa hivyo lakini kwa kufuata kifungu hiki ingaliweza kuwa kosa la kuua kwa kukusudia, atakuwa na hatia ya kosa la kuua mtoto mchanga, na anaweza, kushughulikiwa na kuhukumiwa kwa kosa kana kwamba alikuwa na hatia ya kumuua mtoto huyo bila kukusudia.

Nia ya uovu

**200.** Nia ya uwovu itahesabiwa kuwepo kutokana na ushahidi wa

kudhibitisha mojawapo katika mambo yafuatayo-

- (a) dhamira ya kusababisha kifo au dhara kubwa kwa mtu yeyote, aidha mtu huyo ndiye aliyeuawa au siye;
- (b) kujua kwamba kitendo au kuacha kitendo kinachosababisha kifo kinaweza kusababisha kifo au dhara kubwa kwa mtu, aidha mtu huyo ndiye hasa aliyeuwawa au siye, ingawa kujua huko kunaambatana na tofauti kwamba kifo au dhara kubwa limesababishwa au la, au kwa tazamio kwamba inaweza isisababishwa;
- (c) dhamira ya kutenda kosa linaloadhibiwa kwa adhabu ambayo ni kubwa kuliko kifungo cha miaka mitatu;
- (d) dhamira ya kutenda au kutotenda ili kurahisisha ukimbizi au utorokaji, kutoka kwenye ulinzi wa mtu yeyote ambaye ametenda au amejaribu kutenda kosa.

Kuua kwa  
kukasirishwa

Maana ya  
kukasirishwa  
Sheria Na. 16 ya  
1946 kif: 2

201. Pale ambapo mtu ambaye isivyokuwa halali anamuua mwingine katika mazingira ambayo, lakini kwa masharti ya kifungu hiki ingalifanya kosa la kuua kwa kukusudia, anatenda kitendo ambacho kinasababisha kifo akiwa katika hali ya joto la hasira iliyosababishwa na kukasirishwa kwa ghafla kama ilivyofafanuliwa katika kifungu cha 202, na kabla ya kuwepo muda wa hasira kupoa, ana hatia ya kuuwa bila kukusudia tu.

**202.-**(1) Neno “kukasirishwa” maana yake ni, isipokuwa kama itakavyoolezwa hapa chini, kitendo chochote cha maudhi au tusi la namna yoyote, ambayo akitendewa mtu wa kawaida au akitendewa mbele ya mtu wa kawaida kwa mtu mwingine aliyemo katika uangalizi wake halisi, au kwa mke, mume, mzazi, mwana, ndugu, tajiri au mtumishi kwa kumsababisha asimudu kujizuwia nafsi yake na kumshawishi kufanya shambulio kama alilolifanya huyo mshtakiwa kwa mtu aliyetendewa kitendo hicho au aliyetukanwa.

(2) Wakati ambapo kitendo kama hicho kinatendwa au tusi kama hilo linatolewa na mtu kwa mtu mwingine au mbele ya mtu mwingine kwa mtu aliye katika uangalizi halisi wa huyo mwingine au kwa mtu ambaye huyo mwingine amehusika nayo vyovoyote kama ilivyokwishatajwa katika kifungu kidogo cha (1) huyo mtendaji wa kitendo hicho wa kwanza amemtia hasira yule mwingine ya kufanya.

- (3) Kitendo halali hakimkasirishi mtu yeyote kufanya shambulio.
- (4) Kitendo chochote ambacho mtu akikitenda kutokana na

uchochazi uliofanywa na mtu mwingine ili kumshawishi atende kitendo hicho na kisha iwe ni kwa kufanya shambulio, siyo kumkasirisha mtu mwingine huyo kufanya shambulio.

- (5) Kukamatwa kusiko halali si lazima kukasirishe kwa kiasi cha kuweza kufanya shambulio, lakini kinaweza kuwa ni ushahidi wa kumkasirisha mtu ambaye anajua kuwa ni kinyume cha sheria
- (6) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, usemi “mtu wa kawaida” maana yake ni mtu wa kawaida katika jamii aliyomo mshtakiwa.

Maana ya  
kusababisha kifo

**203** Mtu atachukuliwa kwamba amesababisha kifo cha mtu mwingine, ingawa kitendo chake hakikusababisha kifo papo kwa papo au si sababu pekee ya kifo , katika mojawapo ya mazingira yafuatayo:-

- (a) iwapo amemtia mtu mwingine jeraha mwilini ambalo matokeo yake yamefanya mtu huyo mwingine kufanyiwa upasuaji au matibabu yaliyosababisha kifo; katika mazingira ambayo haijalishi kama matibabu hayo yalikuwa sawa au yalikosewa, kama yalifanywa kwa nia njema na ujuzi wa kawaida na ustadi; lakini mtu aliyetia jeraha hilo hafikiriwi kwamba amesababisha kifo hicho ikiwa matibabu yalikuwa ni sababu ya kifo cha papo kwa papo hayakufanywa kwa nia njema au yalifanywa bila ujuzi wa kawaida au ustadi.
- (b) iwapo anamtia mtu mwingine jeraha ambalo lisingalisababisha kifo kama mtu huyo aliyejeruhiwa alipata upasuaji au matibabu halisi au aligundua tahadhari muhimu juu ya namna ya kuishi kwake.
- (c) iwapo kwa kutumia nguvu au kwa kutishia anasababisha mtu mwingine kutenda kitendo ambacho kinasababisha kifo cha mtu mwingine huyo, kitendo ambacho ni njia ya kuepusha utumiaji wa nguvu ambacho katika mazingira hayo kingekuwa ni cha kawaida kwa huyo mtu ambaye kifo chake kimesababishwa hivyo;
- (d) iwapo kwa kitendo chochote au kutokitenda kitendo hicho anaharakisha kifo cha mtu anayeugua maradhi yoyote au jeraha lolote ambalo, tofauti na kitendo hicho au kuacha kutenda hicho maradhi hayo au jeraha hilo yangalisababisha kifo;

- (e) iwapo kitendo chake au kuacha kutenda kwake kusingesababisha kifo isipokuwa kama kungeambatana na kitendo au kuacha kutenda kwa mtu aliyeuawa au mtu mwingine.

Wakati ambapo  
mtoto  
anadhaniwa  
kuwa ni mtu

Kikomo cha  
muda wa kufa

**204** Mtoto anakuwa mtu wa kuweza kuuawa anapomaliza kabisa kuzaliwa akiwa katika hali ya uhai, awe ametoa pumzi au la, awe anajitegemea mwenyewe kwa mwenendo wa damu au sivyo na iwe kitovu kimekatwa au sivyo.

**205.-**(1) Mtu hachukuliwi kwamba amemuuwa mwingine kama kifo cha mtu huyo hakikutokea ndani ya mwaka mmoja na siku moja tangu siku hiyo ya sababu ya kifo.

(2) Kwa madhumuni ya kuhesabu muda uliotajwa kwenye kifungu kidogo cha(1) hapo juu-

- (a) muda huo utajumuisha siku ile ambayo kitendo cha mwisho kisicho halali kinachohusiana na sababu ya kifo hicho kilitendeka;
- (b) Pale ambapo sababu ya kifo ni ukosefu wa kuangalia au kufanya wajibu fulani, muda huo unahesabiwa pamoja na ile siku ambayo ukosefu wa kuangalia au kufanya wajibu huko ulikoma;
- (c) Pale ambapo sababu ya kifo kwa sehemu moja ni kitendo kisicho halali na sehemu moja kwa kukosa kuangalia au kufanya wajibu fulani, muda huo utahesabiwa pamoja na ile siku ambayo kitendo cha mwisho kisicho halali kilitendeka au ile siku ambayo ukosefu wa kuangalia au wa kufanya wajibu huo ulikoma, mojawapo litakalokuja mwisho ndilo litakalohesabiwa.

#### SURA YA ISHIRINI NA MOJA

Wajibu wa mtu  
anayetuunza mtu  
mwingine  
mwingine

#### WAJIBU KUHUSU HIFADHI MAISHA NA AFYA

**206.** Itakuwa ni wajibu wa kila mtu mwenye uangalizi juu ya mtu mwingine ambaye kwa sababu ya umri, maradhi, upungufu wa akili, kuwekwa kizuijini au kwa sababu nyingine yoyote itakayomfanya asiweze kujiangalia nafsi yake, na ambae hawezu kujipatia mahitaji ya maisha, ama uangalizi huo ni kwa kuajiriwa au kutokana na sheria, au kutokana na kitendo chochote cha halali au kisichokuwa cha halali cha muangalizi huyo, kumpatia mtu huyo mwingine mahitaji ya maisha na

atahesabiwa kusababisha matokeo yoyote yanayoweza kudhuru maisha au afya ya mtu huyo mwingine, kwa sababu ya kuacha kufanya wajibu wake huo.

#### **Wajibu wa mkuu wa familia**

207. Ni wajibu wa kila mtu ambaye, kama mkuu wa familia, ana uangalizi wa mtoto aliye na umri wa chini ya miaka kumi na nne akiwa ni mmoja wa watu wa nyumbani kwake, kumpatia mtoto huyo mahitaji ya lazima ya maisha; na ahesabiwa kusababisha matokeo yoyote yenye kudhuru maisha au afya ya mtoto huyo, kwa sababu ya kuacha kutekeleza wajibu wake huo.

#### **Wajibu wa mwajiri**

208. Ni wajibu wa kila mtu , akiwa mwajiri awe wa kiume au wa kike ambaye amechukua madaraka ya kutoa mahitaji ya lazima kama chakula , nguo au malazi kwa mtumishi au mwanafunzi mwenye umri chini ya miaka kumi na sita kutoa vitu hivyo; na atahesabiwa kusababisha matokeo yoyote yenye kudhuru maisha au afya ya mtumishi au mwanafunzi huyo kwa sababu ya kuacha kutimiza wajibu wake huo.

#### **Wajibu wa watu wanaofanya vitendo nya hatari**

209. Ni wajibu wa kila mtu ambaye, isipokuwa ikilazimika, anachukuwa madaraka ya kufanya utabibu wa kupasua au wa kutoa dawa kwa mtu mwingine yejote, au kufanya kitendo kingine chochote cha halali ambacho ni cha hatari au kinaweza kuwa cha hatari kwa maisha au afya ya mwanadamu, kuwa na ustadi wa kufaa na kutumia uangalifu wa kutosha katika kufanya shughuli hiyo; na atahesabiwa kusababisha matokeo yoyote yenye kudhuru maisha au afya ya mtu yejote kwa sababu ya kuacha kufuata au kufanya wajibu huo.

#### **Wajibu wa watu wanaotunza vitu hatari**

210. Ni wajibu wa kila mtu kuwa mwangalifu nya kutosha na kuchukuwa tahadhari za kutosha kuzuia hatari iwapo ana uangalizi au usimamizi wa kitu chochote, kiwe chenyé uhai au kisicho na uhai, na kiwe kinahamishika au kisichohamishika cha namna ambayo kikikosa uangalizi au tahadhari katika matumizi au uongozi wake, maisha, usalamu au afya ya mtu yejote yanaweza kuhatarishwa; na atahesabiwa kusababisha matokeo yoyote yenye kudhuru maisha au afya ya mtu yejote kwa sababu ya kuacha kufanya wajibu huo.

### **SURA YA ISHIRINI NA MBILI MAKOSA YANAYOHUSIANA NA NA KUUWA KWA KUKUSUDIA NA KUJIUA**

Kujaribu kuua  
kwa kukusudia

#### **211. Mtu yejote ambaye-**

- (a) anajaribu isivyo halali kusababisha kifo cha mwingine; au

- (b) kwa kukusudia isivyo halali kutaka kusababisha kifo cha mwingine, anatenda kitendo chochote, au anaacha kutenda kitendo chochote ambacho ni wajibu wake kukitenda, kitendo cha kutenda au kuacha kutenda kikawa ni cha namna ya kuweza kuhtarisha maisha ya mwanadamu.

Atakuwa anatenda kosa na atahukumiwa kifungo cha maisha.

Kimefutwa

**212.** [Kimefutwa na sh. No. 47 ya1954 kifungo cha 3.]

Mfichaji wa  
muuaji wa  
kukusudia

**213** Mtu yejote atakayekuwa mfichaji wa mauaji ya kukusudia ana hatia ya kosa na atahukumiwa kifungo cha miaka saba.

Maandishi ya  
kutishia kuuwa  
kwa kukusudia

214. Mtu yejote ambaye, akijua maudhui yaliyopo kwenye maandishi, ama moja kwa moja au vinginevyo anasababisha mtu yejote kupokea maandishi yoyote yakutishia kuua mtu yejote ana hatia ya kosa na atahukumiwa kifungo cha miaka saba .

Njama za kuua  
kwa kukusudia

215. Mtu yejote anakayekula njama na mtu mwingine yejote kumuua mtu yejote, iwe mtu huyo yuko Tanzania Bara au pengine, mtu huyo atakuwa anatenda kosa na atawajibika kutumikia kifungo cha miaka kumi na nne jela.

Kumsaidia mtu  
kujiua

**216.** Mtu yejote ambaye–

- (a) anasababisha mtu mwingine ajiuze; au
- (b) anamshauri mtu mwingine ajiuze na akamshawishi kufanya hivyo; au
- (c) anamsaidia mtu mwingine ajiuze,

atakuwa anatenda kosa na atahukumiwa kifungo cha maisha .

Kujaribu kujiua

**217** Mtu yejote anayejaribu kujiua ana hatia ya kosa.

Kuficha kuzaliwa  
kwa mtoto

218. Mtu yejote ambaye, pale ambapo mwanamke anazaa mtoto anajitahidi kwa njia yoyote ya siri, kuisarifu maiti ya mtoto huyo ili kuficha kuzaliwa kwa mtoto huyo, iwe mtoto huyo alikufa kabla ya kuzaliwa au wakati wa kuzaliwa au baada ya kuzaliwa, atakuwa anatenda kosa.

Kuharibiwa kwa  
mtoto

**219.-**(1) Kwa kufuata masharti ya kifungu kidogo cha (2) mtu yeoyote ambaye, anakusudia kuharibu maisha ya mtoto ambaye anaweza kuzaliwa akiwa hai, kwa kitendo chochote cha kunuwia anasababisha mtoto huyo kufariki kabla hajawa na maisha ya kutomtegemea mama yake, atakuwa anatenda kosa la kuangamiza mtoto, na atahukumiwa kifungo cha maisha jela.

(2) Mtu atakuwa na hatia ya kosa chini ya kifungu hiki isipokuwa kama imedhibitishwa kwamba, kitendo kilichosababisha kifo cha mtoto huyo kilitendwa kwa nia njema kwa madhumuni tu ya kuokoa maisha ya mama yake.

(3) Kwa ajili ya kifungu hiki, kukiwa na ushahidi kwamba katika wakati fulani mwanamke alikuwa mjamzito kwa kipindi cha majuma ishirini na nane au zaidi, utakuwa ni uthibitisho ulio wazi kwamba wakati huo alikuwa na ujauzito wa mtoto wa kuweza kuzaliwa akiwa hai.

#### SURA YA ISHIRINI NA TATU MAKOSA YA KUHATARISHA MAISHA AU AFYA

Kulemaza kwa  
nia ya kutenda  
kosa  
Sheria. Na. 47 ya  
1954 kif. 3

**220**     Mtu yeoyote ambaye, kwa njia yoyote inayokusudiwa kusaidia kuzuia pumzi, kumkosesa mtu hewa au kukaba koo, na kwa kusudi la kutenda au kurahisisha kutenda kosa au kurahisisha kukimbiza kwa mkosaji baada ya kutenda au kujaribu kutenda kosa, anafanya au anajaribu kufanya kitendo cha kumfanya mtu yeoyote asiweze kupinga kitendo cha uhalifu atakuwa anatenda kosa na atakuhumiwa kifungo cha maisha jela.

Kumpumbaza  
mtu kwa nia ya  
kutenda kosa

221. Mtu yeoyote ambaye, kwa kusudi la kutenda au kurahisisha kutenda kosa au kurahisisha kukimbiza kwa mkosaji baada ya kutenda kosa au kujaribu kutenda kosa, anatoa au anajaribu kutoa dawa yoyote au kitu chochote cha kumtia mtu ubumbuwazi au kumshinda nguvu, atakuwa anatenda kosa na atahukumiwa kifungo cha maisha jela.

Vitendo  
vinavyokusudia  
kusababisha  
madhara  
makubwa au  
kuzuia ukamataji

222. Mtu yeoyote ambaye, kwa kusudi la kumlemaza mtu yeoyote au kumharibu umbo au kumdhoothisha au kumpletea dhara kubwa mtu yoyote au kupinga au kuzuia ukamataji halali au kutiwa kizuijini kwa mtu yeoyote-

- (a) isivyokuwa halali anamjeruhi au anamletea dhara kubwa mtu yeoyote kwa njia yeoyote iwayo;
- (b) isivyokuwa halali anajaribu kwa namna yoyote ile kumpiga

mtu yeyote kwa kitu chochote cha kurusha au au kwa mkuki, upanga, kisu au silaha nyingine ya hatari au ya kushambulia;

- (c) isivyokuwa halali anasababisha kitu chocote chenye kulipuka kuweza kulipuka;
- (d) anapeleka au anatoa kitu chochote chenye kulipuka au kitu chochote cha hatari au cha kudhuru kwa mtu yeyote;
- (e) anasababisha kitu chochote kilichorejewa katika aya ya (a) kichukuliwe au kupokelewa na mtu yeyote;
- (f) anaweka kitu chochote cha majimaji chenye kuleta uharibifu au cha kuangamiza au kulipuka mahali popote; au
- (g) isivyokuwa halali anammiminia au anamtupia mtu yeyote majimaji au kitu chochote likichorejewa katika aya ya (f) au vinginevyo anatumia majimaji hayo au kitu hicho katika mwili wa mtu mwingine;

atakuwa anatenda kosa na atahukumiwa kifungo cha maisha jela.

Kumiliki viungo  
vyo binadamu  
Sheria Na. 9 ya  
2002 Jedwali

**223**   Mtu yeyote ambaye bila ya halali-

Kumzuia mtu  
kujiokoa katika  
chombo

- (a) anamzuia au anamkinga mtu yeyote ambaye yumo ndani ya chombo, au anakimbia kutoka kwenye chombo (au meli) ambacho kimo hatarini au kinataka kuzama, katika jitihada za kuokoa maisha yake; au
- (b) anamzuia mtu mwingine yeyote ambaye anajitahidi kuokoa maisha ya mtu yeyote katika mazingira yaliyotajwa kwenye aya ya (a),

atakuwa anatenda kosa na atahukumiwa kifungo cha maisha jela.

Kuhatarisha  
usalama wa watu  
wanaosafiri kwa  
njia ya reli.  
Sheria Na. 47 ya  
1954 kif; 3

**224.-**(1) Mtu yeyote ambaye , anakusudia kumjeruhi au kuhatarisha usalama wa mtu yeyote anayesafiri kwa njia ya reli yoyote iwe ni mtu mahsusui au la-

- (a) anaweka kitu chochote kwenye reli hiyo;
- (b) anashughulika na reli hiyo, au na kitu chochote kilichoko kwenye reli hiyo au karibu na reli hiyo kwa namna ambayo itadhuru au kuhatarisha matumizi huru na salama ya reli hiyo au usalama wa mtu huyo;
- (c) analipua au anarusha kitu kwenye reli au ansababisha kitu chochote kugusana na mtu yeyote au kitu chochote katika reli hiyo;
- (d) anaonyesha mwangaza wowote au ishara yoyote au kwa vyovyote anajihuisha na taa au ishara yoyote iliyopo kwenye reli hiyo au iliyopo karibu nayo; au
- (e) kwa kuacha kutenda kitendo chochote ambacho anao wajibu wa kikitenda, anahatarisha usalama wa mtu yeyote,

atakuwa anatenda kosa na atahukumiwa kifungo cha maisha jela.

(2) Mtu ambaye , bila ya halali, lakini bila kusudio lililoelevwa na kifungu cha (1) anasababisha usalama wa mtu yeyote anayesafiri kwa reli kuwa hatarini atakuwa anatenda kosa.

Dhara kubwa

**225** Mtu yeyote ambaye bila ya halali anasababisha dhara kubwa kwa mtu mwingine, atakuwa anatenda kosa na atahukumiwa kifungo cha miaka saba.

Kujaribu  
kujeruhi kwa kitu  
kinacholipuka

**226.** Mtu ambaye bila ya halali, na kwa kusudi la kusababisha dhara kwa mtu mwingine, anaweka kitu chochote chenye kulipuka mahali popote, atakuwa anatenda kosa na atahukumiwa kifungo cha miaka kumi na nne jela.

Kuweka sumu  
kwa nia mbaya  
kwa kusudi la  
kudhuru

**227** Mtu ambaye bila ya halali na kwa kusudi la kumdhuru au kumuudhi mtu mwingine, anasababisha sumu au kitu chochote chenye sumu kupewa mtu au kuliwa na mtu yeyote na hivyo kuhahatarisha maisha yake au kumpa dhara kubwa, atakuwa anatenda kosa na atahukumiwa kifungo cha miaka kumi na nne jela.

- Kujeruhi na matendo yanayofanana na hayo  
Sheria . Na. 5 ya 1961 kif;8
- 228** Mtu yeyote ambaye
- (a) isivyo halali anamjeruhi mwingine ; au
  - (b) isivyo halali, na kwa kusudi la kumjeruhi au kumuudhi mtu yeyote, anasababisha sumu yeyote au kitu kingine chenye kudhuru kupewe mtu mwingine au kuliwa na mtu mwingine

atakuwa anatenda kosa na atahukumiwa kifungo cha miaka mitatu.

- Kushindwa kutoa mahitaji ya muhimu
- 229.** Mtu yeyote ambaye, amepewa wajibu wa kutoa mahitaji ya lazima ya maisha ya mtu mwingine na bila sababu ya msingi anashindwa kufanya hivyo, ambapo anasababisha maisha ya mtu mwingine huyo kuwa hatarini au huenda yakawa hatarini au afya yake kudhurika au huenda ikadhirika daima, atakuwa anatenda kosa na atahukumiwa kifungo cha miaka mitatu jela.

- Wajibu kwa wanaofanya upasuaji wa kitabibu.
- 230.** Mtu yeyote hana hatia ya kosa la jinai kwa kutenda, kwa nia njema na kwa uangalifu wa kufaa na ustadi, upasuaji kwa mtu yeyote kwa faida ya mtu huyo au kwa mtoto ambaye hajazaliwa kwa ajili ya maisha ya mama kama kufanyika kwa upasuaji huo ni wa kufaa, kwa kutilia maanani hali ya mgonjwa huyo kwa wakati huo na mazingira yote yanayosika na hali hiyo.

- Wajibu wa kijinai kwa kwa kutumia nguvu zaidi
- 231.** Mtu yeyote anayeruhusiwa kisheria au kwa idhini ya mtu aliyejeruhiwa naye kutumia nguvu atawajibika kijinai kwa nguvu yoyote itakayopita kiasi kutokana na namna na na jinsi ya kitendo hicho kilicholeta utumiaji wa nguvu iliyopita kiasi.

- Madhara ya ridhaa ya mhanga katika wajibu wa kijinai aliyeruhusu kuuwawa kwake au kulemazwa.
- 232.** Bila kujali chochote katika kifungu cha 231 idhini ya mtu kwa ajili ya kusababisha kifo chake mwenyewe au kulemazwa kwake mwenyewe haitamtoa mtu yeyote katika jukumu la jinai, mtu ambaye amesababisha kifo hicho au ulemavu huo.

### SURA YA ISHIRINI NA NNE JINAI KWA KUTOJALI NA KUPUUZA

- Vitendo vya kupuuza na uzembe
- 233.** Mtu yeyote ambaye kwa namna ya kutokuwa mwangalifu au kupuuza kwa kiasi cha kuhatarisha maisha ya binadamu au kusababisha dhara kwa mtu mwingine yeyote:-

- (a) anaendesha gari lolote , balskeli au piki piki katika barabara yoyote ya umma; au
- (b) anaendesha au kushiriki katika kuendesha au kufanya kazi katika meli yoyote; au
- (c) anafanya kitendo chochote kwa kutumia moto au kitu chochote kiwezacho kuwaka au kuacha kuchukuwa tahadhari dhidi ya hatari yoyote ambao inaweza kutokea kutokana na moto wowote au kitu chochote anachomiliki ambacho kinaweza kuwaka;
- (d) anaacha kuchukuwa tahadhari dhidi ya hatari yoyote ambayo inaweza kutokea kutokana na mnyama yoyote anayemmiliki; au
- (e) anatoa matibabu ya dawa au ya upasuaji kwa mtu yeyote ambaye amediriki kumtibu; au
- (f) anachanganya, anasambaza, anauza anasimamia au anatoa dawa yoyote au sumu au kitu cha hatari; au
- (g) anatenda kitendo chochote, au anaacha kuchukuwa tahadhari ya kutosha dhidi ya hatari yoyote kutokana na mashine yoyote ambayo iko chini yake au sehemu ya mashine hiyo iko chini ya uangalizi wake ; au
- (h) anatenda kitendo chochote, au anaacha kuchukuwa tahadhari ya kutosha dhidi ya hatari yoyote inayoweza kutokea kutokana na kitu chochote cha mlipuko kilichoko chini yake,  
atakuwa anatenda kosa.

Vitendo vingine  
vya uzembe  
vinavyosababisha  
madhara

**234.** Mtu yeyote bila ya halali anatenda tendo lolote, au anaacha kutenda kitendo chochote ambacho ni wajibu wake, kutenda kitendo ambacho sicho kilichotajwa na kifungu cha 233, ambacho utendekaji wake au kutotenda kwake madhara yanababishwa kwa mtu yeyote, atakuwa na hatia ya kosa na atahukumiwa kifungo cha miezi sita.

Kushika vitu vya  
sumu kwa  
uzembe

**235.** Yeyote anayefanya, kwa kutumia kitu chochote chenye sumu, kitendo chochote katika namna ya kutokuwa mwangalifu au kwa uzembe kiasi cha kuhatarisha maisha ya binadamu, au cha kuweza kusababisha maumivu au majeraha kwa mtu mwagine yeyote, au kwa kujua au kwa uzembe kuacha kuwa mwangalifu na kitu chochote chenye sumu anachomiliki kama ilivyo muhimu katika kulinda hatari ambayo inaweza kutokea kwa maisha ya binadamu kutokana na kitu chenye sumu, atakuwa anatenda kosa na atahukumiwa kifungo cha miezi sita au faini ya shilingi elfu mbili.

Kimeachwa

**236.** [Kimenakiliwa kama kifungu cha 224(2).]

Maonyesho ya  
taa za uongo,  
alamu au boyu

**237.** Mtu yejote ambaye anaonyesha taa ya uongo, alamu au boyu, akikusudia au akijua kwamba muonekano wake unaweza kumpoteza nahodha, atakuwa anatenda kosa na atahukumiwa kifungu cha miaka saba .

Kumsafirisha  
mtu kwa kwa  
njia ya majini  
kwa kukodi  
katika chombo  
kisicho salama au  
kilichojaa

**238.** Mtu yejote ambaye kwa hali ya kujua au kuzembea anamsafirisha au anasababisha kusafirishwa kwa kukodi mtu yejote kwa njia ya majini kwenye meli, wakati meli hiyo iko katika hali ambayo au imesheheni kiasi kwamba siyo salama, atakuwa anatenda kosa.

Hatari au  
kizuwizi kwenye  
njia ya umma au  
njia ya meli

**239.** Mtu yejote ambaye, kwa kufanya kitendo chochote au kwa kuacha kuchukua tahadhari ya kutosha kwa mali yoyote anayomiliki au iliyoko chini ya usimamizi wake, akasababisha hatari, kizuwizi au kuumia kwa mtu yejote kwenye njia yoyote ya umma au njia yoyote ya baharini , atakuwa anatenda kosa na atawajibika kutoa faini.

## SURA YA ISHIRINI NA TANO MASHAMBULIO

Shambulio la  
kawaida

**240.** Mtu yejote ambaye bila ya halali anamshambulia mtu mwininge atakuwa anatenda kosa na , iwapo shambulio hilo halikufanyika katika mazingira ambapo adhabu kubwa zaidi imetolewa katika Kanuni hii, atawajibika kwa kifungu cha mwaka mmoja.

Shambulio  
linalosababisha  
madhara ya  
mwili

**241.** Mtu yejote ambaye anafanya shambulio linalosababisha dhara mwilini atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa kifungu cha miaka mitano.

Mashambulio  
kwa watu  
wanaolinda  
chombo

**242.** Mtu yejote ambaye anashambulia na kumpiga au kumjeruhi hakimu yejote, afisa au mtu mwininge aliyepewa mamlaka kihalali, au katika kutimiza wajibu wake au kuhusiana na kulinda meli yoyote iliyoko katika hali ya hatari au meli au bidhaa yoyote kutohana na mavunjiko, kupotea au kuegeshwa ufukweni au majini, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa kifungu cha miaka saba .

Aina nyingine za  
mashambulio

**243. Mtu yelete ambaye-**

- a) anamshambulia mtu mwingine kwa dhamira ya kutenda kosa au anakaidi au kuzuia kukamatwa kihalali au kuzuia yeye mwenyewe au mtu mwingine yelete kwa kosa lolote; au
  - b) anamshambulia, anakaidi au kwa makusudi anamzuia afisa yelete wa polisi wakati anatimiza wajibu wake, au mtu yelete anayemsaidia afisa huyo;
  - c) anamshambulia mtu yelete kufuatia muungano wowote usio halali au njama ili kuinua kima cha mshahara au biashara yoyote, au uzalishaji katika kiwanda au kuhusu mtu yelete anayehusika au aliyeajiriwa humo; au
  - d) anamshambulia, anamzuia au anamkinza mtu yelete aliyeajiriwa kutimiza amri halali aukukamta mali kihalali kwa nia ya kuiokoa mali hiyo yoyote iliyochukuliwa kihalali chini ya mlolongo huo; au
  - e) anamshambulia mtu yelete kwa ajili ya kitendo kilichotendwa na mtu huyo katika kutimiza wajibu wowote aliopewa na sheria,
- atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa kifungo cha miaka mitano.

**SURA YA ISHIRINI NA SITA  
MAKOSA DHIDI YA UHURU WA MTU**

Maana ya kuteka  
nyara kutoka  
Tanzania Bara

- 244. Mtu yelete anayemchukua mtu mwingine nje ya mipaka ya Tanzania Bara bila ya idhini ya mtu huyo, au ya mtu aliyepewa mamlaka kihalali kutoa idhini badala ya mtu huyo, itachukuliwa kuwa ni kumteka mtu huyo kutoka Tanzania Bara.**

Maana ya kuteka  
nyara kutoka kwa  
mlezi halali

- 245. Mtu yelete anayemchukua au anayemshawishi mtu yelete mwenye umri wa chini ya miaka kumi na nne iwapo ni mwanamume au mwenye umri wa chini ya miaka kumi na sita iwapo ni mwanamke, au mtu yelete asiyekuwa na akili timamu, kutoka kwenye uangalizi halali wa mlezi wa mtoto huyo au mtu huyo asiyenye na akili timamu, bila ya idhini ya mlezi huyo, itachukuliwa kuwa ni kumteka nyara mtu huyo kutoka kwenye malezi halali.**

Maana ya  
kutorosha

- 246. Mtu yelete ambaye kwa nguvu au kwa njia zozote za udanganyifu anamlazimisha au anamshawishi mtu yelete kwenda mahali popote itachukuliwa kuwa ni kumtorosha mtu huyo.**

- Adhabu ya kuteka nyara
- 247.** Mtu yeyote ambaye anamteka nyara mtu mwingine yeyote kutoka Tanzania Bara au kutoka kwenye malezi halali atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu kifungo cha miaka saba.
- Kuteka nyara au kutorosha kwa nia ya kuua
- 248.** Mtu yeyote ambaye anamteka nyara au kumtorosha mtu yeyote ili mtu huyo auwawe, au aweze kutupwa ili kuwekwa katika hatari ya kuuwawa, atakuwa anatenda kosa na anawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi
- .
- Kuteka nyara au kutorosha kwa nia ya kufungia
- 249.** Mtu yeyote ambaye anamteka nyara au kumtorosha mtu yeyote kwa dhamira ya kusababisha mtu huyo afungiwe kwa siri na kimakosa, ana hatia ya kosa anawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.
- Kuteka nyara au kutorosha kwa nia ya kujueruhi
- 250.** Mtu yeyote ambaye anamteka au kumtorosha mwingine ili amwache mtu huyo au ili aweze kutupwa katika mazingira ambayo yatamuweka katika hali ya kuweza kuangukia kwenye hatari ya kupata madhara makubwa au utumwa au tamaa mbaya ya mtu yeyote, au akijua kwamba kuna uwezekano mtu huyo akakumbana na mazingira hayo au kuwa katika hali hiyo, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi.
- Kuficha mtu aliyetekwa au kutoroshwa kinyume na sheria
- 251.** Mtu yeyote ambaye, akijua kwamba mtu yeyote ametekwa nyara au ametoroshwa, akamficha au akamfungia mtu huyo kinyume na sheria, atakuwa anatenda kosa na ataadhibiwa kwa namna sawa kana kwamba yeje ndiye aliyemteka au kumpoka mtu huyo kwa dhamira sawa au ufahamu ule ule au madhumuni yale yale, kama aliyokuwa nayo ya kumficha au kumzuia mtu huyo katika kizuizi.
- Kumteka nyara au kumtorosha mtoto kwa nia ya kumuiba
- 252.** Mtu yeyote ambaye anamteka nyara au anamtorosha mtoto yeyote mwenye umri wa chini ya miaka kumi na nne kwa dhamira ya kuiba mali yoyote ya kuhamishika kutoka kwa mtoto huyo, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.
- Adhabu ya kumfungia mtu isivyo halali.
- 253.** Mtu yeyote ambaye anamfungia mtu mwingine kinyume cha sheria atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha mwaka mmoja au faini ya shilingi elfu tatu.

Kumnunua au kumuza mtu yejote kama mtumwa.

**254.** Mtu yejote ambaye anaingiza kutoka nchi za nje, anatuma nje ya nchi, anatoa, ananunua , anauza, au anamtoa mtu yejote kama mtumwa , au anamkubali, anampokea , au anamzuwia mtu yejote kinyume na matakwa yake kama mtumwa, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Mazoea ya kujihusisha na utumwa

**255.** Mtu yejote ambaye ana mazoea ya kuingiza kutoka nchi za nje, kutuma nje ya nchi, kutoa, kununua, kuuza, kufanya biashara ya kusafirisha watu au akujihusisha na watumwa, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi.

Kumlazimisha mtu kufanya kazi isivyo halali.

**256.** Mtu yejote ambaye pasipo halali anamlazimisha mtu yejote kufanya kazi kinyume na matakwa yake, atakuwa anatenda kosa.

*Kigawo cha Tano. – Makosa Yahu Suyo Mali*

SURA YA ISHIRINI NA SABA  
WIZI

Vitu vinavyowezwa kuibwa

**257.-**(1) Kila kitu kisichokuwa na uhai, ambacho ni mali ya mtu yejote na ambacho kinahamishika, kina uwezo wa kuibwa.

(2) Kila kitu kisichokuwa na uhai ambacho ni mali ya mtu yejote na ambacho kina uwezo wa kufanya kihamishike kina uwezo wa kuibwa mara tu kinapokuwa kimehamishika, ingawa kimefanywa kihamishike kwa nia ya kukiiba.

(3) Kila mnyama wa kufugwa , iwe wa kufugwa kwa asili au wa porini, kwa asili , ambaye ni mali ya mtu yejote ana uwezo wa kuweza kuibwa.

(4). Wanyama wa porini kwa asili , wa aina ambayo si kawaida kuonekana kwenye mazingira ya kuwa huru kwa asili Tanzania Bara, amba ni mali ya mtu yejote na amba huwa wanawekwa katika sehemu ya kufungiwa, wanawenza kuibwa, iwe wamefungiwa au wametoroka kutoka kifungoni.

(5) Wanyama wa porini kwa asili, wa aina ambayo si kawaida kuonekana kwenye mazingira ya kuwa huru kwa asili Tanzania Bara, amba ni mali ya mtu yejote, na wana uwezo wa kuweza kuibwa wakati amba wamo kifungoni na wakati wakiwa wanakimbizwa baada ya kotoroka kutoka kifungoni, lakini si katika wakati mwngine wowote.

- Maana ya wizi  
sheria Na. 14 ya  
mwaka 1988  
kif;10
- (6) Mnyama wa porini kwa asili anachukuliwa kuwa katika hali ya kufungiwa ali mradi yukokatika tundu la kumfungia, kizimba, banda, tangi au kwenye uwa mwingine mdogo au pengine amewekwa kwa namna ambayo hawezi kutoroka na kwamba mmiliki anaweza kumpata wakati apendao.
  - (7) Wanyama wa porini wakiwa katika hali ya kufurahia uhuru wao wa asili hawawezi kuibika lakini mizoga yao yaweza kuibika.
  - (8) Kila kitu kilichozaishwa na mnyama au ambacho kinafanya sehemu ya mwili wa mnyama ambaye anaweza kuibwa kitu hicho kinaweza kuibwa

**258.-**(1) Mtu ambaye kwa udanganyifu na bila ya dai la haki anachukua kitu chochote ambacho kina uwezo wa kuibwa, au kwa udanganyifu anabadili matumizi ya mtu yejote tofauti na mmiliki wa jumla au maalum wa kitu chochote chenye uwezo wa kuibwa, atakuwa anaiba kitu hicho.

(2) Mtu yejote ambaye anachukua au anabadilisha kitu chochote ambacho kina uwezo wa kuibwa, anachukuliwa kufanya hivyo kwa udanganyifu iwapo anafanya hivyo akiwa na nia yoyote kati ya hizi, hii ni kusema-

- (a) nia ya la kumnyang'anya kabisa mmiliki wa jumla au maalum wa kitu hicho;
- (b) nia ya kutumia kitu hicho kama rehani au dhamana;
- (c) nia ya kukichukuwa kitu hicho kiasi kwamba wakati wa kukirudisha, ambapo mtu aliyekichukua au kukibadilisha anaweza kushindwa kutekeleza;
- (d) nia ya kukitumia kwa namna ambayo hakiwezi kurejeshwa katika hali kilivyokuwa wakati wa kukichukuwa au kukibadili; au
- (e) ikiwa ni fedha, kusudi la kuzitumia fedha hizo kwa matakwa ya mtu ambaye anachukuwa au anazibadilisha, ingawa anaweza kukusudia baadaye kulipa kiasi hicho cha fedha kwa mmiliki,

na “mmiliki maalum” maana yake ni mtu yejote ambaye anamiliki

kihalali au anatunza au ana maslahi ya kumiliki kitu husika.

(3) Iwapo kitu kilichoibwa kimebadilishwa, haijalishi kama kimechukuliwa kwa madhumuni ya kukibadilisha au labda wakati wa kukibadilisha kilikuwa kinamilikiwa mtu anayekibadilisha au labda mtu huyo anayebadilisha kitu husika anayo hati ya kisheria (**power of attorney**) **kukiiza** au **kukitumia**, au vinginevyo ameruhusiwia kukiiza/kukitumia.

(4.) Iwapo kitu kilichobadilishwa kimepotezwa na mmiliki na kikaonekana na mtu ambaye amekibadilisha, ubadilishaji huo hautachukuliwa kuwa ni udanganyifu iwapo wakati kikibadilishwa mtu aliyechukuwa au aliyebadilisha kitu hicho hamjui mmiliki ni nani na kwa sababu za msingi anaamini kwamba mmiliki hawezi kupatikana.

(5) Mtu hatachukuliwa kwamba amechukuwa kitu isipokuwa kama amekihamisha kitu hicho au amesababisha kitu hicho kihamishike.

Kesi Maalum

**259.**-(1) Iwapo karani au wakala anaweka rehani au anatoa haki ya kuzuiwa kwa mali au nyaraka za kumiliki mali zilizoaminiwa kwake kwa dhumuni la kuuza au vinginevyo kwa kiasi chochote cha fedha ambacho si kikubwa kuliko stahili kutoka kwa mkuu wake wakati wa kuweka rehani hiyo ya kuzuia pamoja na kiasi chochote cha deni la fedha au hawala yoyote au waraka wa ahadi ambaa umekubaliwa au umetolewa naye kwa niaba au kwa ajili ya mkuu wake, mishughuliko hiyo ya bidhaa au hati ya kumiliki haitachukuliwa kuwa ni wizi.

(2) Iwapo mtumishi, kinyume cha amri za mwawake, anachukuwa chakula chochote kilicho mikononi mwake ili kwamba kiweze kupewa mnyama ambaye ni mali ya mwajiri wake au anamilikiwa na mwajiri wake, uchukuaji huo hautachukuliwa kuwa ni wizi.

Fedha n,k  
inayozuiliwa kwa  
maagizo.

**260.** Iwapo mtu , iwe ye ye peke yake au kwa pamoja na mtu mwingine anapokea fedha yoyote au dhamana ya kitu chochote cha thamani au hati ya wakala wa kisheria kwa ajili ya kuuza, kuweka rahani au kwa ajili ya kuisarifu mali yoyote, iwe ya kuweza kuibika au la, kwa maagizo yoyote iwavyo kwamba fedha hiyo au sehemu yoyote ya fedha hiyo, au fedha nyingine yoyote iliyopokelewa kwa kubadilishana na mali hiyo au sehemu yoyote ya fedha hiyo, au pato au sehemu yoyote ya pato la dhamana hiyo au rahani hiyo itatumika kwa dhumuni lolote au kulipwa kwa mtu yeyote aliyetajwa kwenye maagizo hayo, fedha hiyo au mapato hayo yatachukuliwa kuwa ni mali ya mtu ambaye fedha au dhamana au hati hiyo ya wakala vimechukuliwa kwake mpaka maagizo hayo yatakapokuwa yametekelezwa.

Fedha n.k.  
zinazopokelewa na  
wakala kutokana na  
mauzo

**261.** Iwapo mtu, awe peke yake au na kwa pamoja na mtu mwingine, anapokea mali yoyote kutoka kwa mtu mwingine kwa masharti ambayo yanamruhusu au yanamtaka auze au asarifu vingine, na kumtaka ailipe au atengeneze mapato hayo, au kukikabidhisha kitu chochote kilichopatikana badala ya mali hiyo kwa yule mtu ambaye mali hiyo ilipokelewa kutoka kwake, mpaka viwe vimesarifiwa kwa kufuata yale masharti ambayo mali hiyo ilipokewa, ila iwapo ni sehemu mojawapo ya masharti hayo kwamba hayo mapato, kama yapo, yatafanya kitu kimojawapo kwenye orodha ya hesabu ya mdai na mdaiwa kati yake na huyo mtu ambaye anapaswa kumlipa mapato hayo au kumtolea sababu ya mapato hayo na kwamba uhusiano wa mdai na mdaiwa kati yake huyo mtu ambaye anapaswa kumlipa mapato hayo au kumtolea sababu ya mapato hayo na kwamba uhusiano wa mdai na mdaiwa kati yao utakuwapo tu kwa kuhusu kitu kimojawapo.

Fedha  
inayopokelewa kwa  
niaba ya mwengine

**262.** Iwapo mtu, awe peke yake au kwa pamoja na mwingine, anapokea fedha yoyote kwa niaba ya mwingine, fedha hiyo itahesabiwa kuwa ni mali mtu huyo aliyepokelewa kwa niaba, isipokuwa kama fedha hiyo imepokelewa kwa masharti kwamba iwekwe katika orodha ya kwenye akaunti ya mdai na mdaiwa, na kwamba mahusiano ya mdai na mdaiwa yatakuwepo kati ya watu hao.

Wizi wa watu wenye  
masilahi katika kitu  
kilichoibiwa

**263.** Iwapo mtu yejote anachukua au anabadilisha kitu chochote ambacho kina uwezo wa kuibiwa, katika mazingira ambayo vinginevyo inaweza kuwa ni wizi haijalishi kama mtu huyo anayo mali maalum au ana maslahi katika kitu hicho, au yeje ndiye mmiliki wa hicho kitu kilichochukuliwa au kubadilishwa kufuatana na mali maalum au masilahi ya mtu mwingine yaliyomo katika kitu hicho au kwamba ni mkodishaji wa kitu hicho, kwamba yeje ni mmoja kati ya wamiliki wawili kwa pamoja au zaidi wa kitu hicho au kwamba ni mkurugenzi au afisa wa shirika au kampuni au jumuiya anayomiliki.

Mume na mke  
Sheria Na. 5 ya  
mwaka 1971 Jedwali  
la Pili

**264.** Ili kuondoa mashaka, inatangazwa hapa kuwa mume anaweza kuwa na hatia kwa kumuibia mke wake au mke kwa kumuibia mumewe.

Adhabu ya jumla ya  
wizi.  
Sheria Na. 49 ya  
mwaka 1955  
kifungu cha 10;  
Sheria Na2 ya  
mwaka 1972 Jedwali

**265.** Mtu yejote ambaye anaiba kitu chochote ambacho kina uwezo wa kuibiwa ana hatia ya wizi, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba isipokuwa kwa kuangalia mazingira ya wizi au asili ya kitu kilichoibiwa, adhabu nytingine itatolewa.

Kuiba wosia

**266.** Iwapo kitu kilichoibiwa ni waraka wa wosia, iwe mtoawosia huo yupo hai au amefariki, mkosaji huyo atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi.

Kimefutwa.

**267.** [Kimefutwa na Sheria Na. 13 ya mwaka 1994 kifungu cha 63.]

Kuiba wanyama fulani

**268.** (1) Iwapo kitu kilichoibiwa ni mnyama yeyote ambapo kifungu hiki kinatumika mkosaji atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na tano.

(2) Pale ambapo mtu yeyote anamuua mnyama yeyote ambapo kifungu hiki kinatumika kwa kusudi la kuiba ngozi ya mnyama huyo au mzoga wake au sehemu yeyote ya ngozi au mzoga wake kutokana na kifungu cha 265 na kifungu hiki, atachukuliwa kuwa ameiba mnyama huyo na atawajibika kufunguliwa mashtaka dhidi yake na kuadhibiwa ipasavyo.

(3) Kifungu hiki kinatumika kwa wanyama kama farasi, maksai, punda, nyumbu, ngamia, mbuni, ng'ombe, kondoo, mbuzi au nguruwe.

Kumuibia mtu, n.k  
Sheria Na. 49 ya  
1955 kifungu cha  
11;  
Sheria Na. 2 ya  
mwaka 1972  
Jedwali.

**269.** Iwapo wizi umefanyika kati ya mazingira yafuatayo, hiyo ni kusema iwapo—

- (a) kitu hicho kimeibiwa kutoka kwa mtu mwingine;
- (b) kitu hicho kimeibiwa kwenye nyumba ya kuishi watu, na thamani yake inazidi shilingi mia moja au huyo mkosaji wakati ya kuiba au mara moja kabla na baada ya kuiba anatumia au anatishia kutumia nguvu kwa mtu yeyote ndani ya nyumba hiyo;
- (c) kitu hicho kimeibiwa kutoka kwenye chombo chochote cha majini au gari au sehemu yoyote ya kuhifadhi vitu;
- (d) kitu kilichoibiwa kimeunganishwa na reli au ni sehemu ya reli;
- (e) (Imefutwa.Sheria No 49 ya 1955 kifungu cha11)
- (f) Mkosaji,ili aweze kutenda kosa, anafungua chumba chochote kilichofungwa kwa kufuli, sanduku au chombo kingine cha kuweke vitu kwa ufunguo au kwa kitu kingine, mkosaji atawajibika kwa kifungo cha miaka kumi.

**270.** Iwapo mkosaji ni mtumishi wa Serikali na hicho kitu kilichoibiwa ni mali ya Jamhuri, au kilikuja kumilikiwa na mkosaji huyo kutokana na ajira yake, atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne.

Wizi wa watu  
waliopo katika  
utumishi wa umma  
R.L. Sura ya 500  
kifungu cha 2  
Sheria Na. 2 ya  
mwaka 1972 Jedwali

Wizi wa makarani  
na watumishi.  
Sheria Na. 2 ya  
mwaka 1972 Jedwali

**271.** Iwapo mkosaji ni karani au mtumishi wa umma, na kitu kilichoibiwa ni mali ya tajiri yake, au kilikuja kumilikiwa na mkosaji kutoka kwa mwajiri wake, atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi.

Wizi wa  
wakurugenzi au  
maafisa wa  
makampuni  
Sheria Na. 2 ya  
mwaka 1972 Jedwali

Wizi wa mawakala,  
n.k  
Sheria Na 2 ya  
mwaka 1972 Jedwali

**272.** Iwapo mkosaji ni mkurugenzi au afisa wa shirika au kampuni, na kitu kilichoibiwa ni mali ya shirika hilo au kampuni hiyo atawajibika kwa kifungo cha miaka kumi na nne.

**273.** Iwapo kitu kilichoibiwa ni kimojawapo kati ya vitu hivi vifuatavyo, ndio kusema –

- (a) mali ambayo imepokelewa na mkosaji yenyе wakala wa kuisarifu;
- (b) mali iliyoaminishwa kwa mkosaji, iwe peke yake au kwa pamoja na mtu mwengine yeyote kwa ajili yake, kuiweka katika ulinzi salama au kuitumia, kulipa au kuitoa yote au sehemu yoyote ya mali hiyo au mapato yoyote ya mali hiyo kwa dhumuni lolote au kwa mtu yeyote;
- (c) mali ambayo imepokelewa na mkosaji, iwe peke yake au kwa pamoja na mtu mwengine yeyote kwa ajili yake, au kwa ajili ya mtu mwengine yeyote;
- (d) mapato yote au sehemu ya mapato yanayotokana na dhamana yoyote yenyе thamani ambayo yamepokelewa na mkosaji kwa maagizo kwamba mapato ya dhamana hiyo yatatumika kwa dhumuni lolote au kulipwa kwa mtu yeyote aliyetajwa kwenye maagizo ;
- (e) mapato yote au sehemu ya mapato yatokanayo na kusarifiwa kwa mali yoyote, ambayo yamepokelewa na mkosaji kutokana na kuwa na uwakala wa kuisarifu mali hiyo, uwakala huo kwa kupokelewa na mkosaji huyo kwa maagizo kwamba mapato hayo yatatumika kwa dhumuni lolote au kulipwa kwa mtu yeyote aliyetajwa kwenye maagizo.

mkosaji atawajibika kifungo cha miaka kumi.

Wizi wa wapangaji  
au wafikiaji

**274.** Iwapo kitu kilichoibiwa ni chombo kisichohamishika au chombo cha kuondosheka ambacho kimekodishwa kwa mkosaji kwa ajili ya kukitumia pamoja na nyumba au mahali pa kufikia, na thamani yake inazidi shilingi mia moja, anawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Kuiba baada ya  
kuhukumiwa  
Sheria Na.2 ya  
mwaka 1972 Jedwali

**275.** Iwapo mkosaji, kabla ya kufanya wizi, alikuwa amehukumiwa kwa wizi chini ya kifungu cha 265 atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne.

SURA YA ISHIRINI NA NANE  
MAKOSA YALIYO SAWA NA WIZI

Kuficha madaftari  
ya kumbukumbu

**276.** Mtu yeyote ambaye, kwa kusudi la kudanganya, anaficha au anachukuwa sehemu inayohifadhiwa daftari lenye rekodi ambalo linaruhusiwa au linahitajika kisheria kuhifadhiwa kwa ajili ya uthibitisho au kuweka kumbukumbu ya hati ya kumiliki mali yoyote, au kuweka kumbukumbu za kuzaliwa, ubatizo, ndoa, vifo au mazishi au kuificha au kutoa nakala ya sehemu ya daftari lenye rekodi ambalo linahitajika kisheria kupelekwa kwenye afisi yoyote ya Serikali, ana hatia ya kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi.

Kuficha wosia

**277.** Mtu yeyote ambaye, kwa kusudi la kudanganya, anaficha wosia wowote, iwe mtoa wosia yuko hai au amefariki, ana hatia ya kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi.

Kuficha hati

**278.** Mtu yeyote ambaye, kwa kusudi la kudanganya, anaficha waraka wote au sehemu ya waraka ambayo ni hati ya ushahidi wa kumiliki ardhi yoyote au mali katika ardhi, ana hatia ya kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka mitatu.

Kuua wanyama kwa  
nia ya kuiba  
Sheria Na.31 ya  
mwaka 1972 Jedwali

**279.** Mtu yeyote anayemuwa mnyama yeyote ambaye ana uwezo wa kuweza kuibiwa, tofauti na mnyama ambaye kifungu cha 268 kinatumika, kwa nia ya kuiba ngozi au mzogo wake, au sehemu yoyote ya ngozi yake au mzoga wake, atakuwa na hatia ya kosa na atawajibika akitiwa hatiani kwa adhabu sawa kana kwamba alikuwa amemuiba mnyama huyo.

Kuhamisha kwa nia  
ya kuiba

**280.** Mtu yeyote ambaye anafanya kitu chochote kihamishike kwa kusudi la kukiiba, ana hatia ya kosa na atawajibika kwa adhabu sawa kana kwamba alikuwa amekiiba kitu hicho baada ya kuwa kimehamishika.

Kiudanganyifu kutoa  
bidhaa iliyowekwa  
rehani

**281.-1)** Mtu yeyote ambaye ni mweka rehani wa bidhaa zilizowekwa rehani, iwapo anaondoa au anasarifu bidhaa bila idhini ya muweka rehani, kwa nia ya kudanganya, ana hatia ya kosa.

(2) Katika kifungu hiki neno “bidhaa iliyowekwa rehani” inajumuisha bidhaa yoyote na mali zinazohamishika za aina yoyote, mnyama, watoto wa mnyama na mazao au mimea yoyote, iwe inaota au imechengwa, ambayo kwa wakati uliyopo, kutokana na masharti ya sheria yoyote au chombo chochote kilichoandikwa, kwa ajili ya haki thabiti ya kuzuiwa kwa namna ya dhamana kwa ajili ya deni lolote au wajibu wowote.

kiudanganyifu  
kujihusisha na  
madini ndani ya  
machimbo

**282.** Mtu yeyote ambaye anachukuwa, anaficha au pengine anaondoa mawe yenyewe dhamani, metali au madini yoyote, ndani au karibu na chimbo la madini, kwa nia ya kumlaghai mtu yeyote, ana hatia ya kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka mitano.

Kuchukua madaraka  
kwa udanganyifu

**283.** Mtu yejote ambaye, kwa udanganyifu, anatoa au anachepusha kwa matumizi yake mwenyewe au kwa matumizi ya mtu mwengine yejote, mtambo wowote, nguvu ya mwanga au nguvu ya umeme iliyotoka kwenye mashine, zana za kazi au kitu chochote ambacho ni mali ya mtu mwengine, ana hatia ya kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka mitano.

Kuchukua kusiko  
sababisha wizi  
Sheria No. 14 ya  
mwaka 1980 Kif;11

Kusababisha hasara  
ya fedha au kuharibu  
mali ya mamlaka  
Fulani  
Sheria Na. 1 ya  
mwaka 1993  
Jedwali; 9 ya 2002  
Jedwali.

Sura ya 245

Sura ya .212

**284.** Mtu yejote ambaye, isivyokuwa halali na bila ya haki yoyote, lakini sio kwa kiasi kuwa na hatia ya wizi, anachukua au anajihamishia kwa matumizi yake au kwa matumizi ya mtu mwengine yejote, farasi avutae mizigo au mnyama wa kupanda yejote au gari lolote au baiskeli yoyote ya namna yoyote, au meli yoyote, atakuwa na hatia ya kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miezi sita au faini isiyozidi shilingi elfu moja au adhabu zote kwa pamoja.

**284A.-**(1) Mtu yoyote ambaye, ama ni muajiriwa au sio mwajiriwa wa 'mamlaka iliyotajwa' kwa kitendo chochote cha makusudi au kuacha kufanya kwa uzembe wake au kwa mwenendo mbaya au kwa sababu ya kushindwa kuchukua tahadhari inayotakiwa au kutekeleza wajibu wake katika namna inayotakiwa, akasababisha mamlaka yoyote inayotajwa kupata hasara ya kifedha au kusababisha uharibifu wa mali yoyote inayomilikiwa au inayohodhiwa na mamlaka iliyotajwa na ambapo hasara hiyo ya kifedha au uharibifu ina dhamani ya kifedha isiyopungua shilingi milioni kumi, atakuwa, bila kujali sheria yoyote iliyo kinyume, ametenda kosa na akitiwa hatiani atatoa faini isiyopungua milioni tano au kifungo kisichopungua kipindi cha miaka mitatu au adhabu zote kwa pamoja .

(2) Kwa madhumuni ya kifungu cha (1)–  
"mwajiriwa wa mamlaka iliyotajwa" inajumuisha afisa au mjumbe wa mamlaka iliyotajwa aidha ni muajiriwa au si muajiriwa wa mamlaka hiyo na neno "mwajiri" litatsfsiriwa ipaswavyo;  
"mamlaka iliyotajwa" maana yake ni–

- (a) serikali au Idara ya Serikali katika Jamhuri ya Muungano;
- (b) serikali ya mitaa;
- (c) wakala wa utendaji ilijoanzishwa chini ya Sheria ya Mawakala watendaji ;
- (d) jumuiya ya Afrika Mashariki;
- (e) taasisi zinazojitegemea;
- (f) kampuni yoyote iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni ambapo mamlaka iliyotajwa, inamiliki asilimia yoyote ya mtaji unaotolewa au imeweka dhamana ya kulipa kiasi ikitokea kwamba kampuni inafutwa;
- (g) kijiji ambacho kimesajiliwa chini ya sheria yoyote kwa wakati huo inayohusiana na usajili wa vijiji;
- (h) chama cha ushirika kilichosajiliwa chini ya sheria kwa wakati huo inayohusiana na ushirika.

(3) mamlaka iliyotajwa itakuwa, kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), inachukuliwa kuwa imeingia hasara ya kifedha bila kujali-

- (a) kwamba imepokea au ina haki ya kupokea malipo yoyote yatokanayo na hasara chini ya sera ya bima; au
- (b) kwamba imelipwa au ina haki ya kulipwa kutokana na hasara hiyo.

(4) Hakuna mashtaka chini ya kifungu hiki yatakayoanzishwa bila kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka.

(5) Kwa kuepuka wasiwaso inaelezwa hapa kuwa pale ambapo mtu anashtakiwa kwa kuiba kitu chochote au kwa kosa lingine lolote chini ya kifungu chochote cha Kanuni hii ameachiwa huru, bado anaweza kufunguliwa mashtaka na kushtakiwa upya baadaye kwa kosa ambalo liko chini ya kifungu hiki pale tu iwapo shtaka lililofuatia chini ya kifungu hiki linatokana na vitendo au kuacha kutenda kunakohusiana na vile vitendo ambavyo vilitokana na mashitaka yaliyopita.

(6) Pale ambapo mahakama inamhukumu mtu kwa kosa chini ya kifungu hiki, mahakama itamuamuru mtu huyo kuilipa mamlaka iliyotajwa fidia isiyozidi kiasi cha hasara ilijoitokeza kwa mamlaka iliyotajwa na katika kutathmini fidia mahakama itazingatia mambo ya kupunguzia ukubwa wa kosa itakayodhania yanafaa.

(7) Pale ambapo amri imetolewa chini ya kifungu kidogo cha (6) mamlaka iliyotajwa ambayo amri imetolewa kwa faida yake inaweza kufaili kopi ya amri iliyoidhinishwa kwenye mahakama ya wilaya yenye mamlaka kisheria ya eneo husika zaidi ya mahakama yenye mamlaka kisheria iliyotoa amri hiyo, na baada ya kufaili amri hiyo itachukuliwa kuwa hukumu iliyotolewa na mahakama hiyo ya wilaya inaweza kutekelezwa kwa namna sawa kana kwamba ilikuwa ni hukumu iliyopitishwa chini ya vifungu vya Kanuni ya Kesi za Madai, na mahakama ya wilaya itakuwa na mamlaka ya kutekeleza hukumu hiyo bila kujali kwamba kiasi cha fidia kilichotolewa kinazidi kile cha mamlaka ya kifedha.

Sura ya 33

## SURAYA ISHIRINI NA TISA UNYANG'ANYI NA KUPORA KWA NGUVU

Tafsiri ya  
unyang'anyi

**285.** Mtu yeyote ambaye anaiba kitu chochote, na wakati huo huo au kabla ya au mara baada ya kuiba kitu hicho, anatumia au anatishia kutumia nguvu halisi kwa mtu yeyote au mali yoyote ili akipate au akizuwie kitu hicho alichokiiba au kuzuulia au kukinga upinzania dhidi ya uibaji au uzuijiji, atakuwa na hatia ya unyanganyi.

Adhabu ya  
unyang'anyi  
Sheria Na. 2 ya  
mwaka 1972 Jedwali

**286.** Mtu yeyote ambaye anatenda kosa la unyang'anyi atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka ishirini.

na iwapo mkosaji amechukuwa silala yoyote ya hatari au yenyе kudhuru au chombo , au amefuatana na mtu mmoja mwingine, au iwapo, papo hapo au mara tu kabla au mara tu baada ya unyang'anyi huo, anamjeruhi, anampiga, anamgonga au anatumia nguvu yoyote kwa mtu yeyote, atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha ikiambatana na au bila kuambatana na adhabu ya viboko.

Kujaribu kuiba  
Sheria Na. 2 ya  
mwaka 1972  
Jedwali; 10 ya  
mwaka 1989 Jedwali

**287.** (1) Mtu yeyote ambaye anamshambulia mtu mwingine kwa kusudi la kuiba kitu chochote, na papo hapo, au mara tu kabla au mara tu baada ya shambulio hilo, anatumia au anatishia kutumia nguvu halisi kwa mtu yeyote au mali yoyote ili akipate hicho kitu kilichokusudiwa kuibiwa au anazuwia au anakinga kuzuia kitu hicho kisiibiwe, ana hatia ya kosa na anawajibika kwa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka saba na kisichozidi miaka ishirini, pamoja na adhabu ya viboko.

(2) Iwapo mkosaji amechukuwa silaha yoyote ya hatari au yenyе kudhuru au chombo chochote cha kudhuru, au amefuatana na mtu mwingine au , au iwapo papo hapo au mara tu kabla au mara tu baada ya shambulio hilo, anamjeruhi, anampiga, anamgonga au anatumia nguvu nyingine yoyote ya mwili kwa mtu yeyote, anawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha, lakini, kwa namna yoyote , kifungo kisichopungua miaka kumi na tano pamoja na adhabu ya viboko.

Shambulio kwa nia  
ya kuiba  
Sheria Na. 2 ya  
mwaka 1972  
Jedwali; 10 ya  
mwaka 1989

**288.** Mtu yeyote ambaye anamshambulia mtu mwingine yeyote kwa nia ya kuiba kitu chochote, ana hatia ya kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo kisochopungua miaka mitano na sio zaidi ya miaka kumi na nne, pamoja na adhabu ya viboko.

Kudai mali kwa  
vitisho vya  
maandishi.

**289.** Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kutoza kwa nguvu au kupata chochote kutoka kwa mtu yeyote, na ambaye anajua yaliyomo katika maandishi hayo, anasababisha mtu yeyote kupokea maandishi yoyote yakidai kitu chochote kutoka kwa mtu yeyote bila ya sababu yenyе maana au ya kuminika, maandishi ambayo yana vitisho vya kujeruhi au dhara la aina yoyote kusababishwa kwa mtu yeyote, iwe na mkosaji au na mtu mwingine yeyote, iwapo dai hilo halijatekelezwa, ana hatia ya kosa na anawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne.

Kujaribu kupora  
kwa nguvu na  
vitisho

**290. (1)** Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kupora kwa nguvu au kupata kitu chochote kutoka kwa mtu yeyote—

(a) anamshtaki au anatishia kumshitaki mtu yeyote kwa kutenda kosa au anatoa ushauri wowote au anafanya kitisho chochote kwa mtu yeyote kama kishawishi katika kutenda kosa au kuruhusu utendekaji wa kosa lolote; au

(b) anatishia kwamba mtu yejote atashtakiwa na mtu mwingine yejote kwa kosa, au kushtakiwa kwa kitendo chochote kama hicho; au

(c) kwa kujua yaliyomo ndani ya maandishi, anasababisha mtu yejote kupokea maandishi yoyote yenyenye mashtaka au kitisho kilichorejewa katika kifungu hiki kidogo.

atakuwa anatenda kosa na iwapo shitaka au kitisho cha mashtaka hayo ni kwa –

- (i) kosa ambalo adhabu ya kifo au kifungo cha maisha kinaweza kutolewa;
- (ii) kosa lolote mojawapo la makosa yaliyofafanuliwa katika Sura ya Kumi na Tano, au kujaribu kutenda mojawapo ya makosa hayo;
- (iii) kushambulia kwa kusudi la kujamiihana na mtu yejote kinyume na maumbile, au shambulio lisilo halali na la fedheha kwa mwanamume; au
- (iv) shauri lililotolewa au kitisho kilichofanywa kwa mtu yejote kumshawishi mtu huyo kutenda au kuruhusu kutendeka kwa kosa mojawapo katika makosa yaliyoshatajwa katika aya ndogo za (i) – (iv) za kifungu hiki,

atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne au katika kesi nyingine ambayo haikutajwa katika aya hizo ndogo atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka mitatu.

(2) Haidhuru kama huyo mtu aliyeshtakiwa au aliyetishiwa kushtakiwa ametenda au hakutenda kosa hilo au kitendo hicho ambacho anashtakiwa au anatishiwa kushtakiwa nacho.

Kusababisha  
utekelezaji wa hati,  
n.k . kwa vitisho

**291.** Mtu yejote ambaye, kwa kusudi la kudanganya, na kwa njia yoyote isio halali ya kutumia nguvu, au kwa kumzuia mtu wa mwingine, au kwa njia yoyote ya vitisho kwa kutumia nguvu au kuzuia kutumika kwa mtu wa mwingine, au kwa njia ya kushtaki au kutishia kumshtaki mtu yejote kwa kutenda kosa, au kwa kutoa au kufanya ushauri wowote au kufanya kitisho kwa mtu yejote kumshawishi atende au aruhusu kutendeka kwa kosa lolote, anamlazimisha au anamshawishi mtu yejote –

- (a) kutimiliza, kufanya, kukubali, kutia sahihi, kubadilisha au kuharibu yote au sehemu ya dhamana yoyote yenyenye dhamani ;
- (b) kuandika jina lolote au kutia alama au kubandika muhuri wowote kwenye karatasi au ngozi yoyote ya kuandikia, ili baadaye iweze kufanywa au kugeuzwa au kutumiwa au kutendewa kama kwamba ni dhamana yenyenye dhamani,

atakuwa anatenda kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne.

Kudai mali kwa  
kutishia kwa nia ya  
kuiba

**292.** Mtu yelete ambaye, kwa nia ya kuiba kitu chochote chenye thamani, anadai kitu hicho kwa vitisho na nguvu kutoka kwa mtu mwingine, anatenda kosa na anawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka mitano.

**SURA YA THELATHINI**  
**UVUNJAJI WA NYUMBA USIKU, UVUNJAJI WA NYUMBA MCHANA NA**  
**MAKOSA SAWA NA HAYO**

Tafsiri ya kuvunja  
na kuingia

**293.** (1) Mtu ambaye anavunja sehemu yelete,, iwe nje au ndani ya jengo, au anafungua mlango uliyofungwa, anavuta, anasukuma au anainua, au kwa namna nyingine yoyote, mlango wowote, dirisha, kifungio chochote, kilango cha dari au kitu kingine, ambavyo vimekusudiwa kufunga au kuziba uwazi katika jengo hilo, au uwazi unaotoa njia ya kutoka sehemu moja ya jengo mpaka nyingine, anachukuliwa kuwa amevunja jengo hilo.

(2) Mtu anachukuliwa kuingia ndani ya jengo mara tu ambapo sehemu yoyote ya mwili wake au sehemu yoyote ya chombo chochote alichokitumia kipo ndani ya jengo hilo.

(3) Mtu ambaye ameingia ndani ya jengo kwa njia za kitisho au hilo itumikayo kwa haja hiyo, au kwa kushirikiana kwa hila na mtu yelete aliye ndani ya jengo hilo, au kwa kula njama na mtu yelete aliyeo katika jengo au kwa kupanya katika bomba la kutokea moshi au sehemu jingine la jengo hilo, ambalo daima limekaa wazi kwa mahitaji yoyote ya lazima, lakini kwa kawaida halikukusudiwa kutumika kama njia ya kuingilia, anachukuliwa kwamba amevunja na kuingia ndani ya jengo hilo.

Uvunjaji nyumba  
mchana na uvunjaji  
nyumba usiku.  
Sheria Na. 2 ya  
mwaka 1972 Jedw

**294.** Mtu yelete ambaye—

- (a) anavunja na kuingia jengo lolote, hema au chombo chochote kitumikacho kwa kuishi mwanadamu kwa dhamira ya kutenda kosa humo ndani; au
- (b) ameingia jengo lolote, hema au chombo chochote kitumikacho kwa kuishi wanadamu kwa dhamira ya kutenda kosa humo ndani, au ametenda kosa ndani ya jengo hilo, hema au chombo hicho anavunja na kutoka.

Atakuwa anatenda kosa la uvunjaji nyumba na anawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne.

(2) Iwapo kosa chini ya kifungu hiki limefanyika wakati wa usiku, itakuwa ni uvunjaji wa nyumba wa usiku na mhalifu anawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka ishirini.

Kuingia kwenye  
nyumba ya kuishi  
kwa nia ya kutenda  
kosa.  
Sheria Na. 2 ya  
mwaka 1972 Jedw..

**295.** Mtu yelete ambaye anaingia au yumo ndani ya jengo lolote, hema au chombo chochote kitumikacho kwa kuishi binadamu kwa dhamira ya kutenda kosa humo ndani, ana hatia ya kosa, na anawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na iwapo kosa

hilo limetendeka usiku, atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne.

Kuvunja nyumba na kuingia kwa nia ya kutenda kosa.  
Sheria Na. 50 ya mwaka 1968 Jedw la kwanza; 2 ya mwaka 1972.

Kuvunja nyumba na kuingia kwa nia ya kutenda kosa lolote .  
Sheria Na. 50 ya mwaka 1968 Jedw. ; 2 ya mwaka 1972.Jedw.

Kuchukuwa silaha nk., kwa nia ya kutenda kosa .  
Sheria Na. 2 ya mwaka 1972.

**296. Mtu yejote ambaye-**

- (a) anavunja na kuingia nyumba ambayo ni shule, duka, ghalaa, stoo, karakana, gereji, ofisi au nyumba ya mapato, au jengo ambalo liko jirani na nyumba ya kuishi na ambalo linakaliwa pamoja na nyumba hiyo, lakini si sehemu yake, au jengo lolote ambalo linatumika kama mahali pa kufanyia ibada, na anatenda kosa humo ndani; au;
- (b) baada ya kutenda kosa ndani ya jengo lolote lililotajwa katika aya ya (a) anavunja na kutoka ndani ya jengo hilo; atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi.

**297. Mtu yejote ambaye anavunja na kuingia nyumba ambayo ni shule, duka, ghalaa, stoo, karakana , gereji, ofisi au nyumba ya mapato au jengo ambalo liko jirani na nyumba ya kuishi na ambalo linakaliwa pamoja na nyumba hiyo lakini si sehemu yake, au anavunja na kuingia jengo lolote ambalo linatumika kama mahali pa kufanyia ibada, kwa dhamira ya kutenda kosa humo ndani, atakuwa anatenda kosa , na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne.**

**298. Mtu yejote anayekutwa katika mojawapo ya mazingira yafuatayo, ndio kusema—**

- (a) amechukua silaha au kitu chochote cha hatari au cha kudhuru na amechukua silaha hiyo kwa kusudi la kuvunja au kuingia ndani ya nyumba ya kuishi na kutenda kosa humo ndani;
- (b) amechukua silaha wakati wa usiku, katika nanma iliyotajwa kwenye aya ya (a) kwa kusudi la kuvunja au kuingia ndani ya jengo lolote liwalo, na kutenda kosa humo ndani;
- (c) anamiliki wakati wa usiku bila kuithibitisha uhalali wa kuwa nacho, chombo chochote cha kuvunja nyumba ;
- (d) anamiliki wakati wa mchana chombo chochote cha kuvunja nyumba kwa kusudi la kutenda kosa;
- (e) amevaa kiziba uso au amejitia rangi nyeusi au kwa vinginevyo amejigeuza umbo, kwa kusudi la kutenda kosa; au
- (f) yumo ndani ya jengo lolote liwalo wakati wa mchana au usiku kwa kusudi la kutenda kosa humo ndani;

atakuwa anatenda kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka mitano au, kama alishawahi hukumiwa kabla kwa kosa litokanalo na mali, atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne.

Jinai ya kuingia bila  
idhini R.L. Sura ya  
445; kif 25.

**299. Mtu yelete ambaye—**

- (a) Isivyokuwa halali anaingia ndani ya mali inayomilikiwa na mwingine kwa kusudi la kutenda kosa au kumtisha, kumtukana au kumuudhi mtu yelete mwenye kumiliki mali hiyo; au
- (b) ameingia kwa halali ndani ya mali hiyo na bila ruhusa halali akabaki humo kwa kusudi la kumtishia, kumtukana au kumuudhi mtu anayemiliki mali hiyo au kwa kusudi la kutenda kosa.

atakuwa anatenda kosa la kuingia kwa jinai na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miezi mitatu;  
iwapo mali hiyo ambayo kosa hilo limetendwa ndani yake ni jengo lolote, hema, chombo chochote ambacho kinatumwiwa kama sehemu ya kuishi au jengo lolote ambalo linalotumiwa kama ni mahali pa ibada au kama sehemu ya kuhifadhia mali, mkosaji huyo anawajibika kwa adhabu ya kifungo cha mwaka mmoja.

Kuhodhi  
Sura ya. 500 Kif;12

**300. Iwapo mtu yelete amepatikana na hatia kwa kosa chini ya Sura hii, mahakama inaweza kuamuru kwamba silaha yoyote ya hatari au yenyе kudhuru au chombo chochote cha kuvunjia nyumba ambacho kilichukuliwa au kutumiwa katika kuanganisha kosa vitahodhiwa na Jamhuri ya Muungano.**

**SURA YA THELATHINI NA MOJA  
UDANGANYIFU**

Ufafanuzi wa  
udanganyifu  
Sheria Na. 14 ya  
mwaka 1980  
kifungu cha 13

Kupata bidhaa kwa  
njia ya udanganyifu.  
Sheria Na. 2 ya  
mwaka 1980 Jedw.

Kupata kutekelezwa  
kwa dhamana kwa  
udanganyifu.  
Sheria Na.2 ya  
mwaka 1972

**301. Kitendo cha uwakilishi wowote unaofanywa kwa maneno, maandishi au kwa vitendo, kuhusu jambo fulani, ambapo uwakilishi huo ni kitendo cha uwongo na mtu anayefanya uwakilishi huo anajua kuwa ni wa uwongo au haamini kuwa ni wa kweli, utakuwa ni udanganyifu.**

**302. Mtu yelete ambaye kwa njia ya udanganyifu na kwa nia ya kudanganya, anapata kutoka kwa mtu mwingine yelete kitu chochote ambacho kinawenza kuibiwa, au anamshawishi mtu mwingine yoyote kupeleka kwa mtu yelete kitu chochote ambacho kinawenza kuibiwa, atakuwa anatenda kosa , na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.**

**303. Mtu yelete ambaye, kwa njia yoyote ya udanganyifu, na kwa nia ya kudanganya, anamshawuri mtu yelete kutimiliza, kufanya, kukubali, kusaini, kubadilisha au kuharibu yote au sehemu ya dhamana ya kuthaminika au kuandika jina lolote au kubandika alama au kutia muhuri wowote kwenye karatasi yoyote au karati ya ngozi ambapo baadaye inaweza kufanywa au kugeuzwa au kutumiwa au kutendewa kama kwamba ni dhamana ya thamani, atakuwa anatenda kosa na**

atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Kuhadaa

**304.** Mtu yeyote ambaye, kwa njia yoyote ya hila au ya udanganyifu, anapata kutoka kwa mtu mwingine yeyote kitu chochote ambacho kinaweza kuibiwa au anamshawishi mtu mwingine yeyote kuwasilisha kwa mtu yeyote kitu chochote ambacho kinaweza kuibiwa au kulipa au kuwasilisha kwa mtu yeyote fedha yoyote au bidhaa au kiasi chochote kikubwa cha fedha au idadi kubwa zaidi ya bidhaa kuliko ambavyo angelipa kama isingekuwa hila au mbinu hiyo, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka mitatu.

Kupata mkopo n.k.,  
kwa njia ya uongo.  
Sheria Na. 2 ya  
mwaka 1972

**305.** Mtu yeyote ambaye—

- (a) katika kuijingiza, katika deni lolote au dhima yoyote, anajipatia muamana kwa njia yoyote ya uongo au kwa njia nyingine yoyote ya udanganyifu ; au
- (b) kwa nia ya kuwadanganya wadai wake, anafanya au anasababisha kutolewa zawadi yoyote, kuwasilisha au kuhamisha au tozo yoyote katika mali yake; au
- (c) kwa nia ya kumdanganya yeyote katika wadai wake, anaficha, anaauza au anaondoaa sehemu yeyote ya mali yake baada au ndani ya miezi miwili kabla ya tarehe ya hukumu ambayo hairidhishi au amri yoyote iliyotolewa dhidi yake,

Atakuwa anatenda kosa na anawajibika kwa kwa adhabu ya kifungo cha miaka mitano.

Pale mbapo mali au  
muamana  
umepatikana kwa  
ajili ya mtu  
mwingine. Sheria  
Na.26 ya mwaka  
1971 kif ;4

**305A.** Katika kila uendeshaji mashtaka wa kosa chini ya kifungu cha 302 au kifungu cha 305 cha Kanuni hii, mshitakiwa hatakuwa na haki ya kuachiwa kwa sababu tu kuwa ushihidi uliotolewa umetaja mtu ambaye ananufaika na mali ambayo mshitakiwa amepata au kujaribu kupata, au, kama itakavyokuwa, muamana, alikuwa ni mtu tofauti na mshitakiwa au mtu aliyetajwa kwenye shitaka.

Kula njama kwa nia  
ya kudanganya  
Sheria Na. 2 ya  
mwaka 1972 Jedw.

**306.** Mtu yeyote anayekula njama na mwingine, kwa hadaa au njia yeyote ya udanganyifu na kuidhuru bei ya soko ya kitu chochote kinachouzwa kwa umma, au kudanganya umma au mtu yeyote, awe mtu mahsus au sivyo, au kunyang'anya mali yoyote kwa nguvu kutoka kwa mtu yeyote, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka mitano.

Udanganyifu katika  
kuuza au kuweka  
rehani mali.  
Sheria Na. 2 ya  
mwaka 1972 Jedw.

**307.** Mtu yeyote ambaye, akiwa ni muuzaji au muweka rehani wa mali yoyote, au akiwa ni wakili au wakala wa muuzaji au mweka rahani , kwa nia ya kumshawishi mnunuzi au mwekewa rehani kukubali hati ya kumiliki ambayo imewasilishwa au imetolewa kwake, na kwa kusudi la kudanganya—

(anamficha mnunuzi au mweka rehani kitu chochote cha msingi

kuhusiana na hati ya miliki hiyo au mgogoro wowote;  
(b) anageuza ukweli wa asili ye yeyote ambapo hati inategemea au inaweza kutegemea; au  
(c ) anatoa maelezo yoyote ya uwongo kuhusiana na hati iliyotolewa au anaficha jambo lolote la msingi kwenye hati hiyo, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa kosa la adhabu ya kifungo cha miaka mitano.

Kujifanya kupiga ramli

**308.** Mtu yeyote ambaye, kwa ajili ya pato au bahashishi, anachukua daraka la kupiga ramli, au anajifanya kutokana na ustadi au ujuzi wake wa elimu ya mambo ya mizungu, kugundua mahali au kwa namna ambayo kitu chochote ambacho kimeibiwa au kimepotea kinaweza kuonekana, atakuwa anatenda kosa.

Kujipatia usajili,n.k  
kwa udanganyifu  
Sheria Na. 2 ya  
mwaka 1972 Jedw.

**309.** Mtu yeyote, ambaye kwa kunuwia anajipatia au anajaribu kujipatia au kumpatia mtu mwingine yeyote uandikishaji wowote, leseni au cheti chochote chini ya sheria yoyote kwa udanganyifu, atakuwa anatenda kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka miwili.

Tamko la uwongo ili  
kupata hati ya  
kusafiria

**310.** Mtu yeyote ambaye anatoa maelezo ambayo anajua ni ya uwongo kwa dhumuni la kujipatia hati ya kusafiria, iwe kwa ajili yake mwenyewe au kwa ajili ya mtu mwingine yeyote, atakuwa anatenda kosa .

**SURA YA THELATHINI NA MBILI**  
**KUPOKEA MALI ILIYOIBWA AU ILIYOPATIKANA ISIVYO HALALI**  
**NA MAKOSA KAMA HAYO**

Kupokea mali  
iliyoibiwa au  
iliyopatinaka isivyo  
halali, n.k.  
Sheria Na.. 2 ya  
mwaka  
1972

Watu kusafirisha au  
kumiliki mali  
ambazo zinadhaniwa  
kuibia au  
kupatikana isivyo  
halali.  
Sheria Na. 26 ya  
mwaka 1971  
Kifungu. 5; 14 ya  
mwaka 1980 kif. 14  
Sura ya 20

**311.** (1) Mtu yeyote ambaye anapokea au anahifadhi chombo chochote, fedha, dhamana ya thamani au mali nyingine kama iwayo, huku akijua au akiwa na sababu ya kuamini kwamba mali hiyo imeibiwa, imenyang'anywa, imechukuliwa kimakosa au imepatikana, imebadilishwa au imeuzwa isivyo halali kisheria atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi.

**312.-(1)** Mtu yeyote ambaye–

- (a) amewekwa kizuizini kutokana na utekelezaji wa mamlaka yaliyotolewa na kifungu cha 25 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na amepatikana anamiliki, au anachukua kwa namna yeyote, kitu chochote ambacho kinaweza kutuhumiwa kwamba kimeibiwa au kimepatikana isivyo kuwa halali; au
- (b) amepatikana na afisa polisi akimiliki au akiwa na mamlaka juu ya mali yoyote ambayo inaweza, kwa kuzingatia

mazingira yote, kudhaniwa kuwa imeibiwa au imepatikana isivyokuwa halali,

anaweza kushtakiwa kuwa anamiliki, au anachukuwa, au ana mamlaka juu ya, kama itakavyokuwa, mali ambayo inatuhumiwa kuwa imeibiwa au imepatikana isivyokuwa halali na, kama anashindwa kuiridhisha mahakama kwamba hakuiba au vinginevyo kuipata mali hiyo isivyokuwa halali, atakuwa anatenda kosa ambalo akipatikana na hatia atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha muda usiozidi miaka mitatu.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, “ kujipatia isivyokuwa halali” maana yake ni kujipatia katika mazingira ambayo yanafanya kosa la jinai chini ya sheria yoyote na pia inamaanisha kujipatia-

- (a) kama mapatano ya mauzo, kubadilishana bidhaa au uuzaaji wa mali yoyote iliyopatikana isivyokuwa kihalali; au
- (b) kwa njia ya kununua kwa fedha, yote au sehemu yoyote ya mali ambayo ilipatikana isivyokuwa halali.

(3) Katika mwenendo wa kosa chini ya kifungu hiki-

- (a) mtuhumiwa hatakuwa na haki ya kuachiwa kwa sababu tu ya uhakika kuwa, kwenye ushahidi mbele ya mahakama, angeweza kushitakiwa na, au kuhukumiwa kwa, wizi au kosa lingine la kufanana kutokana na mali hiyo;
- (b) pale ambapo mahakama imeridhika kwamba mshitakiwa alikuwa amewekwa kizuizini na afisa polisi katika kutekeleza wajibu aliopewa chini ya kifungu cha 25 cha Sheria ya Makosa ya Jinai, inaweza kudhaniwa kuwa mali iliyopatikana anamiliki au amehamisha, inaweza kutuhumiwa kuwa mali hiyo iliibiwa au aliipata isivyokuwa kihalali.

(4) Pale ambapo mtuhumiwa amehukumiwa kwa kosa chini ya kifungu hiki kuhusiana na mali yoyote, hatashitakiwa au kuhukumiwa kwa kosa la kuiba au kosa linalofanana na hilo kuhusiana na mali ile ile.

**312A.-**(1) Waziri ambaye, kwa wakati huo ndiye mwenye dhamana ya mambo ya sheria , kwa taarifa iliyochapishwa kwenye *Gazeti*, anaweza kutoa maelekezo kuhusu alama ambazo zinaweza kutumiwa katika vifaa vyovyyote ambavyo viko chini ya udhibiti na ambayo ni mali ya tawi au idara ya Serikali ya Jamhuri wa Muungano.

(2) Mtu ye yoyote ambaye anashitakiwa kwa kuhamisha au kumiliki au kuviveka ndani ya jengo lolote au mahali popote, iwe pa wazi au pamefungwa, vifaa vyoye viliviyotiwa alama hizo kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) ambavyo kimsingi vinaweza kutuhumiwa kuwa vimeibiwa au vimepatikana isivyokuwa kihalali na ambaye anashindwa kutoa maelezo ya kuiridhisha mahakama kuhusu namna gani alivyovipata, atakuwa anatenda kosa.

(3) Mtu ye yoyote anayehamisha au kumiliki au kutunza ndani ya jengo lolote au mahali popote, pawe pako wazi au pamefungwa, vifaa

Kumiliki au kusafirisha vifaa vya umma isivyokuwa halali .  
Sheria Na 32 ya mwaka.1951 kif;2; 10 ya 1959 kifungu cha 5; R.L . Sura ya 455 kifungu cha 26; G.Ns Na . 433 ya 1961; 349 ya 1967 Jedw.

Kumiliki vifaa vya umma au vya idara ya reli isivyokuwa halali

vyovyyote vikiwa ni mali ya Jeshi la Ulinzi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambavyo kimsingi vinaweza kutuhumiwa kuwa vimeibiwa au vimepatikana isivyokuwa halali, na ambaye anashindwa kutoa maelezo ya kuiridhisha mahakama kuhusu namna gani alivyopipata, atakuwa anatenda kosa.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki neno “vifaa’ inajumuisha badhaa zote na vyombo vyote na mali yoyote au kitu chochote kimoja kimoja au sehemu yake, na neno “alama” inajumuisha sehemu yoyote ya alama.

Kupokea bidhaa  
zilizoibowi nje ya  
Tanzania Bara

**313.** Kila mtu ambaye, bila udhuru halali, kwa kujua kitu chochote kitakuwa kimeibiwa au kupatikana isivyokuwa halali kwa njia yoyote iwayo katika mazingira ambayo kama kitendo hicho kingelitendeka Tanzania Bara mtu huyo anayekitenda kitendo hicho angelikuwa na hatia ya kosa, anapokea au anamiliki kitu chochote kilichoibiwa au kilichopatikana nje ya Tanzania Bara, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

**SURA YA THELATHINI NA TATU**  
**UDANGANYIFU WA WADHAMINI NA WATU WALIO KATIKA NAFASI ZA**  
**DHAMANA NA HESABU ZA UWONGO**

Wadhamini kuuza  
mali za muamana  
kwa udanganyifu

**314.** (1) Mtu yeyote ambaye, ni mdhamini wa mali yoyote, na kwa kusudi la kudanganya anaharibu au anaibadilisha mali hiyo kwenye matumizi yoyote ambayo hayaruhusiwi na amana hiyo, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki neno “mdhamini” maana yake ni ni kat i ya watu wafuataao—

- mdhamini ambaye udhamini wake umewekwa kwa mkataba, wosia au hati iliyandikwa, iwe kwa ajili ya umma au kwa ajili ya mtu binafsi au kwa ajili ya msaada;
- mdhamini aliyeteuliwa chini ya mamlaka ya Sheria kwa ajili hiyo;
- mtu ambaye amekabidhiwa wajibu wowote kuhusiana na dhamana yoyote kulingana na kifungu hiki kidogo; au
- wasii na msimamizi wa mirathi.

**315.** Mtu yeyote ambaye—

- akiwa mkurugenzi au afisa wa shirika au kampuni, anapokea au anamiliki mwenyewe mali yoyote ambayo ni ya shirika au kampuni tofauti na malipo ya deni la haki au uhitaji, na kwa nia ya kudanganya, anaacha ama kufanya maingizo yote na ya kweli katika vitabu na katika hesabu za shirika au kampuni, au anaacha kuagiza au kuelekeza maingizo kufanyika;
- akiwa mkurugenzi, afisa au mwanachama wa shirika au

Ubahirifu na  
udanganyifu wa  
wakurugenzi na  
maafisa wa  
mashirika, n.k.  
Sheria Na. 2 ya  
mwaka 1972 Jedw..

kampuni, anatenda mojawapo kati ya vitendo vifuatavyo, kwa dhamira ya kudanganya, ndio kusema—

- (i) anaharibu, anabadili, anachana, au anaghushi kitabu chochote, nyaraka, dhamana yenyе thamani au hesabu yoyote, ambayo ni mali ya shirika au kampuni, au maingizo yoyote katika kitabu chochote, nyaraka au hesabu au anashiriki kwa siri katika kitendo hicho;
- (ii) anafanya au anashiriki kwa siri katika kufanya, maaingizo yoyote ya uongo katika kitabu chochote, nyaraka au hesabu; au
- (iii) anaacha, au anashiriki kwa siri katika kuacha, kuandika habari ndani ya kitabu chochote, nyaraka au hesabu,

atakuwa anatenda kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne.

Maelezo ya uwongo  
ya maafisa wa  
makampuni.

**316.** Mtu yeyote ambaye, akiwa ni muanzishaji, mkurugenzi, afisa au mkaguzi wa mahesabu wa shirika au kampuni, iwe ipo au inakusudiwa kuundwa, anatengeneza, anaeneza au anachapisha, au anashiriki katika kutengeneza , kueneza au kuchapisha maelezo yoyote yaliyoandikwa au hesabu yeyote ambayo, katika maelezo yoyote yaliyomo humo, anajua ni ya uwongo, kwa nia ya kutekeleza mojawapo ya madhumuni yafuatayo—

- (a) kumhadaa au kumdanganya mwanachama yeyote, mwanahisa yeyote au mdai yeyote wa shirika au kampuni , awe mtu fulani au sivyo;
- (b) kumshawishi mtu yeyote, awe mtu fulani au sivyo, ili awe mwanachama wa shirika au kampuni hiyo, au adhaminishe au kukopesha mali yoyote kwenye shirika hilo au kampuni hiyo, au aingie katika dhamana yoyote kwa faida ya shirika au kampuni hiyo,

atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Kugushi au  
udanganyifu wa  
hesabu kwa Karani.  
Sheria Na.2 ya  
mwaka 1972

**317.** Mtu yeyote ambaye, akiwa karani au mtumishi, au akiwa ameajiriwa au anasaidia kazi ya karani au mtumishi, anafanya kati ya vitendo vifuatavyo kwa nia ya kudanganya—

- (a) anaharibu, anabadili, anapasua au anaghushi kitabu chochote, nyaraka yoyote, dhamana yenyе thamani au mahesabu ambayo yako ni mali ya mwajiri au yako chini ya uangalizi wa mwajiri wake, au vimepokelewa na mtu huyo kwa ajili ya mwajiri wake au anaharibu au anabadili maingizo yoyote kwenye kitabu chochote, nyaraka au hesabu au anashiriki kwa siri katika kitendo hicho;
- (b) anafanya au anashiriki kwa siri katika kufanya maingizo ya

- uongo katika kitabu, nyaraka au hesabu; au
- (c) anaacha au anashiriki kwa siri katika kuacha maelezo yoyote husika kutoka kwenye kitabu hicho, nyaraka au hesabu,
- atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne.

Kugushi hesabu kwa mtumishi wa Serikali.  
Sheria Na.2 ya mwaka 1972 Jedw

**318.** Mtu yejote ambaye, akiwa afisa anayehusika na kusimamia kupokea, kutunza au kusimamia sehemu yoyote ya mapato ya umma au mali, kwa kujua kwamba anatoa maelezo yoyote ya uongo au anarudisha pesa yoyote au mali aliyopokea au aliyodhaminiwa aitunze, au kiasi chochote cha pesa kilichopo au mali yoyote anayomiliki au iliyoko chini ya udhibiti wake, atakuwa anatenda kosa na anawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Kuhatarisha usalama wa vyombo vyaa anga.  
Sheria Na. 31 ya 1972 Jedw., 17 ya 1989 Jedw la pili

**SURA YA THELATHINI NA NNE  
MAKOSA DHIDI YA USALAMA WA ANGA**

318A(1) Mtu yejote ambaye-

- (a) anafanya kitendo cha kutumia nguvu dhidi ya mtu aliyeko ndani ya ndege inayoruka kama kitendo hicho kina uwezekano wa kuhatarisha usalama wa ndege hiyo;
- (b) anaharibu ndege wakati wa matengenezo au anasababisha madhara kwenye ndege hiyo ambapo inaifanya ishindwe kuruka au kuna uwezekano wa kuhatarisha usalamawakati wa kuruka ;
- (c) anaweka au anasababisha kuwekwa katika ndege wakati wa matengenezo, kwa njia yoyote iwayo, kifaa au kitu chochote ambacho kina uwezekano wa kuharibu ndege hiyo au kusababisha uharibifu kwenye ndege hiyo au ambayo ingeweza kuifanya ishidwe kuruka au kusababisha madhara kwenye ndege hiyo ambapo kuna uwezekano wa kuhatarisha usalama wakati wa kuruka;
- (d) anaharibu au anasababisha madhara vyombo vyaa kuongozea angani au anaingilia utendaji wa vyombo hivyo, iwapo kitendo chochote kama hicho kina uwezekano wa kuhatarisha usalama wa ndege wakati wa kuruka; au
- (e) anatoa taarifa ambayo anajua ni ya uongo, na kuhatarisha usalama wa ndege kwenye kuruka,
- atakuwa anatenda kosa kosa na anawajibika kuhukumiwa kifungo kisichozidi miaka thelathini pamoja na adhabu ya viboko.
- (2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki-
- (a) ndege itachukuliwa kuwa inaruka katika muda wowote kuanzia pale

ambapo milango yake yote ya nje imefungwa baada ya upandaji mpaka wakati pale mlango wowote ule umefunguliwa kwa ajili ya ushukaji; na ikitokea kuna ulazima wa kutua , kuruka huko kutachukuliwa kuwa kunaendelea mpaka mamlaka zenyenye uwezo zimechukuwa jukumu la ndege hiyo, watu na mali zilizopo ndani ya ndege;

(b) ndege itachukuliwa kuwa iko katika matengenezo kuanzia mwanzo wa maandalizi ya kuruka yanayofanywa na mtumishi wa ardhini au mfanyakazi katika ndege kwa ajili ya ndege husika mpaka masaa ishirini na nne baada ya kutua na kipindi cha kutumika , katika tukio lolote, kitaongezeka kwa kipindi chote wakati ambapo ndege hiyo inaruka kama ilivyofafanuliwa katika aya ya (a) ya kifungu hiki;

(c) kitendo cha nguvu kinajumuisha kitisho chochote cha kutumia nguvu.

(3) Mtu anaweza kushtakiwa kwa kosa chini ya kifungu hiki bila kujali kwamba kosa hilo limetendeka nje ya Tanzania Bara:

Isipokuwa tu pale ambapo kosa limetendeka kuhusiana na ndege iliyosajiliwa Tanzania Bara au inamilikiwa na raia wa Jamhuri ya Muungano mkazi wa kuzaliwa katika Jamhuri ya Muungano au bodi iliyanzishwa na au chini ya sheria , ikijumuisha kampuni iliyanzishwa chini ya Sheria ya Makampuni, mtu hataweza kushtakiwa na kuhukumiwa kwa kosa chini ya kifungu hiki kama alishawahi kushtakiwa na kutiwa hatiani au, kama itakavyokuwa, kuachiwa kwa kosa hilo hilo au kwa kosa linalohusisha jambo hilo hilo ambalo limetendeka, na mahakama au mamlaka yoyote ya mahakama nje ya Tanzania Bara.

(4) Hakuna mtu atashtakiwa kwa kosa chini ya kifungu hiki isipokuwa kwa idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai.

#### *Kigawo cha Sita – Kuharibu Mali kwa Uhsasidi*

### SURA YA THELATHINI NA TANO MAKOSA YANAYOSABABISHA UHARIBIFU WA MALI

Uchomaji wa mali  
kwa makusudi.  
Sheria Na. 2 ya  
mwaka 1972

**319.** Mtu ye yote ambaye, kwa kunuwia na isivyokuwa halali anatia moto katika–

- (a) Jengo lolote lile liwe limekamilika au bado ; au
- (b) chombo chochote kile kiwe kimekamilika au bado; au
- (c) lundiko lolote la mazao ya mboga, au la makaa ya mawe, madini au la kuni; au
- (d) viwanda vya machimbo au matengenezo au zana za machimbo ya madini

atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha.

Kujaribu kuchoma  
mali.  
Sheria Na.2 ya  
mwaka 1972 Jedwali

- 320.** Mtu yeyote ambaye–
- (a) anajaribu isivyokuwa halali kuwasha moto kitu chochote kilichorejewa katika kifungu cha 319; au
  - (b) kwa kunuwia na isivyokuwa halali anatia moto kwenye kitu chochote ambacho kipo karibu na kitu chochote ambacho kimerejewa katika kifungu cha 319 na kuna uwezekano wa kushika moto kutoka hapo.

atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne.

Kutia moto katika  
mazao na mimea  
iotayo

- 321.** Mtu yeyote ambaye kwa kunuwia na isivyokuwa halali anatia moto–

- (a) mazao ya mavuno ya ukulima, yawe mitini, yamechumwa au yamekatwa; au
- (b) mazao ya nyasi za kulisha wanyama zilizolimwa, ziwe za kuota zenyewe au za mazao ya asili ya ardhi hiyo au sivyo, ziwe zimesimama au zimekatwa;

atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne.

Kujaribu kutia moto  
mazao n.k.

- 322.** Mtu yeyote ambaye–

- (a) anajaribu isivyokuwa halali kuwasha moto kitu chochote kama kilichotajwa kwenye kifungu cha 321; au
- (b) kwa kunuwia na isivyokuwa halali anatia moto kitu chochote kilichopo mahali ambapo kitu chochote kilichorejewa katika kifungu cha 321 kina uwezekano wa kushika moto kutoka hapo.

atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa kifungo cha miaka saba.

Kukalibu vyombo  
Sheria Na. 47 ya  
mwaka 1954 kif; 3

- 323.** Mtu yeyote ambaye–

- (a) kwa kunuwia na isivyokuwa halali anakalibu au anaharibu chombo chochote cha majini, kiwe kimekamilika au sivyo;
- (b) kwa kunuwia na isivyokuwa halali anatenda kitendo chochote ambacho mara moja kitasababisha kupotea au kuharibika kwa chombo cha majini wakati wa dhoruba/hatari; au
- (c) kwa kusudi la kukitia chombo hicho hatarini, anaingilia taa yoyote, nguzo ya kuonyesha hatari, boyo, alama au ishara yoyote itumiwayo kwa ajili ya usafiri wa baharini, au kuonyesha taa au ishara yoyote ya uwongo,

atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne.

Kujaribu kukalibu

- 324.** Mtu yeyote ambaye anajaribu, isivyokuwa halali,

vyombo.  
Sheria Na 47 ya  
mwaka 1954 kif;3

kupeperusha au kuharibu chombo cha majini, kiwe kimekamilika au sivyo au isivyokuwa halali kutenda kitendo chochote ambacho mara moja kitapelekea kupotea au kuharibika kwa chombo cha majini kilichomo katika dhoruba/ hali ya hatari, atakuwa anatenda kosa, na atawajibka kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Kujeruhi wanyama

**325.** Mtu ye yeyote ambaye, kwa kunuwia na isivyokuwa halali, anamuwa, anamlemaza au anamjeruhi mnyama ye yeyote ambaye anaweza kuibiwa, atakuwa anatenda kosa.

Adhabu ya kuharibu  
mali kwa makusudi  
Sheria Na. 47 ya  
mwaka 1954  
kifungu cha 3; 5 cha  
mwaka 1961; Sheria  
Na. 65 ya mwaka  
1966 kifungu 8; 2 ya  
mwaka 1972  
Jedwali; 12 ya  
mwaka 1998  
Jedwali.

Sura ya 40

Kazi za ukingo au  
ukuta wa mto usafiri  
wa bahari au  
madaraja

**326.-**(1) Mtu ye yeyote ambaye, kwa kunuwia na isivyokuwa halali anaharibu au anaathiri mali yoyote , atakuwa anatenda kosa, na isipokuwa kama ilivyoelezwa vinginevyo katika kifungu hiki, atawajibka kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

(2) Kama mali husika ni nyumba ya kuishi au chombo cha majini, na madhara yamesababishwa kwa mlipuko wa kitu chochote kinacholipuka, na kama-

- (a) mtu ye yeyote yumo ndani ya nyumba hiyo ya kuishi au chombo hicho; au
- (b) uharibifu huo au hasara hiyo imehatarisha maisha ya mtu ye yeyote,

Mkosaji atawajibka kwa adhabu ya kifungo cha maisha.

(3) ) Kama mali husika-

- (a) ni ukingo au ukuta wa mto, mfereji, mfumbi, birika au maji ya bara, au kazi ihusihayo na majahaba, birika au maji ya bara, na uharibifu huo unasababisha hatari halisi ya mafuriko au hasara kwenye ardhi au jengo lolote;
- (b) ni njia ya reli au daraja, ulalo au mfereji wa maji uliojengwa juu ya barabara, njia ya reli au njia ya maji iliyojimbiliwa, au mali ambayo juu yake yapita njia ya reli, barabara au njia ya maji iliyojimbiliwa, na mali hiyo imeharibika;
- (c) ikiwa ni njia ya reli au daraja lolote, ulalo au mfereji wa maji, umeharibiwa, na uharibifu wenyewe umefanywa kwa nia ya reli hiyo, daraja, ulalo au mfereji wa maji, au barabara inayopita juu au chini yake au kwenye sehemu yoyote ya mali hiyo, iwe kwenye hatari au kushindwa kupidika, na kwa hiyo inafanywa yote au sehemu tu kuwa ya hatari au isiyopitika; au
- (d) ni bomba lililorejewa kwenye Sheria ya Bomba la Tanzania - Zambia na hasara imesababishwa kwa nia ya kuzuia au kupinga matumizi ya bomba hilo,  
atawajibka kwa adhabu ya kifungo cha maisha.

(4) Iwapo mali husika ni waraka wa wosia, iwe mtoa wosia huo

yuko hai au amefariki au daftari la kumbukumbu lililoidhinishwa au kutakiwa na sheria kuwekwa kwa ajili ya kuhakikisha au kuweka kumbukumbu ya hati ya kumiliki mali yoyote, au kuweka kumbukumbu ya vizazi, ubatizo, ndoa, vifo au mazishi, au nakala ya sehemu yoyote ya daftari hiyo ambayo inatakiwa kisheria kupelekwa kwa afisa yeyote wa umma, mkosaji huyo atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne.

(5) Iwapo mali husika ni chombo cha majini kilichomo katika dhoruba au hali ya hatari, kukwama au ni kitu chochote katika chombo hicho , mkosaji huyo atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

(6) Iwapo mali husika ni sehemu yeyote ya njia ya reli, au kazi yoyote ihusikanayo na njia ya reli, mkosaji huyo atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne.

(6A) Iwapo mali husika inatumika au inakusudiwa kutumika kwa kwa ajili ya kutoa huduma muhimu, mkosaji huyo atakuwa na hatia na–

- (a) iwapo kuna uwezekano wa kosa hilo kusababisha tukio la hatari katika maisha ya mwanadamu au kusababisha uharibifu, kuzuia au kuingiliana na huduma nyingine yoyote au katika kutoa huduma hiyo atawajibika kwa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka ishirini na kisichozidi miaka thelathini;
- (b) kama kosa limetendeka katika mazingira ambayo hayatasabisha hatari kwa maisha ya binadamu, atawajibika kwa adhabu ya kifungo kisichozidi kipindi cha miaka kumi na tano na kisichozidi miaka ishirini.

(6B) Katika kifungu hiki, “huduma muhimu” inajumuisha–

- (a) huduma yoyote inayohusiana na kuunganisha, kurusha, kutawanya au kusambaza umeme au mawasiliano ya simu;
- (b) huduma yoyote ya moto;
- (c) huduma yoyote ya mabomba ya maji machafu, shimo la takataka au huduma nyingine ya usafi;
- (d) huduma yoyote ya afya, hospitali au gari la wagonjwa;
- (e) huduma yoyote inayohusiana na utoaji au usambazaji wa maji, gesi au petroli;
- (f) barabara yoyote, reli, daraja, shimo la chini, maegesho ya gari, feri, pantoni, bomba la kutawanya maji au mafuta, uwanja wa ndege, bandari au guda.

(7) Iwapo chombo husika kinatumika kwa dhununi la kuzalishia, kusafirishia au kusambaza umeme, mkosaji atawajibika na–

- (a) iwapo kosa hilo lina uwezekano wa kuhatarisha maisha ya mtu, kifungo cha miaka kumi na nne; au
- (c) katika hali yoyote, kifungo cha miaka saba.

Njia za reli

Mali itumikayo kwa  
kuleta nguvu ya  
umeme

(8) Mtu atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba iwapo mali husika -

- (a) ni chombo cha majini, kiwe kimekamilika au la, kimeharibiwa;
- (b) kama ni chombo, kiwe kimemalizika au la, kimeharibika na uharibifu huo umefanyika kwa nia ya kuharibu au kukifanya kisitumike tena; au
- (c) iwapo ni taa, nguzo, boyo, alama au ishara itumikayo kwa ajili ya usafiri wa bahari, au kwa ajili ya kuwaongoza watu wanaoshughulika na usafiri wa baharini;
- (d) kama ni ukingo au ukuta wa mto, njia ya maji iliyochimpuliwa, mfereji wa maji, birika la maji au maji ya bara, au shughuli inayohusu majahabu, njia ya maji iliyochimpuliwa, mfereji wa maji, birika la maji, au maji ya bara, au ambayo inatumiwa kwa madhumuni ya kupakia au kupakuwa bidhaa; au
- (e) kama ni njia ya reli, au ni daraja, ulalo au mfereji wa maji uliojengwa juu ya barabara, njia ya reli au njia ya maji iliyochimpuliwa, imeharibiwa, na uharibifu huo umefanyika kwa nia ya kuifanya njia ya reli, daraja, ulalo au mfereji wa maji, au barabara ya njia ya reli au njia ya maji iliyochimpuliwa inayopita juu au chini ya sehemu hiyo au penye sehemu yake yoyote iwe yenye hatari au isiyopitika; au
- (f) kama ni kitu chochote kilichomo katika harakati za kutengenezwa, au mashine ya kilimo au ya kuzalisha au mtambo wa kufanya vitu au chombo cha kazi ya mtambo wa kufanya vitu , au mashine au zana zinazotumiwa au zinazokusudiwa kutumiwa kwa ajili ya kufanya kazi yoyote inayohusika na utayarishaji wa mapato yoyote ya kilimo au ufugaji, kimeharibiwa; au
- (g) kama ni kitu chochote kilichorejewa kwenye aya (f), kimeharibiwa na uharibifu huo umefanyika kwa nia ya kuharibu kitu husika au kukifanya kisitumike;
- (h) ni mpini au njia ya machimbo ya madini na uharibifu umefanyika kwa nia ya kuharibu machimbo ya madini au kuzuia ufanyaji wake kazi;
- (i) ni mashine, zana, ala ya kufanya kazi, jengo, ukuta, daraja au barabara inayohusika au inayotumika pamoja na chimbo hilo, iwe kitu husika kimekamilika au sivyo; au
- (j) kama ni kamba, mnyororo au koweko, au zana yoyote iwayo , ambayo inatumika ndani ya chimbo, au kwenye njia yoyote au kazi yoyote inayohusika au inayotumika kwenye chimbo, imeharibiwa; au

- (k) kama ni kitu chochote kilichorejewa kwenye aya (f) kimeharibiwa na uharibifu huo umefanyika kwa nia ya kuharibu kitu hicho husika au kukifanya kisitumike; au
- (l) ni kisima, au bomba la maji, au bwawa, ukingo, ukuta au mlango wa kuzuia maji ya bwawa la kinu , au bwawa.

(9) Iwapo mali husika ni nyaraka ambayo imewekwa amana au imehifadhiwa katika ofisi ya umma, au ambayo ni ushahidi wa kumiliki ardhi yoyote, au kumiliki mali katika ardhi, mkosaji atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

**327.** Mtu yejote ambaye, isivyokuwa halali na kwa kusudi la kuangamiza au kuharibu mali yoyote, anaweka milipuko yoyote mahali popote pawapo, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne.

**328.** Mtu yejote ambaye, kwa kunuwia na isivyokuwa halali anasababisha au anahuksika na kusababisha au anajaribu kusababisha maradhi yoyote ya kuambukiza kwa mnyama yeyote au kati ya mnyama yeyote au wanyama amba wanaweza kuibiwa, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

**329.** Mtu yejote ambaye, kwa kunuwia na isivyokuwa halali na kwa nia ya kudanganya, anaondosha au anafuta kitu chochote au alama ambayo iliyowekwa kihalali kama alama ya mpaka wa ardhi yoyote atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka mitatu.

Kujaribu kuharibu  
mali kwa milipuko

Kusababisha  
wanyama kupata  
magonjwa ya  
kuambukiza

Kuondoa alama za  
mipaka kwa nia ya  
kudanganya

Kimefutwa

Kusababisha  
uharibifu n.k. katika  
kazi za reli

**330.** [Kimefutwa na R.L Sura ya 390 kifungu cha 33.]

**331.** Mtu yejote ambaye-

- (a) kwa kunuwia anaharibu, anadhuru au anazuia kazi, njia, barabara, jengo, langa, mizani ya kupimia, mtambo, gari dogo la kupakizia behewa, bogi kubwa, bogi la wazi, zana au mashine iliyopatikana kwa au kwa ajili ya kazi zozote za reli;
- (b) anang'oa, anaondoaa, anafuta au anaharibu, au kwa vyovyyote, anaingilia boriti zozote, nguzo, bendera, vizingi, mistari, alama zozote au kitu chochote kilichochimbiwa ardini au kilichowekwa juu ya ardhi, miti, mawe au majengo, au mali nyininge yoyote ambayo ni mali ya kazi zozote za reli;
- (c) anafanya kosa la kuweka uchafu wowote au kuingia bila idhini ndani ya ardhi yoyote, majengo au nyumba ambayo vimepatikana kwa au ni mali ya kazi zozote za reli; au
- (d) kwa kunuwia, anamnyanyasa, anamzuwia au anamkinga afisa msimamizi wa reli yoyote au wasaidizi wake au

wafanyakazi wake katika kutimiliza kazi yoyote iliyofanywa au ambayo itafanywa kuhusiana na ujenzi au utunzaji wa reli hiyo,  
atakuwa anatenda kosa na anawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miezi mitatu au fani ya shilingi mia nne.

Vitisho vya  
kuchoma au  
kuharibu

Kuharibu noti za  
benki

Kurusha kishada.  
Sheria Na. 17 ya  
mwaka 1990 Jedw la  
tatu

**332.** Mtu yelete ambaye anapeleka, anawasilisha, anatoa ama kwa dhahiri au kwa siri au anasababisha kupokelewa kwa barua au maandishi yoyote ambayo yanatishia kuunguza au kuharibu nyumba, ghal ya nafaka au jengo jingine, au ghal la majani makavu au rundo la mazao, majani ya kulisha wanyama au majani makavu, au mazao mengine ya kilimo, yawe yamo ndani ama chini ya jengo au la, au chombo chochote ambacho kinatishia kuua, kutia kilema au kuheruhi mifugo yoyote atakuwa anatenda kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

**332A.** Mtu yelete, bila mamlaka, kwa kunuwia anaharibu, anachana, anakata au vinginevyo anachanachana noti yoyote ya benki au fedha ambayo inatumika kihalali, atakuwa anatenda kosa ambalo limo kwenye Jedwali, na atakuhumiwa kutoa faini ya shilingi elfu tano kwa kila noti iliyoharibiwa au, akishindwa adhabu ya kifungo cha mwaka moja.

**332B.-(1)** Kulingana na kifungu kidogo cha (3), mtu yelete ambaye kwa udanganyifu anajipatia faida au fedha ya kiasi chochote kutoka kwa mtu anayefanya kazi benki kwa njia ya kurusha kishada atakuwa anatenda kosa na kwenye hukumu anawajibika kwa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi.

(2) Mtu yelete aliyeajiriwa na benki, kutokana na ofisi yake, kwa njia ya udanganyifu anamsaidia mtu mwingine kupata faida au fedha kiasi chochote kutoka benki kwa njia ya kurusha kishada anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha kipindi kisichozidi miaka kumi.

(3) Mtu atajulikana ni mdanganyifu na anatenda kosa chini ya kifungu hiki kama hundi iliyotolewa na mtu huyo hajaidhinishwa kwa sababu ya kukosa au upungufu wa fedha kwenye akaunti na ndani ya siku nane baada ya kupewa taarifa kuhsusu kutokuidhinishwa kwa hundi hiyo anashindwa au anakataa kuweka akaunti sawa.

(4) Pale ambapo mtu yoyote amehukumiwa kwa kosa chini ya kifungu hiki, mahakama itatoa amri ya kuhodhiwa katika Jamhuri ya Muungano fedha yoyote, bidhaa au mali iliyopatikana wakati wa au baada ya kutenda kosa hilo, pamoja na fidia yote kwa benki kuhsiana na fedha iliyotumika kwenye kurusha kishada.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki neno "kurusha kishada" maana yake ni kujipatia fedha au faida kwa njia ya hundi kwenye akaunti ambayo haina fedha ya kutosha au hakuna fedha kabisa, na kusababisha kukopa akiba isioruhusiwa kwa mwenye benki.

*Kigawo cha Saba. – Kughushi,, Utengenezaji Sarafu,  
Kubuni Sarafu na Makosa sawa na hayo*

## SURA YA THELATHINI NA SITA TAFSIRI

Tafsiri ya kughushi  
Sheria Na.5 ya  
mwaka 1990 Jedw

Ufafanuzi wa  
nyaraka

Utengenezaji wa  
nyaraka ya uwongo.  
Sheria Na. 14 ya  
mwaka 1980 kif;15

Nia ya kudanganya

**333.** Kugushi ni kutengeneza nyaraka ya uwongo kwa nia ya kudanganya au kuhadaa.

**334.** Neno “nyaraka” katika kigawe hiki cha Kanuni hii hakijumuishi chapa ya biashara au alama nyingineyo yoyote ambayo inatumika kwa ajili ya bidhaa za biashara ingawa alama hizo zinaweza kuandikwa au kupigwa chapa.

- 335.** Mtu ye yeyote anayetengeneza nyaraka ya uwongo ambaye–
- (a) anafanya nyaraka ambayo ni ya uwongo au ambayo ana sababu ya kuamini kuwa si ya kweli;
  - (b) anabadili nyaraka bila ya mamlaka kwa namna ambayo iwapo kubadili huko kungekuwa na mamlaka kungebadili matokeo ya nyaraka hiyo;
  - (c) anaingiza katika nyaraka hiyo bila ya mamlaka , wakati nyaraka hiyo inaandikwa, jambo ambalo kama lingeruhusiwa lingebadilisha matokeo ya nyaraka hiyo;
  - (d) anatia sahihi nyaraka –
    - (i) kwa jina la mtu ye yeyote bila ya ruhusa ya mtu huyo, liwe jina hilo ni la yule anayetia sahihi hiyo au silo;
    - (ii) kwa jina la mtu ye yeyote wa kubuniwa ambaye anadhaniwa kwamba yupo, iwe mtu wa kubuniwa huyo anadhaniwa kwamba ni wa jina sawa na aliyetia sahihi hiyo au sivyo;
    - (iii) kwa jina linalofanywa liwe jina la asiyekuwa yule mwenyewe kutia sahihi nyaraka hiyo, na ambalo linakusudiwa likosewe kwa jina la huyo anayetia sahihi;
    - (iv) kwa jina la mtu ambaye mwenye kutia sahihi nyaraka hiyo anajifanya ni yeye isipokuwa kwamba matokeo ya nyaraka hiyo inategemea utambulisho kati ya mtu anayetia sahihi na mtu aliyekubali ni yeye.

**336.** Nia ya kudanganya inadhaniwa kuwepo iwapo inaonekana kwamba wakati ambao nyaraka ya uwongo inatengenezwa kulikuwepo na mtu mahasusi anayejulikana au asiyejulikana ambaye anaweza kudanganya, na kudhaniwa huko hakutakanushwa kwa uthibitisho kwamba mkosaji huyo alichukuwa au alikusudia kuchukua hatua za

kuzuia mtu huyo asidanganywe, wala kwa kuwa alikuwa na haki au alidhani kwamba alikuwa na haki ya hicho kitu ambacho kitapatikana kwa nyaraka hiyo ya uwongo.

### SURA YA THELATHINI NA SABA ADHABU YA KUGHUSHI

Adhabu ya, na  
adhabu ya jumla ya  
kugushi  
Sheria Na. 2 ya  
mwaka 1972 Jedwali

Kughushi ambapo  
adhabu ni kifungo  
cha maisha

Kughushi hati ya  
mahakama au  
nyaraka ya kiofisi

Kughushi ambapo  
adhabu ni kifungo  
cha miaka saba

**337.** Mtu yejote ambaye anagushi nyaraka yoyote atakuwa na hatia ya kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba isipokuwa kwa kizingatia mazingira ya kughushi au aina ya kitu kilichoghushiwa adhabu nyingine imetolewa.

**338.** Mtu yejote ambaye anaghushi wosia wowote, nyaraka ya hati ya kumiliki ardhi, kumbukumbu ya mahakama, hati ya wakala, hati ya benki, noti ya sarafu, hundi, hawala, hati ya bima au hati nyingine ya kuamuru malipo ya fedha inayotolewa na mtu anayefanya biashara kama mwenye benki, atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha na kwa nyongeza mahakama inaweza kuamuru kwamba nyaraka yoyote hiyo ihodhiwe na Jamhuri ya Muungano.

**339.** Mtu yejote ambaye anaghushi hati yoyote ya mahakama au nyaraka ya kiofisi anawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

**340.** -(1) Kwenye kifungu hiki, neno “stampus” maana yake ni stempu inayotumika kwa madhumuni ya mapato au muhuri wa idara yoyote ya Serikali.

(2) Mtu yejote ambaye-

- (a) anaghushi stampu/muhuri wowote uwe wa kugandamiza au wa moto;
- (b) bila ya udhuru wa halali, uthibitisho wa udhuru huo kama upo utakuwa juu yake, anatengeneza au, anajua anamiliki dawa au kifaa chochote ambacho kinaweza kutia muhuri;
- (c) kwa udanganyifu anakata, anabandua kwa namna yoyote, au anaondoa kutoka kwenye kitu chochote stampu yoyote kwa dhamira kwamba stampu hiyo au sehemu ya stempu hiyo itatumika kwa matumizi mengine au;
- (d) kwa udanganyifu, anaharibu stampu yoyote kwa dhamira kwamba stempu hiyo itatumika kwa matumizi mengine au
- (e) kwa udanganyifu, anabandika au anaweka kwenye waraka wowote au kwenye stempu yoyote, stampu au sehemu ya stempu ambayo, ama kwa udanganyifu au sivyo, imekatwa, imechanwa au, kwa njia yoyote imetolewa kutoka kwenye waraka mwingine wowote au imekatwa au imechanwa kutoka stampu nyingine yoyote; au

- (f) kwa udanganyifu anafuta au vinginevyo anaondoa kiukweli au kumuonekano kutoka waraka wowote uliotiwa stampu, jina lolote, hesabu yoyote, tarehe au jambo jingine, au kitu chochote kiwacho ambacho kimeandikwa humo kwa nia kwamba matumizi mengine ya stampu hiyo yatafanywa kwenye waraka huo; au
- (g) kwa hali ya kujuja na bila udhuru wa halali, uthibitisho wa udhuru huo utakuwa juu yake, anamiliki stempu yoyote au sehemu ya stempu ambayo kwa udanganyifu imekatwa, imechanwa au, kwa vingine, imebanduliwa kutoka kwenye waraka wowote, au stempu yoyote ambayo imekatwa kwa udanganyifu, au waraka wowote wenyewe stempu ambapo jina lolote, hesabu yoyote tarehe au jambo jingine au kitu kimefutwa kwa udanganyifu au vinginevyo kiukweli na kiuwazi kimeondolewa,
- atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Kutengeneza au  
kumiliki makaratasi  
au zana za kughushi  
Sura ya 500 kifungu  
cha 36; Sheria Na.  
12 ya mwaka 1966  
Jedw.

**341.** Mtu yejote ambaye bila ya ruhusa au udhuru wa halali na ambaye uthibitisho wa udhuru huo ni juu yake—

- (a) anatengeneza, anatumia au kwa hali ya kujuja anamiliki karatasi yoyote inayokusudiwa kufanana na kupita kama karatasi maalum kama ile iliyotolewa na kutumika kwa kutengenezea noti yoyote au hati ya benki;
- (b) anatengeneza, anatumia au, kwa hali ya kujuja anamiliki, kiunzi chochote, umba, au chombo kwa ajili ya kutengenezea karatasi hiyo, au kwa ajili ya kutengeneza ndani ya au juu ya karatasi hiyo maneno yoyote , tarakimu, herufi, alama, mistari au ishara zozote zilizo mahasusi na zitumikazo ndani au juu ya karatasi yoyote kama hiyo;
- (c) anachora au kwa vingine vyovyote vile anatengeneza maneno yoyote, tarakimu, herufi alama, mistari au ishara yoyote kwenye bamba lolote, ubao, jiwe au kitu chochote kingine, kuchora kwa ukamilifu au kwa baadhi kufanana na maneno yoyote, tarakimu herufi, alama, mistari au ishara zozote zilizo mahasusi na zitumikazo ndani au juu ya hati yoyote ya benki, au ndani au juu ya waraka wowote ambao unampasisha au unamshuhudia mtu yejote kuwa na hisa yoyote au kuwa na masilahi kwenye mali ya Serikali, malipo ya kila mwaka, fedha ya akiba au deni lolote la shirika yoyote, kampuni au chama chochote, kiwe ndani au nje ya Jumuiya ya Madola;
- (d) anatumia, au kwa hali ya kujuja anayo kwenye umiliki wake bamba lolote, ubao, jiwe au kitu kingine ambacho maneno yoyote, tarakimu, herufi, alama, mistari au ishara kama zilivyoelezwa mwanzo zimechorwa juu yake au kwa

vinginevyo vyovyote zimetengenezwa; au

- (e) anatumia au, kwa hali ya kujuu, anayo kwenye umiliki wake, karatasi yoyote ambayo maneno yoyote kama hayo, tarakimu, herufi, alama, mistari au ishara kama hizo zimechapwa juu yake au kwa vinginevyo vyovyote, zimefanywa kama ilivyokwishasemwa;

atakuwa anatenda kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Kutoa nyaraka za uwongo

**342.** Mtu ye yote ambaye, anajua na kwa kudanganyifu anatoa nyaraka ya uwongo atakuwa na hatia ya kosa, na atawajibika kwa adhabu iliyotolewa kutokana na kosa la kugushi kuhusiana na nyaraka hiyo.

Kutoa nyaraka zilizofutwa au zilizomalizika muda

**343.** Mtu ye yote ambaye, kwa kujuu anatoa nyaraka yoyote ambayo, imeamriwa na mamlaka yoyote halali ikataliwe ifutwe au isimamishwe, au ambayo matumizi yake yamemalizika kwa muda wake kupita, au kwa kifo au kwa kutokea tukio lolote linginelo, akaitoa kuwa ni hati ya badala ya hati inayotumika na kufaa, atakuwa na hatia ya kosa, na atawajibika kwa adhabu ile ile, kana kwamba ameghushi hati hiyo.

Kupata utimilizaji wa nyaraka kwa njia ya udanganyifu

**344.** Mtu ye yote ambaye, kwa njia ya udanganyifu na hadaa kuhusu asili, yaliyomo au utumikaji wa nyaraka, anamfanya mtu mw ingine kuitia sahihi au kutekeleza nyaraka hiyo, atakuwa na hatia ya kosa, na atawajibika kwa adhabu ile ile, kama vile amegushi nyaraka hiyo.

Kufuta michanjo katika hundi

**345.** Mtu ye yote ambaye, kwa nia ya kudanganya–  
(a) anaharibu, anaongeza au kubadilisha michanjo kwenye hundi; au  
(b) kwa kujuu anatoa hundi iliyokatwa, michanjo ambayo imeharibiwa, kuongezwa au kubadilishwa na mtu mw ingine,  
atakuwa na hatia ya kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Kutengeneza nyaraka bila mamlaka

**346.** Mtu ye yote ambaye, kwa nia ya kudanganya au kulaghai –  
(a) bila mamlaka halali au udhuru, anatengeneza, anasaini au anatekeleza kwa jina au badala ya mtu mw ingine, iwe kwa upatikanaji au vinginevyo, nyaraka yoyote au maandishi; au  
(b) kwa hali ya kujuu anatoa nyaraka yoyote au maandishi yoyote yaliyotengenezwa, yaliyosainiwa au kutekelezwa na mtu mw ingine,

Atakuwa anatenda kosa , na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Kudai mali kwa nyaraka za wosia zilizoghushowi

**347.** Mtu yeyote ambaye anafanya uwasilishaji wa mali au fedha au malipo yoyote kwake mwenyewe au mtu mwingine yeyote, kutokana na mirathi au barua ya usimamizi iliyotolewa kwenye wosia ulioghushowi, huku akijua kwamba wosia huo umegushiwa, au kutokana na mirathi yoyote au barua ya usimamizi iliyopatikana kwa ushahidi wa uwongo, huku akijua kwamba vimepatikana kwa hali hiyo, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ile ile kana kwamba ameigushi nyaraka hiyo kutokana na kufanya uwasilishaji au malipo.

Kununua noti zilizoghushowi

**348.** Mtu yeyote ambaye, bila mamlaka au udhuru halali, ambapo uthibitisho utakuwa juu yake, ananunua au anapokea kutoka kwa mtu yeyote, au anamiliki noti ya sarafu ya benki iliyoghushowi, iwe imejazwa au haikujazwa, huku akijua imeghushowi atakuwa anatenda kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Kugushi hati za fedha zilipwazo chini ya mamlaka ya umma

**349.** Mtu yeyote ambaye, akiwa ni mtumishi wa umma, huku akijua na kwa nia ya kudanganya, anatengeneza au anawasilisha kwa mtu yeyote hati ya malipo ya fedha yoyote inayolipwa na mamlaka ya umma, kwa kiasi kikubwa au kidogo kuliko kile ambacho huyo mtu anayeandikiwa hati hiyo anapaswa atakuwa anatenda kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Kughushi daftari la kumbukumbu

**350.** Mtu yeyote ambaye, ana usimamizi halisi wa daftari au kumbukumbu yoyote iliyowekwa na mamlaka ya halali, huku akijua, anaruhusu maingizo yoyote ambayo katika kila taarifa muhimu anajua ni ya uwongo, atakuwa anatenda kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Kupeleka shahada za ndoa za uwongo kwa msajili

**351.** Mtu yeyote ambaye, anatia sahihi au anapeleka kwa mtu anayeruhusiwa na sheria kuandikisha ndoa, shahada ya ndoa au nyaraka yoyote inayoonekana kuwa ni shahada ya ndoa, ambayo katika kila taarifa muhimu anajua ni ya uwongo, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Maelezo ya uongo katika daftari la uandikishaji wa vizazi, vifo na ndoa

**352.** Mtu yeyote ambaye, huku akijua na kwa nia ya kutaka kuandikisha ndani ya daftari la vizazi, vifo au ndoa, anatoa maelezo yeyote ya uwongo kuhusu jambo lolote linalotakiwa na sheria kuandikishwa ndani ya daftari lolote hilo, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka mitatu.

**352A.** Mtu yeyote ambaye anatoa au ni mmojawapo katika kutoa–

(a) noti yoyote ambayo inaonekana kuwa ni noti ya fedha ya

- Tanzania; au  
(b) noti yoyote ya benki ambayo inaonekana kuwa noti ya fedha kwa Tanzania ,

tofauti na masharti ya Sheria ya Benki ya Tanzania, atakuwa anatenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha kipindi kisichozidi miaka mitano.

### SURA YA THELATHINI NA NANE MAKOSA YANAYOHUSU SARAFU

Tafsiri C.A. Sura ya 500 kifungu cha .36 . Sheria Na 12 ya mwaka 1966

- 353.** Ndani ya sura hii—  
"sarafu" inajunisha sarafu yoyote iliyosarifiwa katika kiwanda cha kutengeneza sarafu kwa matumizi ya Tanzania, au fedha halali ya Tanzania au kwenye sehemu yeyote ya Jumuiya ya Madola; na sarafu yoyote ya nchi ya kigeni na sarafu ambayo ilitumika kihalali Tanzania au kwenye nchi nyingine na ambayo inaweza kubadilishwa kuwa sarafu halali;  
"sarafu ya bandia" maana yake ni sarafu isiyo halisi lakini inafanana au iliyokusudiwa kufanana au kuishinda sarafu halisi; na inajumuisha sarafu halisi ambayo imetengezwa au imebadilishwa ili iweze kuonekana kuwa ni sarafu ya thamani ya kiwango cha juu.

Kughushi sarafu

- 354.** Mtu yeyote ambaye anatengeneza au anajaribu kutengeneza sarafu yoyote ya bandia atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha.

Matayarisho ya kutengeneza sarafu bandia

- 355.** Mtu yeyote ambaye—  
(a) anachovyea kipande chochote cha metali cha saizi ya kufaa au kutengeneza umbo, kwa kusudi la kukifanya kitengenezwe kwa kugushi kuwa sarafu;  
(b) anatengeneza kipande chochote cha metali cha saizi ya kufaa au kitengeneze umbo kwa nia kwamba kitengenezwe kuwa sarafu ya kughushi au  
(c) bila mamlaka ya kisheria au udhuru, uthibitisho uko juu yake—  
(i) ananunua, anauza, analipa au anasarifu sarafu yoyote kwa thamani ndogo kuliko thamani ipasayo au ionekanayo a, au kusaidia kufanya kitendo hicho;  
(ii) analeta au anapokea akiwa Tanzania sarafu yoyote ya bandia, huku akijua kwamba ni ya bandia;  
(iii) anafanya au anatengeneza, au anaanza au

- (iv) anajitayarisha kufanya au kutengeneza, au anamiliki, au anasarifu muhuri ambao unatumika kufananisha pande zote au upande mmoja wa sarafu au sehemu yoyote ya sarafu, akijua kuwa stempu au umbo hilo litatumika; anafanya au anatengeneza, au anaanza au anajitayarisha kufanya au kutengeneza, au anamiliki, au anasarifu chombo chochote au mali au mashine ambayo inatumika na kukusudiwa itumike kwa ajili ya kutengeneza sarafu yeye ukingo pamoja na alama au tarakimu ambazo zinafanana na zile zilizoko kwenye kingo za sarafu, huku akijua kuwa vyote hivyo vinafanywa na kukusudiwa; au
- (v) anafanya au anatengeneza, au anaanza au anajitayarisha kufanya au kutengenezaa, au anamiliki au anasarifu mtambo wowote wa kuchapisha sarafu au kifaa, zana au mashine ambayo inatumika kwa ajili ya kukatia duwara zisizo na maandishi kutoka kwenye dhahabu, fedha au metali yoyote, huku akijua kwamba mtambo huo, kifaa hicho, zana au mashine hiyo imetumiwa au inakusudiwa kutumiwa kwa ajili ya kutengeneza sarafu yoyote ya kughushi.

Atakuwa ana hatia ya kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha.

Kupunguza sarafu

**356.** Mtu yejote ambaye anajihuisha na sarafu yoyote kwa namna ambayo katika kupunguza uzito wa sarafu hiyo kwa dhamira kwamba iwapo amefanya hivyo inaweza kupita kama sarafu, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Kuyeyusha sarafu  
Sheria Na. 5ya  
mwaka 1990 Jedw

**357.** Mtu yejote ambaye anayeyusha, anavunja au anafuta kwa kupiga muhuri juu yake jina lolote, neno au alama yejote juu ya sarafu inayotumika Tanzania kwa wakati huu, atakuwa anatenda kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka miwili au faini ya shilingi elfu hamsini au adhabu zote kwa pamoja.

Kuzuia na kuharibu  
sarafu iliyoghushiwa  
Sheria Na. 12 ya  
mwaka 1996 Jedw

**358. -(1)** Afisa yejote wa Serikali au meneja wa benki yoyote ambaye anapokea, wakati anatekelza wajibu wake, sarafu yoyote ambayo, ana sababu ya msingi ya kuamini kwamba sarafu hiyo imeghushiwa, ataizua sarafu hiyo na kuipeleka kwa Afisa wa Benki Kuu ya Tanzania aliyeetuwa na Benki kwa dhumuni la kuikata, kuifuta au kuiharibu kwa fidia au bila ya fidia, kama anavyoona inafaa ikiwa

kwa maoni yake ni bandia.

(2) Uamuzi wa Afisa wa Benki Kuu ya Tanzania aliyeteuliwa na Benki kwa dhumi ni kwamba sarafu ni ya bandia, na kwamba fidia itatolewa au kutotolewa utakuwa ni wa mwisho na hakuna mtu atakayekuwa na haki ya kudai, na hakuna kesi au mashtaka yatakayoletwa dhidi ya Benki Kuu ya Tanzania au Serikali kuhusiana na hasara yoyote au uharibifu uliyotokea kutohukana na kuzuiwa na kukatwa, kufutwa au kuharibiwa kwa sarafu hiyo.

Kumiliki sarafu zilizokatwa

**359.** Mtu ye yoyote ambaye, isivyokuwa halali, anamiliki, au anasarifu unga au vijipande vyovyote vya dhahabu au fedha, au dhahabu au fedha yoyote ya donge, vumbi, maji au iliyo katika hali yoyote nyingine ambayo imepatikana kwa kujihusisha na sarafu ya dhahabu au fedha katika namna ya kupunguza uzito wa sarafu hiyo, kwa kujuwa kwamba vitu hivyo vimepatikana kwa njia hiyo, atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa kifungo cha miaka saba.

Kutoa sarafu za kughushi

**360.** Mtu ye yoyote ambaye anatoa sarafu yoyote ya kughushi, huku akijua kwamba ni sarafu ya kughushi, atakuwa anatenda kosa.

Utoaji uliorudiwa

**361.** Mtu ye yoyote ambaye–

- (a) anatoa sarafu yoyote ya bandia, huku akijua kwamba ni sarafu ya kughushi, na wakati wa kutoa sarafu hiyo anamiliki sarafu nyingine yoyote ya bandia;
- (b) anatoa sarafu yoyote ya bandia, huku akijua kwamba ni sarafu ya kughushi, na, ama kwa siku ile ile au kwa siku yoyote ndani ya siku kumi zinazofuata, anatoa sarafu nyingine yoyote ya kughushi huku akijua kwamba ni sarafu ya bandia ; au
- (h) anamiliki sarafu tatu au zaidi za bandia, huku akizijua kwamba ni za kughushi kwa dhamira ya kutoa mojawapo ya sarafu hizo;

atakuwa anatenda kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka mitatu.

Kutoa nishani au metali kuwa kama sarafu

**362.** Mtu ye yoyote ambaye, kwa nia ya kudanganya, anatoa kama sarafu nishani yoyote au kipande chochote cha metali, iwe ni sarafu au sivyo, ambacho ni cha thamani ndogo kuliko sarafu ambayo ingetolewa, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha mwaka mmoja.

Kusafirisha sarafu za kughushi

**363.** Mtu ye yoyote ambaye, bila mamlaka halali au udhuru, ambapo uthibitisho utakuwa juu yake, anasafirisha au anapakiza katika chombo chochote cha majini au gari la namna yoyote kwa madhumuni ya kuisafirisha kutoka Tanzania, sarafu ya kughushi yoyote iwayo, huku akijua kwamba sarafu hiyo ni ya bandia, atakuwa anatenda kosa.

**364.** Iwapo mtu yejote amehukumiwa kwa kosa chini ya sura hii au sura ya THELATHINI NA SABA, mahakama itaamuru kuhodhiwa katika Jamhuri, noti yoyote ya benki iliyoghushiwa, noti yoyote ya sarafu iliyoghushiwa, sarafu yoyote ya bandia, stempu, kalibu, chombo cha kazi, chombo cha matumizi, mashine, mtambo wa kupigia chapa au sarafu vilivytumika katika utendaji wa kosa hilo.

#### SURA YA THELATHINI NA TISA MIHURI YA KUGHUSHI

Kumiliki kihesi  
kwa madhumuni ya  
kutengeneza mihuri.  
Sura ya 500 kifungu  
cha 12 na 36

**365.** Mtu yejote ambaye, bila ya mamlaka halali au udhuru , ambapo uthibitisho wa hayo utakuwa juu yake–

- (a) anatengeneza au anafanya, au anaanza au anajitayarisha kutengeneza au kubadilisha, au kutumia, au hali akijua kwamba anamiliki, au anasarifu kihesi chochote cha kupiga chapa, bamba au chombo kinachotumika kwa madhumuni ya kutengeneza stempu yoyote, iwe ya moto au ya kubandika, ambayo inatumika kwa madhumuni ya mapato ya umma au ya Shirika la Posta la Tanzania au ya nchi yoyote ya kigeni au ambayo unaweza kutoa, kwenye karatasi, maneno yoyote, tarakimu, herufi, alama au mistari inayofanana na maneno yoyote, tarakimu, herufi, alama au mistari inayotumiwa ndani au nje ya karatasi yoyote maalum iliyotolewa na mamlaka husika kwa ajili ya matumizi yoyote ya namna hiyo;
- (b) hali akijua anamiliki au anatoa karatasi yoyote au kitu kingine chenye alama ya kihesi hicho, bamba au kitu chochote, au karatasi yoyote ambayo ndani au nje yake mna maneno tarakimu, herufi, alama au mistari yoyote iliyorejewa katika aya ya (a);
- (c) kwa udaganyifu, na kwa nia kwamba muhuri au stampu hiyo itumike au sehemu ya stampu hiyo, itumike anatoa stampu kutoka kitu kingine chochote kwa njia yoyote;
- (d) kwa udanganyifu, na kwa nia kwamba sehemu yoyote ya stempu hiyo inaweza kutumiwa, anachana stempu hiyo;
- (e) kwa udanganyifu anabandika au anaweka juu ya kitu chochote au juu ya stempu yoyote hiyo, stempu yoyote au sehemu ya stempu ambayo imeondolewa kwa namna yoyote kutoka kwenye kitu kingine chochote au kukatwa kutoka kwenye stempu nyingine;
- (f) kwa udanganyifu, na kwa dhamira kwamba stempu yoyote inaweza kutumika ambayo tayari ilikwishachapwa au ilikwishabandikwa kwenye kitu chochote anafuta au vinginevyo anabandua kwa hakika au kwa dhahiri, kwenye kitu hicho, kitu chochote kiwacho ambacho kimeandikwa

- juu yake; au
- (g) kwa kujua anamiliki au anasarifu kitu chochote ambacho kimepatikana au kimetengenezwa kwa kitendo chochote kilichokatazwa chini ya aya ya (a) hadi (f); au kama ilivyosemwa hapo juu
  - (h) kwa udanganyifu au kwa dhamira ya kusababisha hasara katika mapato ya umma, yanayotumika kwa dhununi lolote stempu yoyote ambayo anajua ilikwishatumika,,

atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba na kihesi chochote, bamba, mali, karatasi au kitu kingine kama kilichokwikutajwa kwenye kifungu hiki ambacho ameonekana kuwa anacho kitahodhiwa na Jamhuri ya Muungano.

Karatasi na vihesi  
vya kutengenezea  
stempu za posta R.L.  
Sura ya 500 vifungu  
vya 12 na 36

**366.-**(1) Mtu ye yoyote ambaye, bila mamlaka halali au udhuru, ambapo uthibitisho ni juu yake –

- (a) anatengeneza, au anaanza au anatayarisha kutengeneza, au anatumia kwa madhumuni yoyote ya posta, au anamiliki, au anadhibiti au uwakilishi kwenye karatasi au kitu chochote kingine, mfano wa stempu yoyote inayotumiwa kwa kuonyesha kiwango chochote cha posta ya Tanzania au nchi nyingine yoyote ya kigeni; au
- (b) anatengeneza au anabadilisha, au anaanza au inatayarisha kutengeneza au kubadilisha, au anamiliki au anasarifu kihesi chochote, bamba, chombo chochote au zana za kutengenezea kiigizo chochote kama hicho au mfano huo,

atakuwa anatenda kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha mwaka mmoja, au faini ya shilingi elfu moja na stempu zozote au vitu vingine vyovoyote vilivyorejewa katika kifungu hiki ambavyo vimepatikana anamiliki, vitahodhiwa na Jamhuri ya Muungano.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki stempu inayokusudiwa kuonyesha kiwango cha posta cha nchi yoyote itachukuliwa kuwa ni stempu inayotumiwa kwa madhumuni ya posta ya nchi hiyo mpaka itakapoonyeshwa vinginevyo.

### SURA YA AROBAINI KUGUSHI ALAMA ZA BIASHARA<sup>2</sup>

Alama za biashara  
zafafanuliwa

**367.** Alama ya biashara ni–

- (a) alama inayotumiwa kihalali na mtu ye yoyote kuonyesha chombo chochote au kitu cha kutengeneza, ustadi, uzalishaji au bidhaa ya mtu huyo au kuwa ni kitu cha namna ya pekee au cha namna mahsus ambacho kinatengenezwa au kinauzwa na mtu huyo;
- (b) alama au ishara yoyote ambayo kutokana na sheria yoyote

---

<sup>2</sup>Sura ya AROBAINI imefutwa na Sheria ya Alama za bidhaa ya 1963 (Na. 20 ya mwaka 1963 kifungu cha 19)

inayotumika kwa wakati huu, inayohusiana na alama zilizoandikishwa, inatakiwa kuwekwa au kubandikwa kwenye chombo au kitu chochote ndani ya, wakati wa kuwepo au kuendelea kuwepo kwa haki miliki yoyote au haki nyingine ya pekee ambayo imepatikana chini ya sheria hiyo.

Kughushi alama za biashara.  
Sheria Na.19 ya mwaka 2004 Jedw.

**368.** (1)– Mtu yeyote ambaye, kwa dhamira ya kudanganya au kumuwezesha mwingine kumdanganya mtu yeyote, ndio kusema -

- (a) anaghushi au anaiga alama yoyote ya biashara;
- (b) anaweka alama yoyote ya biashara, au alama yoyote ya biadhara iliyoghushiwa au iliyogizwa kutoka, kwenye chombo au kitu chochote ambacho sio bidhaa ya mtu yeyote ambaye alama yake ya biashara imegushiwa au imeigizwa ;
- (c) anaweka alama yoyote ya biashara au alama yoyote ya biadhara iliyoghushiwa au illiyogizwa kwenye chombo au kitu chochote ambacho sio mahsusii au namna ya pekee ya bidhaa inayoonyesha au inayokusudiwa kuonyeshwa na alama hiyo ya biashara au na alama hiyo ya biadhara iliyoghushiwa au kuigizwa;

Sura ya. 85

- (d) anaweka alama yoyote ya biashara au alama yoyote ya biashara iliyoghushiwa au iliyogizwa kwenye kitu chochote kinachokusudiwa kwa madhumuni ya biashara au uzalishaji, au ndani, juu au ambapo chombo au kitu chochote, kinachokusudiwa kuuzwa, au kimeuzwa, au kinatolewa au kinaonyeshwa kwa ajili ya kuuzwa;
- (e) anafungia au anaweka chombo au kitu chochote ndani, juu, chini au pamoja na kitu chochote ambacho alama yoyote ya biadhara imetumiwa uongo au ambapo alama yoyote ya biashara ya kughushi au kuigizwa imetumika;
- (f) anaweka au anaambatanisha chombo chochote au kitu chochote kwenye kasha , kifuniko, kigurudumu, tiketi, alama au kitu kingine chochote ambacho alama ya biashara imetumika kimakosa, au ambapo alama yoyote ya biashara ya uongo au ya kuigizwa imetumika; au
- (g) anafungia, anaweka au anaambatisha chombo au kitu chochote ndani, juu, chini au kwa kitu chochote ambacho juu yake kina alama ya biashara ya mtu yeyote mwingine, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kulipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi na isiyozidi milioni kumi na tano au, kifungo kisichopungua miaka minne na kisichozidi miaka kumi na tano au adhabu zote mbili kwa pamoja.

- (2) Kila mtu anayetenda kosa lililorejewa kwenye kifungu kidogo cha (1) ataihodhisha katika Jamhuri ya Muungano –
- (a) Vyombo na vitu vyote ambapo alama ya biashara au alama ya biashara iliyoigizwa inatumika au iliyofanywa au iliyowekeshwa ili itumike;
  - (b) Anamiliki au iko katika mamlaka yake kila zana ya kuwekea alama ya biashara au alama ya biashara ya kuigizwa
  - (c) Vyombo, vifaa na vitu vilivyotajwa kwenye vifungu nya (d),  
 (e) na (g) ya kifungu kidogo cha (1) na vitu vyote sawa na hivyo ambavyo vilifanywa vitumike kwa namna hiyo katika utaalam au uwezo wake.

### SURA YA AROBAINI NA MOJA KUJIFANYA MTU MWINGINE

Kujifanya mtu mwingine kwa ujumla

Kwa udanganyifu kukubali hati kwa, kuidhinisha, n.k

Kujifanya mtu aliyetajwa kwenye cheti.

Kuazimisha, n.k., cheti kwa kujifanya mtu mwngine

**369.** -(1) Mtu yeoyote ambaye, kwa dhamira ya kumhadaa mtu yeoyote, kwa uwongo anajiwakilisha kuwa ni mtu mwngine, aliye hai au aliyekufa, atakuwa anatenda kosa.

(2) Iwapo uwakilishi huo ni kwamba huyo mkosaji ndiye mwenye haki ya wosia au kwa sheria kupata mali fulani yoyote, na anatenda kosa kupata mali hiyo au kuimiliki, atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

**370.** Mtu yeoyote ambaye, bila ya mamlaka halali au udhuru, ambapo kuthibitisha hayo ni juu yake, anakubali, kwa jina la mtu mwngine yeoyote mbele ya mahakama yoyote au mtu mwenye mamlaka halali ya ukubali huo , ukubali wa wajibu wa aina yoyote , au ukubali wa hati au chombo kingine , atakuwa anatenda kosa.

**371.** Mtu yeoyote ambaye anatoa nyaraka yoyote, ambayo imetolewa na mamlaka halali kwa mtu mwngine na kwamba huyo mtu mwngine anashuhudiwa kuwa ni mtu mwenye sifa inayotambulikana na sheria kwa madhumuni yoyote, au ni mwenye ofisi yoyote, au ni mwenye haki ya kutumia utaalam wowote, biashara au kazi au kuwa anastahili kupata haki au upendeleo wowote, au kutumia cheo au nafasi yoyote, na akajionyesha yeye kuwa ndie huyo mtu aliyetajwa katika hati hiyo, atakuwa anatenda kosa la namna hiyo na atawajibika kwa adhabu kama vile ameghushi nyaraka.

**372.** Mtu yeoyote ambaye, akiwa yeye ndiye aliyepewa nyaraka yoyote iliyotolewa na mamlaka halali ambapo amedhibitishwa kuwa ni mwenye sifa zozote zinazotambulika na sheria kwa madhumuni yoyote, au kuwa ni mwenye ofisi yoyote, au kuwa na haki ya kufanya kazi ya taaluma yoyote, biashara, au kuwa na haki yoyote au upendeleo, au kwa kutumia cheo chochote au hadhi, anauza, anatoa au anaazima nyaraka hiyo kwa mtu mwngine kwa dhamira kwamba huyo mtu mwngine anaweza kujiwakilisha kuwa yeye ndiye mtu aliyetajwa katika nyaraka

Kujifanya mtu  
aliyetajwa kwenye  
udhibitisho wa tabia

Kuazimisha, n.k.  
udhibitisho wa  
kujifanya mtu  
mwingine

Imefutwa

Kujaribu  
kufafanuliwa

Kujaribu kutenda  
makosa

Adhabu kwa  
majaribio ya kutenda  
makosa

Kupuuza kuzuia  
kosa

hiyo, atakuwa anatenda kosa.

**373.** Mtu yejote ambaye, kwa madhumuni ya kutaka kupata kazi yoyote , anatoa nyaraka yoyote yeye asili ya kuthibitishwa kisherai iliyotolewa kwa mtu mwingine, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha mwaka moja.

**374.** Mtu yejote ambaye, ikiwa yeye ndiye ambaye nyaraka yoyote hiyo kama iliyotajwa katika kifungu cha 373 amepewa, anatoa, anaauza au anaazima nyaraka hiyo kwa mtu mwingine kwa dhamira kwamba mtu huyo mwingine anaweza kuitumia nyaraka hiyo kwa madhumuni ya kupata kazi yoyote , atakuwa anatenda kosa.

### SURA YA AROBAINI NA MBILI MATENDO YA SIRI

**375.-379.** [ Vimefutwa na R.L. Sura ya. 400 kifungu cha 15.].

*Kigawo cha NANE – Majaribio, Njama za kutenda Uhalifu, Kuficha  
Uhalifu na Ushawishi na Uchochezi*

### SURA YA AROBAINI NA TATU MAJARIBIO

**380.** -(1) Iwapo mtu kwa nia ya kutenda kosa, anaanza kuweka nia yake hiyo katika utekelezaji kwa njia ya kutimiza nia hiyo, na anaonyesha dhahiri kwa kitendo kilicho wazi, lakini hawezi kutimiza nia yake kwa kiasi cha kutenda kosa, atachukuliwa kujaribu kutenda kosa.

(2) Haijalishi, isipokuwa kuhusiana na adhabu, kama mkosaji amefanya yote ambayo ni muhimu kwa upande wake kukamilisha kutenda kosa, ama iwe kumaliza kutimiza nia yake kumezuiwa na mazingira yaliyo nje na matakwa yake , au iwe amejizuia mwenyewe kuendelea kutekeleza nia yake .

(3) Haijalishi kwamba kwa sababu ya mazingira ambayo hayafahamiki kwa mkosaji ni vigumu kutenda kosa.

**381.** Mtu yejote ambaye anajaribu kutenda kosa, atakuwa na hatia ya kosa ambalo, anawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka miwili au faini au adhabu zote kwa pamoja, isipokuwa kama adhabu nyingine imetolewa.

**382.** Mtu yejote atakaejaribu kutenda kosa la namna ambalo mtu akitenda na kuhukumiwa atapaswa kuhukumiwa adhabu ya kifo au kifungo cha muda wa miaka kumi na nne au zaidi, na au bila adhabu nyingine, atakuwa ametenda kosa na atahukumiwa adhabu ya kifungo cha miaka saba kama hakuna adahabu tofauti iliyoelekezwa.

**383.** Kila mtu ambaye anajua kwamba mtu fulani anaazimia kutenda au anatenda kosa, na akashindwa kutumia kila njia inayofaa ya kuzuia utendaji au ukamilishaji wa kosa, atakuwa anatenda kosa.

### SURA YA AROBAINI NA NNE

## NJAMA

Njama ya kutenda kosa linaloadhibiwa kwa kifungo cha miaka mitatu au zaidi

Njama ya kutenda kosa linaloadhibiwa kwa kifungo kisichozidi miaka mitatu

Njama nyaginezo. Sheria Na 5 ya mwaka 1971 Jedw la pili

**384.** Mtu yejote ambaye anakula njama na mtu mwingine katika kutenda kosa lolote, ambalo linaadhibiwa kwa kifungo cha kipindi cha miaka mitatu au zaidi, au kutenda kitendo chochote katika sehemu yoyote ya dunia ambalo kama limetendeka Tanzania lingekuwa ni kosa ambalo linaadhibiwa, na ambalo ni kosa chini ya sheria zinazotumika katika sehemu ambayo limefanyika, atakuwa anatenda kosa, na atawajibika, kama hakuna adhabu nyingine iliyotolewa, kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba au, iwapo adhabu kubwa kabisa ambapo mtu huyo amehukumiwa kwa kosa husika ni ndogo kuliko kifungo cha miaka saba, basi kwa adhabu hiyo ndogo kuliko.

**385.** Mtu yejote ambaye anakula njama na mtu mwingine katika kutenda kosa ambalo linaadhibiwa kwa kifungo cha kipindi kisichopungua miaka mitatu, au kufanya kitendo chochote katika sehemu yoyote ya dunia ambalo kama limetendeka Tanzania lingekuwa ni kosa ambalo linaadhibiwa, na ambalo ni kosa chini ya Sheria zinazotumika katika sehemu ambayo imependekezwa kufanyika, atakuwa anatenda kosa.

**386.** -(1) Mtu yejote ambaye anakula njama na mtu mwingine ili kutimiza lolote katika madhumuni haya yafuatayo, ndio kusema – .

- (a) kuzuia au kupinga utmilizaji au utumikaji wa Sheria yoyote;
- (b) kusababisha dhara lolote kwa mtu au sifa ya mtu yejote au kushusha thamani ya mali yoyote ya mtu yoyote;
- (c) kuzuia au kukinga uuzaji huru na wa halali wa mali yoyote ya mmiliki ili kupata thamani inayostahili kwa mali hiyo;
- (d) kumdhuru mtu yejote katika biashara au taaluma yake; au
- (e) kuzuia au kukinga, kwa njia yejote tendo lolote au matendo yejote ambayo kama yatafanywa na mtu yatasababisha kosa kwa upande wake, uendeshaji huru na wa halali wa mtu katika biashara, taaluma au nafasi yake ya kazi;
- (f) kutimiza madhumuni yoyote yasiyokuwa halali; au
- (g) kutimiza madhumuni yoyote ya halali kwa njia yoyote isiyokuwa halali, atakuwa anatenda kosa.

(2) Kwa kuropa mashaka, inatamkwa kuwa mume na mke wanawenza kuwa na hatia ya kula njama pamoja, iwe ndoa yao ni ndoa ya mke moja au ni ndoa ya wake wengi.

## SURA YA AROBAINI NA TANO WAFICHAJI UHALIFU

Ufanuzi wa wafichaji uhalifu

**387.** - (1) Mtu ambaye anampokea au anamsaidia mtu mwingine ambaye, kwa ufaamu wake, anatenda kosa, , ili kumuwezesha mtu huyo mwingine kuropa adhabu, ni mfichaji mhalifu wa kosa hilo.

(2) Mke hatakuwa mfichaji uhalifu wa kosa ambalo mumewe ndiye amelitenda kwa kumpokea au kumsaidia mumewe ili kumuwezesha kuropa adhabu; au kwa kupokea au kusaidia kuwepo mbele ya mumewe na kwa ruhusa ya mumewe, mtu mwingine ambaye

anatenda kosa utendaji ambao mumewe alishiriki, ili kumuwezesha huyo mtu mwingine kuепuka adhabu; wala mume hatakuwa mfichaji uhalifu wa kosa ambalo mkewe ametenda kwa kumpokea au kumsaidia mkewe ili kumuwezesha kuепuke adhabu.

**388.** Mtu yejote ambaye anakuwa ni mfichaji wa uhalifu wa kosa linaloadhibiwa kwa kifungo cha miaka mitatu au zaidi, atakuwa anatenda kosa, na atawajibika, kama hakuna adhabu nyingine iliyotolewa, ya kifungo cha miaka saba.

**389.** Mtu yejote ambaye anakuwa mfichaji uhalifu wa kosa linaloadhibiwa kwa kifungo kisichopungua miaka mitatu atakuwa anatenda kosa.

#### SURA YA AROBAINI NA SITA USHAWISHI NA UCHOZEZI

Kushawishi au  
kuchochea  
utendekaji wa kosa.  
Sheria Na. 47 ya  
mwaka 1954  
.kifungu cha 2.

**390.** Mtu yejote ambaye anamshawishi au anamchochea mtu mwingine kutenda kosa, atakuwa anatenda kosa bila kujali kwamba ushawishi au uchozezi huo hauna madhara.